**23 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Hamsini – Tarehe 23 Juni, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jerry William Slaa Mbunge wa Ukonga sasa aulize swali lake.

Na. 439

**Kutenga siku ya kutoa huduma kwa wateja kwenye Ofisi za Dar es Salaam**

**MHE. JERRY W. SILAA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga siku za kutoa huduma kwenye ofisi za Dar es Salaam ili kupunguza gharama kwa wateja wanaosafiri kufuata huduma Dodoma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuhamishia ofisi za Makao Makuu yake Dodoma, bado huduma zote zimeendelea kupatikana Dar es Salaam kama ilivyo kwa mikoa mingine nchini.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa umma zitaendelea kuimarishwa na kutolewa katika maeneo yote nchini ikiwemo Dar es Salaam. Pamoja na hayo, Serikali inaendelea na maboresho ya mifumo ya utoaji huduma kwa umma kwa njia ya kieletroniki ili kupunguza ulazima wa wateja kusafiri au kufuata huduma hizo ofisini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry William Slaa swali la nyongeza

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa iliyoifanya ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma. Naomba nitumie fursa hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ziko taasisi yakiwemo mashirika ya kimataifa na nchi wahisani ambazo bado shughuli zake zinafanyia Dar es Salaam.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuweka siku maalum za viongozi wakuu wa Wizara kwa maana Waziri na Katibu Mkuu kuwa Dar se Salaam kwa ajili ya mazungumzo nao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya kodi inakusanywa katika mkoa wa Dar es Salaam.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuweka kitengo cha *tax investigation* Dar es Salaam ili kuwapunguzia wafanyabiashara adha ya kuja Dodoma kila wakati kufuatilia matatizo ya kodi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jerry William Silaa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya Serikali tunapokea pongezi hizi za Mheshimiwa Mbunge kwa Serikali kuhamia Dodoma; lakini vile vile nami nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya kuwatetea wana Jimbo la Ukonga na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza tunapokea maoni yake na ushauri na tutayafanyia kazi ili Serikali iendelee kuwatembelea wadau walioko Dar e Salaam kama ilivyo pia kwa wadau wengine katika mikoa mingine yote nchini. Tunashukuru kwa ushauri Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa swali lake la pili, nipende kulihakikishia Bunge lako, kwamba ile *department* inayohusika na mambo ya *tax investigation* iliyopo Mamlaka ya Kodi Tanzania ambayo ipo chini ya Kamishna Mkuu wa TRA ofisi yake iko nchi nzima hadi ngazi ya wilaya. Hivyo kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi Serikali kuhamia Dodoma haimaanishi kuhamisha au kusitisha huduma zake katika mkoa wa Dar es Salaam. Utendaji wa idara utakuwa kama ilivyo kwa idara zingine zenye wadau wengi maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mifano ya nchi ambazo zina miji mikubwa yenye idadi kubwa ya watu lakini bado makao makuu yake ya nchi yameendelea kuhamishwa na wameendelea kufanya vizuri. Mfano Lagos ni mji mkubwa wa Nigeria kwa idadi kubwa ya watu na biashara na ndiko kuna walipa kodi wengi, lakini Makao Makuu ya Serikali na taasisi zake zipo Jijini Abuja. Pia Pritoria ni Mji Mkuu wa Serikali wa Afrika Kusini, lakini mji mkubwa wenye biashara na idadi kubwa ya watu ni Johannesburg. Kwa hiyo sisi kama Serikali kwa kuwa tumehamia Dodoma bado tutaendelea kutoa huduma kwa wananchi kama kawaida. Niendelee kuwahamasisha watu waendelee kuja na kuwekeza katika Jiji la Dodoma ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana yaliyotolewa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Ndarienanga, na nimpongeze kwa majibu hayo; nimetaka kusimama hapa kwa umaalum kabisa kutoa msimamo wa Serikali juu ya kuhamisha makao makuu kuja Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya maamuzi haya mwaka 1973, na maamuzi haya yamekuwa katika Ilani za Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kwa miaka yote. Nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza maamuzi haya; na hivi sasa tunavyozungumza taasisi zote muhimu ikiwa pamoja na Ikulu zinakamilisha majengo yake makubwa Wizara zote zimepewa fedha na Bunge limetenga takriban bilioni 20 kwa kila Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita na majengo yanaendelea. Ukienda kule mji wa Serikali ni maajabu yanatokea na watu wanatakiwa kuja kuona Tanzania ambavyo tunatekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini zipo taasisi ambazo mpaka leo hii zinasitasita kuhamia Dodoma; vilevile wako watu wanaofikiria fikiria kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan hapendi Dodoma. Ninataka niliseme hili wazi kwa sababu maneno haya ni kumsingizia Rais. Anatekeleza kwa vitendo tumeendelea kutenga bajeti na mpaka hata bajeti hii tumetenga kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu. Fedha inayoingia Dodoma ni nyingi sana kuliko mikoa yote kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niwahakikishie Watanzania na nataka niwahakikishie wana Dodoma na hasa wale wazee wa *one way,* kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hana makusudi yoyote ya kurejesha Makao Makuu Dar es Salaam. Makao Makuu ni Dodoma na Serikali inawekeza vya kutosha, tuna miradi mingi mikubwa ambayo mikoa mingine hawajapata. Tuna kila sababu wana-Dodoma, na sasa nizungumze kama mwanadodoma siyo tena Waziri, kwamba tuna kila sababu ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu kwa sababu ya uamuzi huu na anavyoendelea kuusimamia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo taasisi zote ambazo zinasitasita kumalizia kuhama ninapata tathmini wiki hii na wiki ijayo nitatoa tamko la nini kifanyike kwa wale ambao bado wanajiulizauliza; lakini Serikali itaendelea kufanyakazi katika mikoa yote *equally*. Kama ilivyo kwa mkoa wa Dodoma na mikoa mingine Serikali ipo. Kama kuna shughuli maalum kama hii ya kodi au kitengo cha *investigation* hata mikoa mingine wanahitaji na kuna wafanyabiashara watakwenda huko kama ni *ad hocly* au kutakuwa na kuna vitengo hivyo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu Mheshimiwa Kungu karibu uulize swali.

Na. 440

**Hitaji la vifaa – Kituo cha Afya Mtakanini – Namtumbo**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba katika Kituocha Afya cha Mtakanini – Namtumbo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA**

**SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi TAMISEMI naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Jimbo la Namtumbo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga Shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini kote. Kati ya fedha hizo Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imetengewa shilingi milioni 450 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika vituo vya afya kikiwemo Kituo cha Afya cha Mtakanini ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza swali la kwanza;

Kwa kuwa kituo hicho cha afya cha Mtakanini kilikamilika ujenzi wake mwanzoni mwa mwaka 2020 na kinaendelea kutoa huduma jamopokuwa kina upungufu wa vifaa tiba na kupelekea usumbufu wa wagonjwa wengi kupata rufaa kwenda hospitali ya Songea mjini.

Je, Serikali itakamilisha lini ama itafanikisha lini ununuzi wa vifaa tiba na kupeleka kwa haraka zaidi katika kituo hicho?

Swali la pili, katika kituo cha afya cha Nakapanya Tarafa ya Nakapanya Wilayani Tunduru jengo la upasuaji limekamilika na vifaa vipo kwa asilimia 85.

Je, Serikali itakamilisha lini vifaa hivyo ili huduma ya upasuaji ipatikane katika kituo kile cha Nakapanya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu Mbunge wa Jimbo la Tunguru Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hiki Kituo cha Afya cha Mtakanini Wilayani Namtumbo kimekamilika mwanzoni mwa mwaka 2020, na Serikali hii sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujali umuhimu wa kituo hicho kuanza kutoa huduma za afya mapema iwezekanavyo tumetenga milioni 450 kwa ajili ya vifaa tiba, ambavyo mwezi Julai mwezi ujao huu vitapelekwa *MSD* na vifaa hivyo vitapelekwa Mtakanini ili huduma za afya zianze.

Kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshalifanyia kazi hilo nii suala la muda mfupi vifaa vitafika kwa ajili ya kutoa huduma.

Lakini kuhusiana na Kituo cha Afya cha Nakapanya ambacho kimekamilika na vifaa tiba kwa asilimia 85, nikuhakikishie pia katika Halmashauri ya Tunduru mmetengewa fedha za vifaa tiba kwa ajili ya kukamilisha vituo ambavyo vina vifaa tiba kwa kiasi kidogo lakini pia vile ambavyo havina ili vianze kutoa huduma za afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy John Sabu swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii.

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba katika kituo cha afya cha Mwabayanda wilayani Maswa katika jengo la *mortuary*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Lucy John Sabu Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Mwabayanda nacho kimekamilika. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika vituo vya afya ambavyo vimekamilika ifikapo 30 Juni mwaka huu vyote vimetengewa fedha kwa ajili ya kununua vifa tiba ambapo jumla bilioni 47.7 imetengwa. Kwa hiyo Kituo cha Mwabayanda pia nacho ni sehemu ya vituo ambavyo vimetengewa fedha hiyo ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Jimbo la Kilolo lina jumla ya vituo vya afya vitatu pamoja na zahanati tisa ambazo zimekamilika na nyingine zina zaidi ya mwaka mmoja. Je, ni lini vifaa tiba vitapelekwa ili vituo vya afya hivyo na zahanati ziweze kuanza kufanyakazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga Mbunge wa Jimbo la Kilolo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha jumla ya shilingi bilioni saba zimetengwa kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba kwenye zahanati zilizokamilika kwa awamu ya kwanza zikiwemo zahanati ambazo zipo kwenye Jimbo la Kilolo. Pia jumla ya shilingi bilioni 47.7 zimetengwa kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba kwenye vituo vya afya vya awamu ya kwanza na ya pili, vikiwemo vituo hivi vya Jimbo la Kilolo. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba Serikali inalifanyia kazi mwaka ujao wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kilwa Kaskazini tuna kituo cha afya cha Tingi katika kituo cha afya kile kuna upungufu mkubwa wa vifaa tiba hasa katika wodi ya wazazi, wodi ya wagonjwa mchanganyiko na tatizo *la x-ray*.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya upatikanaji wa vifaa hivyo tiba katika kituo hiki cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Tingi na vituo vingine ambavyo viko kwenye awamu ya kwanza na ya pili ya ukamilishaji vimetengewa fedha kwa ajili ya vifaa tiba. Kwa hivyo nielekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kuleta andiko ili tujue kituo hiki kiko awamu ya kwanza au ya pili. Kama kipo awamu hizo nikuhakikishie kwamba kipo kwenye mgao wa kupata fedha kwa ajili ya vifaa tiba, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Wyclife Makamba swali la nyongeza.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi; na mimi naomba niulize. Kituo cha Afya cha Kambarage Kata ya Chamaguha kilichopo katika Jimbo la Shinyanga Mjini kinahudumia wananchi wengi lakini kinakabiliwa na changamoto kubwa sana ya vifaa tiba. Nini mpango wa Serikali kupeleka vifaa tiba katika vituo hivi viwili vya afya vilivyopo katika Jimbo la Shinyanga mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salome Makamba Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha vituo vya afya vilivyokamilika vinapata vifaa tiba ili vitoe huduma stahiki. Kwa hiyo Kituo cha Afya hiki cha Kambarage ambacho nakifahamu, ni cha siku nyingi, na kwa kweli kinahudumia wananchi wengi sana; nikuhakikishie kabisa tutakipa kipaumbele kipate vifaa tiba ili kitoe huduma bora zaidi. Pia Kituo cha Afya cha Maguha tutakiona kama kipo awamu ya kwanza au ya pili ili kiweze kupata mgao wa vifaa tiba ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi wananchi wa Mafinga mjini wanaishukuru Serikali kwa ujenzi wa kituo cha afya cha Ifingo na Bumilayinga hata hivyo wanauliza;

Je, ni lini Serikali italeta vifaa ili huduma zianze kutolewa katika halmashauri hizo katika Vituo hivyo vya Ifingo na Bumilayinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi Mbunge wa Jimbo la Mafinga mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, vituo hivi ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja nimevipokea, tumevichukua kama Serikali na tutakwenda kuona uwezekano pia wa kupata fedha

kwenda kununua vifaa tiba hivyo kwa awamu hii au kwa awamu ijayo kulingana na vigezo ambavyo tumeviweka, ahsante.

**SPIKA**: Mheshimiwa Nashon Bidyaguze swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru; naomba kumuuliza;

Je, ni lini Serikali itapeleka shilingi milioni 10 katika kituo cha Kazulamimba ambayo ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano Mheshimiwa Magufuli?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nashon Bidyanguze kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ahadi za viongozi wetu wa kitaifa sisi tunazichukua kama maelekezo na tunaziwekea mpango mkakati ili kuhakikisha zinatekelezwa mapema iwezekanavyo. Ninakumbuka kweli tuna ahadi hii ya milioni 10 Kazuramimba. Nikuhakikishie kwamba tumeshaanza mchakato ikiwemo Unyarioba kule kwa Mheshimiwa Mbunge Muhambwe, lakini pia Kigoma Vijijini. Kwa hiyo maeneo haya yote ambayo ni ahadi za Waheshimiwa viongozi wetu wa kitaifa tunazifanyiakazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Katani Katani swali la nyongeza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI aliwahi kufika Nata ya Nanyanga ambako wananchi wamejitolea kujenga kituo cha afya. Alipofika akajiridhisha kwamba wananchi wale wanapaswa kusaidiwa na Serikali na akawaahidi kuwapa fedha kukamilisha ujenzi ule.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kata ya Manyanga kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Katani Katani, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Nanyanga kwa kuitikia wito wa Serikali wa kutoa nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya…

**SPIKA:** Mimi nadhani ni Mbunge wa Tandahimba; asije akasikia Mheshimiwa Abdallah hapa, ikawa mtihani.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni Mbunge wa Jimbo la Tandahimba.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wananchi kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na ni kweli Mheshimiwa Waziri alifika pale. Nimhakikishie kwamba mpango wa Serikali katika Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi ni kuchangia nguvu za

wananchi. Tutatafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono nguvu za wananchi katika ujenzi wa kituo hicho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma Xaday, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kituo cha Afya Hirbadaw kimepelekewa watumishi mwaka 2021 na hakina vifaa tiba: Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kupeleka vifaa tiba ili watumishi wale waweze kufanya kazi iliyotarajiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eng. Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hiki cha Afya ambacho kipo awamu ya pili ni miongoni mwa vituo ambavyo vimetengewa fedha na ninakumbuka tulikuwa kwenye Ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwezi wa pili, ni sehemu ambayo tulikubaliana kwamba lazima tulete vifaa tiba. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba Serikali inalifanyia kazi jambo hilo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamgha, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kutujengea Kituo cha Afya cha Mugitu, Wilaya ya Hanang: Je, ni lini Serikali sasa itatuletea vifaa tiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamgha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Kituo hili cha Afya cha Mugito ni miongoni mwa vituo ambavyo Serikali imeweka mpango wa kutafuta fedha ili kupeleka vifaa tiba kupitia *MSD* ili kiweze kutoa huduma bora za afya kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Swali langu ni dogo. Tunashukuru Serikali kwamba imetupa fedha, Shilingi milioni 500 kukarabati Kituo cha Afya cha Kirua Vunjo, lakini fedha hizi hazijatosheleza kujenga vyumba vya *Ultrasound* na *X-Ray machines*: Je, Serikali iko tayari kutuongezea fedha kidogo tu kukamilisha suala hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nipokee pongezi zake kwa Serikali yetu kwa kupeleka Shlingi milioni 500 ambayo ilikuwa ni kilio cha

muda mrefu cha wananchi wa Jimbo la Vunjo, na kituo kimekarabatiwa, kipo kwenye kiwango kizuri. Nimhakikishie kwamba safari ni hatua, tutatafuta fedha kwa ajili ya kujenga jengo la *X-Ray*. Kuhusu jengo la *Ultrasound,* nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi kuhakikisha wanatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la *Ultrasound* kwa sababu lipo ndani ya uwezo wao. *X-Ray,* tutatafuta fedha Serikali Kuu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Malum, sasa aulize swali lake.

Na. 441

**Hitaji la Masoko ya Madini – Ulanga**

**MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini wa Ulanga kupata masoko ya uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa lengo la kuwasaidia wachimbaji wadogo na kuhakikisha wanapata soko la uhakika, ilifungua Soko la Madini na Kituo cha Ununuzi wa Madini eneo la Mahenge, Wilaya ya Ulanga. Hadi Mei, 2022, Soko la Madini Mahenge lilikuwa na jumla ya wanunuzi wakubwa wa madini ya vito *(dealers)* wapatao 50, na katika Kituo cha Ununuzi wa Madini, Mahenge kulikuwa na jumla ya wanunuzi wadogo wa madini *(brokers)* wapatao 99. Katika Soko la Madini Mahenge kuna changamoto ya kutokuwepo kwa wanunuzi wakubwa wa madini ya dhahabu kutokana na uzalishaji wake kuwa mdogo, hivyo, kutowavutia wanunuzi wakubwa wa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha wanunuzi wakubwa wa madini kuwekeza katika Soko la Madini Mahenge na kupandisha hadhi, tumeamua kama Wizara ya Madini kwamba katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 tumepanga kuipandisha hadhi Ofisi ya Afisa Migodi Mkazi *(MRO)* Mahenge kuwa Ofisi ya Afisa Madini Mkazi *(RMO)* ili kurahisisha upatikanaji vibali vya kusafirisha madini kwenda nje ya nchi na kuongeza wigo wa kutangaza rasilimali madini zilizopo ili kuvutia wawekezaji na hivyo kuongeza uzalishaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Mzeru, swali la nyongeza.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Je, Serikali ina mpango gani wa kugawa maeneo mapya kwa wachimbaji wadogo wadogo wa madini, Malinyi Ulanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: Ni nini mpango wa Serikali kuwawezesha wachimbaji kwa mikopo, kwani wachimbaji wengi wana mitaji duni sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kugawa maeneo mapya ya uchimbaji kwa wachimbaji wa Wilaya ya Ulanga au Mkoa wa Morogoro kwa ujumla, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Wilaya ya Ulanga peke yake mpaka sasa Wizara imegawa leseni 171 kwa wachimbaji wadogo na tutaendelea kufanya hivyo kadri maeneo yatakavyokuwa yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwa yale maeneo yenye leseni kubwa za utafiti kuna eneo moja linaitwa Lukande ambapo wachimbaji wadogo walioanza kufanya uchimbaji katika eneo hilo lenye leseni ya utafiti tuliingia kwenye maridhiano na mwenye leseni akatenga maeneo 26 ambayo wamepewa vikundi na watu mmoja mmoja ambao hadi sasa zaidi wa wachimbaji wadogo wadogo 500 wamefaidika na eneo hilo. Tutaendelea kutenga maeneo kadri ya uwepo wa madini unavyobainika katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, kuhusu uwezekano wa kupatikana mitaji au mikopo ya kuwawezesha wachimbaji wadogo, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpaka sasa Wizara ya Madini imeendelea kuelimisha benki zetu hapa nchini juu ya *potential* kubwa iliyopo katika sekta ya madini na uwezekano wa kukopesheka kwa wachimbaji wadogo. Sasa hivi Benki za *NMB, KCB, CRDB* na *NBC* wameshakopesha wachimbaji wadogo zaidi ya Shilingi bilioni 38.

Mheshimiwa Spika, kana kwamba hiyo haitoshi, tumeendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo waweke kumbukumbu za takwimu ya mauzo yao, sambamba na uzalishaji wao, maana hicho ndicho kigezo kimoja muhimu ambacho benki zinataka kuona, wajue kama wakikopeshwa wana uwezo wa kurejesha mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na utaratibu wa Serikali mwaka 2012 mpaka 2014 ya kuwapa wachimbaji wadogo mikopo. Wachimbaji wengi walitumia vibaya ile mikopo wakaipeleka kwenye maeneo mengine, Serikali ikasitisha mpango huo na ndiyo sasa ikaja na huu mpango wa kuhamasisha benki za ndani ziweze kuwakopesha, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu limeshajibiwa.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Jimbo la Isimani Mkoa wa Iringa kuna machimbo ya Nyakavangala ambapo wachimbaji wadogo wanachimba dhahabu; je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia masoko wachimbaji hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mikoa yote ya madini nchini, Serikali kupitia Wizara ya Madini imeanzisha masoko ya madini na vituo vya kuuza na kununua madini. Katika eneo la Isimani alilolisema, sisi kama Wizara tukishaona uzalishaji kwamba unakidhi vigezo, tunakwenda kuanzisha kwa kuanzia kituo cha kuuza na kununua madini pale pale kwa *brokers* lakini baadaye madini yale yanakwenda kwa *dealers* katika soko ambalo lipo katika kila Mkoa wa Madini nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatafutia soko la uhakika wachimbaji wadogo wa Ruby katika Wilaya ya Longido?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia na makusudi ya Wizara ya Madini ni kuhakikisha kwamba popote pale katika nchi yetu palipo na hazina hiyo ya madini na uzalishaji unaendelea, masoko huanzishwa na vituo vya kuuza na kununua huanzishwa. Wafanyabiashara wa madini kutoka ndani na nje ya nchi kupitia mikutano mikuu ya madini ambayo huwa tunaandaa, kama tulivyokuwa na Mkutano wa Kimataifa mwezi wa Pili wa kutangaza fursa za madini, wanatambua fursa hizo, na hivyo

wanafahamu maeneo ya kwenda kupata yale madini. Kwa njia hiyo tunafanya *promotion* na *marketing* ya rasilimali ili wachimbaji wadogo wapate masoko ya bidhaa zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Wachimbaji wengi hawana dhamana: Serikali ina mpango gani wa kuwakopesha ma- *excavator*, makarasha na vifaa vingine vya uchimbaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwakang'ata, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilijaribu mwaka 2012 mpaka 2014 kutoa mikopo, lakini baadaye kwa sababu ya wachimbaji kutokuwa waaminifu na kupeleka ile mikopo pasipohusika, utaratibu huo ulikoma. Huu utaratibu sasa wa kutumia benki za ndani baada ya kuwapa elimu, nasi kuwapa vitalu wachimbaji wa madini na kuwatambua wale waliopewa leseni kama *brokers* au *dealers,* tukaweka utaratibu wa hawa wahusika wa biashara hizi za madini kwenda kwenye hizo taasisi za ndani. Wakitimiza vigezo, watapewa mitaji. Benki nyingine zipo tayari kutoa fedha, wengine wanatoa vifaa au vyote kwa pamoja. Kwa hiyo, hiyo fursa ipo wazi, ni suala la kuzingatia vigezo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara

ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 442

**Hitaji la Masoko ya Samaki ukanda wa Pwani**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itajenga Soko la kisasa la wavuvi katika Ukanda wa Pwani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo ya Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha na kujenga masoko ya mazao ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo ukanda wa Pwani. Aidha, kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa Soko la Samaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.8. Awamu ya kwanza ya ujenzi huo tayari imeanza mwezi Februari, 2022 ambapo gharama iliyotumika hadi sasa ni Shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Spika, masoko yaliyopangwa kujengwa katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi kwa mwaka 2022/2023 ni pamoja na Soko la Samaki la Kipumbwi, Wilayani

Pangani Mkoani Tanga litakalogharimu shilingi 1,241,247,753. Soko hilo litaambatana na ujenzi wa chumba cha baridi chenye uwezo wa kuhifadhi tani 40 za samaki na kusimika mtambo wa barafu kwa gharama ya shilingi 259,194,802. Vilevile kupitia Programu Maalum ya Uchumi wa Bluu na Programu ya Mkopo wa Masharti Nafuu kutoka *IMF,* Serikali imepanga kujenga masoko mapya katika maeneo ya Somanga na Kilwa Kivinje, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Serikali wameahidi kwenda kujenga masoko mengine ya Samaki; na kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022 walituahidi pia kwenda kujenga Soko la Samaki Kikumbwi katika Mkoa wa Tanga; je, ni lini sasa Serikali itakwenda kujenga soko hilo la samaki katika Wilaya ya Pangani Kata ya Kikumbwi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ina mapango wa kujenga masoko mengi ya Samaki: Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha wanakwenda kufunga miamba ya kuvutia samaki ili kuongeza uzalishaji? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lini tutajenga? Tutakwenda kujenga katika mwaka huu wa fedha, mara baada ya kuhama na fedha zile katika mwaka uliokwisha tunaoumaliza wa 2021/2022. Kuhusu mpango gani tulionao ili kuongeza rasilimali hii ili tuweze kwenda sambamba na ujenzi huu wa masoko; tunakwenda kujenga hizi *Fish Aggregating Devices (FATs),* ni miamba isiyokuwa ya asili, na tayari hatua ya kiutafiti ya wapi tutakapokwenda kuweka miamba ile imeshakamilika. Kwa hiyo, tunasubiri mpango wa bajeti ya mwaka huu ukamilike na utekelezaji uanze mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa soko hili la Bagamoyo gharama yake ni karibu Shilingi bilioni 2.8 na mpaka sasa zimetumika Shilingi bilioni 1.6; na nina imani kabisa katika bajeti ya mwaka huu Serikali itamalizia fedha hizi: Je, ni lini sasa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi italeta *cold rooms*, chanja za kuanikia samaki pamoja na vifaa vingine vya kisasa kwa ajili ya kuendeleza soko hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muharami, Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2022/2023 tunaouendea, katika programu tulizonazo ni pamoja na vichanja vya kukaushia samaki. Hivyo basi, nitoe rai kwa Mheshimiwa Mbunge kuweza kuwapanga wavuvi wake wa

pale Bagamoyo kuwa tayari kuweza kuitumia fursa hii, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na kukosekana kwa masoko ya kisasa ya Samaki, kuna tatizo kubwa sana la kukosekana vyumba vya baridi ambayo inapelekea wavuvi kuuza samaki hata kwa bei ndogo kwa kushindwa kuwahifadhi. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ana mkakati gani wa kujenga vyumba hivyo hasa katika Majimbo ya Mtwara Vijijini na Mtwara Mjini ambako tuna wavuvi wengi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba moja ya jambo linalotusumbua kwa kiasi kikubwa katika tasnia hii, ni juu ya upotevu wa mazao yetu *(post harvest loss)* mara baada ya kuwa wamevuliwa samaki hawa. Moja ya mkakati tulionao ni kuhakikisha kwamba tunajenga vyumba hivi. Vile vile pamoja na kujenga vyumba hatua inayofuata ni kununua vichanja ili wale watakaokuwa wameshindwa kupata fursa ya kuingia kwenye *cold chain,* basi waweze kukaushwa vizuri ili waweze kwenda kuwa na ubora utakaoweza kuwahudumia watu.

Mheshimiwa Spika, tunayo programu ambayo itakwenda kujenga baadhi ya maeneo. Naomba nilichukue jambo hili la Mtwara Vijijini na Mtwara Mjini ili tuweze kuona namna ya

kuweza kuwa-*accommodate* na ninyi ili muweze kunusuru mazao haya, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Napenda kufahamu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo ni lini atakwenda kuangalia eneo ambalo wananchi wa Kata ya Manda wameliandaa kwa ajili ya kujengewa soko la mazao ya samaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kamonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Bunge la Bajeti. na kwa kuwa Halmashauri ya Ludewa tayari imeshachagua eneo, tupo tayari sasa kuhakikisha mara moja tutakwenda kwa ajili ya kuliona na harakati na utaratibu wa kiujenzi uweze kuendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Je, ni lini mwalo na soko letu la samaki katika Kata ya Mchinga litajengwa kwa kuwa wataalam wameshakwenda zaidi ya mara mbili; sasa nataka kujua, lini soko hili litajengwa katika Kata yetu ya Mchinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la mama yangu, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba taratibu za kimanunuzi zimekwishaanza na mara baada ya kukamilika taratibu hizi tunakwenda kujenga mwalo huu wa pale Mchinga na bajeti yake iko tayari na fedha zipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Katika Kata ya Mbweni kuna eneo kubwa ambalo wavuvi wanavua kiholela na kusababisha Serikali kukosa mapato. Je, ni lini Serikali itajenga soko hilo ili tuweze kupata mapato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felista Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mbweni na kwenyewe wako wavuvi na mapato ya Serikali yanapotea, naomba katika programu hii kubwa tuliyonayo, tunayo pia programu ya *SWIOFish* ambayo inahudumia na Dar es Salaam. Kwa hivyo naomba nilichukue jambo hili, tutakwenda kulizungumza na wataalam wetu na kuona namna ambavyo tunaweza kuifanya Mbweni kuwa ni sehemu ya watakaonufaika na miradi hii ya ujenzi wa masoko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 443

**Mchezo wa Kamari**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwanusuru vijana wanaoshiriki mchezo wa kamari kwa matarajio ya kupata fedha ya haraka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba jamii yetu inalindwa dhidi ya madhara yanayoweza kusababishwa na uwepo wa michezo ya kubahatisha inayosimamiwa na Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41, pamoja na kanuni zake, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania inatekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Kutoa elimu ya kwa umma kuhusu michezo ya kubahatisha ambapo inasisizitizwa kuwa michezo hiyo ni burudani na siyo mbadala wa ajira;

(ii) Kuwaelekeza waendeshaji wa michezo hii kuzuia ushiriki wa mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18 na wachezaji wanaobainika kuelekea kwenye uraibu; na

(iii) Kufanya ukaguzi kwa kampuni zinazoendesha biashara ya michezo ya kubahatisha ili kuhakikisha zinaendesha michezo hiyo kwa mujibu wa sheria, taratibu na miongozo ya Bodi.

Mheshimiwa Spika, Bodi itaendelea kusimamia na kuiratibu Sekta ya Michezo ya Kubahatisha ili iendelee kuchangia ipasavyo katika uchumi wa nchi yetu bila kuleta madhara kwa jamii, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni umefika wakati wa maeneo yale ambayo yanafanya biashara ya michezo ya kubahatisha kufunguliwa saa kumi jioni ili kuwanusuru wale vijana au wananchi ambao wamekuwa wakishinda huko tangu asubuhi waweze kufanya kazi na kujiingizia kipato?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kumekuwa na baadhi ya wananchi ambao wamekuwa wakiendesha michezo ya bahati nasibu kwa kutumia karata maeneo mbalimbali nchini na hivyo kuwaibia wananchi wengi. Je, nini kauli ya Serikali kwa ajili ya hawa wanaowaibia baadhi ya wananchi wetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu maswali hayo naomba nimpongeze sana mama, Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa maswali yake mazuri yanayoonesha kujenga na malezi ya watoto wetu. Swali lake la kwanza ni shauri, shauri lake kwa kuwa tunajua lengo la mama ni ulezi, tunalichukua na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kauli ya Serikali; tunatoa wito kwa wale wote ambao wameona watu wanacheza michezo haramu kutoa taarifa zao haraka iwezekanavyo katika vituo vyetu vya polisi, lakini Serikali inalifanyia uchunguzi pia suala hilo na tutalifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Michezo hii ya bahati nasibu kule vijijini imeleta mmomonyoko mkubwa wa maadili kwa vijana na watoto na usimamizi wake umeachwa kwenye Bodi ya Michezo ya Kubahatisha pekee, kule kwenye Serikali za Mitaa wameonekana hawajahusishwa na hakuna taratibu zinazowasukuma kusimamia michezo hii. Je, ni nini kauli ya Serikali kuwapa mamlaka Serikali za Mitaa kusimamia michezo hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwamba Serikali inachukua mapendekezo hayo na kushusha Bodi iweze kufanya kazi mpaka katika Serikali za Mitaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu wamekuwa wakijiingiza katika michezo ya bahati nasibu hasa nyakati za masomo. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ambao muda wa masomo wao wanakwenda kucheza michezo ya bahati nasibu na hivyo kupoteza muda wa masomo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Paulina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme nalo tunalifanyia uchunguzi, kama kweli wanafunzi wetu wa vyuo vikuu wanashiriki katika

mchezo huu haramu, basi Serikali itatoa tamko rasmi hatua gani zichukuliwe kwa vijana hao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu rekebisha kidogo hapo; huu mchezo wa bahati nasibu ni mchezo haramu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, mchezo wa bahati nasibu siyo haramu, lakini hao vijana ambao wanacheza kwao ni haramu.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, sasa aulize swali lake.

Na. 444

**Fidia kwa wananchi wa Kata za Mbasa na Katindiuka – Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, ni lini wananchi wa Kata za Mbasa na Katindiuka watalipwa fidia kwa kupisha ujenzi wa barabara inayoelekea Malinyi na Ulanga?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuhuisha taarifa ya uthamini ambayo itahuisha mali zilizomo katika eneo la barabara na mita 60 linatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Julai, 2022. Zoezi hilo litakapokamilika kazi ya ulipaji wa fidia itaanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaasa wananchi hao kutoa ushirikiano wakati zoezi la kuhuisha taarifa ya uthamini likiendelea. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa kujenga barabara kutoka Njombe kuelekea Makete, lakini wananchi wa Ramadhani na Tandala, hasa Shule ya Msingi ya Lupalilo, hawajapewa fidia hadi leo.

Je, ni lini Serikali itawapa fidia ili shule hii tuweze kujenga eneo lingine na wanafunzi wetu waendelee na masomo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kuna baadhi ya wananchi na baadhi ya taasisi ambazo hazijalipwa fidia kati ya barabara ya Makete kwenda Njombe. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tathmini imeshafanyika na tayari imeshafikishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo

kinachosubiriwa sasa hivi ni kutafuta fedha ili wananchi hao na taasisi zilizoathirika ziweze kulipwa fidia hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara kuu itokayo Masasi kuelekea Nachingwea, uthamini wake umekamilika na hivi karibuni itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami baada ya kupatikana pesa, lakini wananchi wa Kata za Chikunja na Lukuledi walifanyiwa uthamini kwa muda mrefu sana na mpaka sasa hawajalipwa fidia ya mali zao zilizoko pale.

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza ambacho kitafanyika ni ku-*review* tathmini ya ile fidia na wakati Serikali itakapoanza ujenzi kitu cha kwanza itakuwa ni kuwalipa fidia wananchi watakaoathirika kupisha barabara hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Barabara ya Itoni – Lusitu ambayo karibu inaanza ujenzi na wao vilevile

bado hawajalipwa fidia. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, sikusikia barabara aliyoitaja Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Itoni – Lusitu, Njombe, wananchi bado hawajalipwa fidia na barabara hiyo karibu inaanza ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Itoni – Lusitu ndiyo kwanza imetangazwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi watakaoathirika wa Itoni – Lusitu kwamba Serikali ilishafanya tathmini na wananchi hao watalipwa wakati wowote fedha itakapopatikana na hasa kwa sababu ndiyo tunaanza ujenzi, kipaumbele kitakuwa ni kuanza kuwalipa kwanza hao wananchi wa eneo la Itoni – Lusitu. Ahsante.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza katika swali langu la msingi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari, inabidi uulize moja kama Wabunge wengine kwa sababu hukusimama mwanzo.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, sawa na nakushukuru sana. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kuwa mchakato wa upembuzi utaanza mwishoni mwa mwezi Julai. Wananchi wanataka kujua, ni lini mchakato huo utakamilika na pengine lini watalipwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini ikishakamilika tutaanza kulipa hiyo fidia. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tushirikiane na kuwaelimisha wananchi kwamba tunachohitaji ni wao kutoa ushirikiano, wakitoa ushirikiano haraka kazi inakuwa ni rahisi na mara baada ya kukamilisha, basi Serikali itatafuta fedha na kuwalipa wananchi hao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Serikali imeshapata fedha za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mnivata – Nanyamba – Tandahimba – Masasi; je, ni lini Serikali italipa fidia kwa waathirika wa ujenzi wa barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii barabara ambayo inafadhiliwa na *African Development Bank* ndiyo kwanza tunategemea tuanze kuijenga pengine kuanzia mwezi Septemba au Oktoba. Naomba niwahakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi watakaopisha ujenzi huo kwamba watalipwa fidia kabla ya kuanza kwa ujenzi wa barabara hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi. Barabara ya kutoka Kibirashi – Chemba – Kwamtoro, Singida ina zaidi ya miaka 27 tangu ilivyotangazwa na Serikali. Wananchi walisimamishwa kuendeleza makazi yao kwa ajili ya kupisha ujenzi huo wa barabara. Nataka kujua, je, ni lini Serikali itafanya uthamini na kuwalipa wananchi wa Kata za Mrijo, Songolo, Goima, Chemba mpaka Kwamtoro, Farkwa, Kinyamshindo na kuunganisha Singida? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti Majala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara aliyoitaja ya Handeni – Kibereshi – Kwamtoro – Singida kama alivyoitaja na kata zinazohusika ilifanyiwa tathmini, lakini kabla ya kuanza kulipa

wakati wa kuanza kuijenga ni lazima tutafanya *review* ya tathmini kwa sababu ni sheria inatuambia hivyo. Tukishafanya sasa *review* ya tathmini, wananchi hao watalipwa kulingana na fidia ya wakati itakapoanza kujengwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali yanayotoka kwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Sasa nilete matangazo tuliyonayo hapa mbele kabla hatujaendelea na ratiba yetu na mambo mengineyo.

Waheshimiwa Wabunge wanaozunguka na Wabunge wanaozungumza, sasa ni muda wa kusikiliza.

Tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika; wapo wageni wa Bunge ambao ni ujumbe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, yupo Mheshimiwa Jacques Kyabula ambaye ni Gavana wa Katwe, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia Mheshimiwa Aertes Joseph Kayumba, huyu ni Waziri wa Kilimo; Mheshimiwa Said Mshana ambaye ni Balozi wa Tanzania Nchini *DRC;* Ndugu Selestine Kakele ambaye ni Konsela Mkuu Lubumbashi; Ndugu Sylvie Chanvula ambaye ni mkalimani; Ndugu Joris Johana, Msaidizi wa Gavana; Ndugu Jos Mabondane, Msaidizi wa Gavana; Ndugu Consolate Kandja Ngadi, Mwandishi wa Habari wa *DRC;* na Ndugu Momat Kilonda Emmanuel ambaye ni Mwandishi wa Habari pia kutoka *DRC,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa wageni hawa kutoka *DRC* wameambatana na wenyeji wao ambao ni Ndugu Gerald

Mweli, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Herman Berege ambaye ni Afisa Mambo ya Nje Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, karibu sana.

Yupo pia Ndugu Mwanaasha Ngenya ambaye ni Afisa Mambo ya Nje Mkuu. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimejulishwa hapa kwamba Gavana tuliyemtangaza Mheshimiwa Jacques Kyabula ni Gavana wa Jimbo la Haut-Katanga lakini wao wameandikwa Katwe, kwa hiyo ni Haut – Katanga, karibu sana Gavana wetu na pole kwa kukosea Jimbo unaloliongoza. Balozi atakuwa anafanya hapo tafsiri kama wanaongea Kifaransa ama na Kiswahili nadhani wanaweza kuwa wanasikia pia hawa Ndugu zetu sana Wakongo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo mengine niliyonayo hapa mbele, moja linatoka kwa Katibu wa Bunge ambae anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba mnakaribishwa kutembelea banda la vijana wa Kitanzania wenye Kampuni inayoitwa *Veritable Complete Motors* yenye Ofisi Dar es Salaam na Uingereza, kampuni hii inajihusisha…

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza nikiwa nimesimama.

Kampuni hii inajihusisha na uuzaji na uagizaji wa magari binafsi, magari ya biashara, magari ya huduma za jamii na wagonjwa pamoja na vifaa vya kilimo na ujenzi wapo kwenye viwanja vya Bunge mnakaribishwa kwenda kuwatazama siku ya

leo wapo hapo nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, mnakaribishwa sana kwenda kuwaona.

Waheshimiwa Wabunge, pia mnatangaziwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq - Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Masuala ya UKIMWI anawatangazia kwamba hawa vijana wetu tuliowatangaza hapa wa *dreams* wanalo banda linaloeleza shughuli wanazozifanya na pia namna walivyojengewa uwezo wa kujieleza na kujiamini na pale mtapata nafasi ya kujifunza pia tabia hatarishi na namna ya kupambana na *VVU*. Kwa hiyo, mnakaribishwa pia na wao banda lao lipo maeneo hayo ya nyuma ya jengo letu la Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo niliombwa Mwongozo ambao sasa nataka kuusema hapa. Mwongozo huu uliombwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi kuhusu kauli iliyotolewa dhidi yake na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Tarehe 21 Juni, 2022 katika Mkutano wa Saba wa Bunge, Mkutano wa Bajeti, Kikao cha 48 Mheshimiwa Godwin Kunambi aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika maelezo yake Mheshimiwa Kunambi alilalamikia kauli iliyotolewa dhidi yake na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambayo alidai imemvunjia heshima yake kama Mbunge na hivyo kutaka kupata ufafanuzi kama jambo hilo linahuruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Kiti kilielekeza kuwa kitatoa majibu hapo baadaye baada ya kuzipitia Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kwa mujibu wa Kanuni ya 76. Jambo hili lilitokana na mchango wa Mheshimiwa Kunambi wakati

akichangia katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo katika mchango wake alielezea namna sekta ya ardhi inavyoweza kuongeza wigo wa kodi. Pamoja na mambo mengine aliongelea faida za kupanga na kupima ardhi kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, ninanukuu "Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya Kwanza, tunakuwa na matumizi bora ya ardhi kama nchi, kila eneo linakuwa limepangwa; Pili, kuiongezea ardhi thamani na kuifanya kuwa mtaji; Tatu, kuziongezea mapato Halmashauri zetu; Nne, kufanikisha zoezi la anuani za makazi''.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kunambi aliendelea kutoa mchango wake na kueleza mafanikio yake yaliyotokana na jinsi alivyosimamia jukumu la kupima na kupanga ardhi wakati alipokuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, alisema kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye *success story* hapa Dodoma, miaka mitatu, minne iliyopita Dodoma Jiji nilikabidhiwa jukumu la kupima na kupanga Dodoma. Mtakumbuka siku moja nikiwa nahudumu kama Mkurugenzi wa Jiji Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniita ofisini nikiwa na Mstahiki Meya na Afisa Mipango Miji wangu akiniuliza ni lini utagawa viwanja kwa Watumishi wa Umma. Sikumuomba fedha, sikwenda benki kukopa, nilimjibu nipe miezi mitatu naenda kukabidhi viwanja kwa Watumishi wa Umma. Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Dodoma mpaka ninaondoka ninahitimisha utumishi wangu wa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma niliacha viwanja takribani 400,000 na nilitumia njia gani? Naomba niseme kidogo.

Niliwaita watalaam wangu yaani *Management Team* nikawaambia wanishauri, sasa wengi walisema tupime wenyewe nikachukua eneo la Michese viwanja 2,000, walinikabidhi viwanja hivyo kwa muda wa miaka mitatu nikatumia sekta binafsi nikapima viwanja zaidi ya 390,000 kwa sekta binafsi. Sasa hii naielezea kwa sababu ni *success story*".

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Kunambi akiendelea na mchango wake alisimama Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi nakuomba kutoa taarifa. Baada ya kuruhusiwa na Kiti Waziri alitoa taarifa kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ninaomba Msemaji anapozungumza asitupe *story* ambazo sasa hivi ndizo zinatuletea matatizo kwa nchi hii. Akiwa Mkurugenzi wa Dodoma kama anavyosema, tulikuwa na *story* ya Kinondoni kuongoza migogoro, sasa hivi Kitaifa Dodoma inaongoza kwa dhuluma ambazo wamezifanya kwa wananchi. Kwa hiyo, huo siyo mfano ambao anaweza akautolea kama *success story* kwenye kazi aliyoifanya." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii ndiyo iliyosababisha Mheshimiwa Kunambi kuomba Mwongozo wa Spika ambapo pamoja na mambo mengine alisema: nanukuu "Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limenipotezea heshima yangu kama Mbunge, neno dhuluma ni tuhuma nzito sana. Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa kuwa limenipotezea heshima kama Mbunge, lakini pia na wananchi wangu wa Jimbo la Mlimba na kwa kuwa neno hili limeingia kwenye *Hansard* ya Bunge mimi bado ni kijana, kutakuwa na rekodi mbaya huko mbele ya yanayonihusu. Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mambo mawili jambo la kwanza ninaomba Mwongozo wako Mwenyekiti kama jambo hili linaruhusiwa na kama linaruhusiwa

au haliruhusiwi ninaomba athibitishe au afute kauli hii ili *Hansard* za Bunge mimi kama Mbunge heshima yangu kwa kweli imevunjika, ahsante. Waheshimiwa Wabuge mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard)* na kusoma maelezo ya pande zote mbili, nilijielekeza kutaka kujua kama jambo linalolalamikiwa linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni zetu, na kama haliruhusiwi ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyorekebishwa Wabunge wanao uhuru wa mawazo na majadiliano wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kibunge. Aidha, masharti ya Ibara hiyo yametiliwa mkazo katika kifungu cha 3 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge yaani *the Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, Cap 296 Revised Edition 2020.* Hivyo, kwa kuzingatia masharti ya Katiba na Sheria Mbunge anao uhuru wa kutoa mawazo na maoni wakati wa majadiliano katika Bunge, uhuru huo hautahojiwa na mtu au chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au mahali pengine popote nje ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mchango wa Mheshimiwa Kunambi ulijielekeza katika umuhimu wa kupima na kupanga ardhi nchini ili kuhakikisha kuwa faida za matumizi bora ya ardhi zinapatikana. Aidha, katika mchango wake alieleza namna alivyoshiriki kwenye zoezi hilo wakati alipokuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, ni maelezo hayo yaliyomwinua Mheshimiwa Waziri kuomba taarifa na katika taarifa yake zaidi

ya kueleza kwamba kilichofanyika Dodoma siyo mfano wa *success story* kwenye kazi aliyoifanya Mheshimiwa Kunambi bali pia alitumia maneno yafuatayo na nanukuu; "Ninaomba msemaji anapozungumza asitupe *story* ambazo sasa hivi ndiyo zinatuletea matatizo kwa nchi hii." Aidha aliendelea kusema nanukuu; "Sasa hivi kitaifa Dodoma inaongoza kwa dhuluma ambazo wamezifanya kwa wananchi. Kwa hiyo, huo siyo mfano ambao anaweza akautolea kama *success story* kwenye kazi aliyoifanya."

Waheshimiwa Wabunge, maneno hayo yanaingilia uhuru wa mawazo na majadiliano wa Mheshimiwa Kunambi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyolalamika maneno hayo hayaleti taswira nzuri kwa nafasi yake kama Mbunge na kwa wananchi anaowawakilisha na aliowahi kuwahudumia alipokuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma. Aidha, hayo si maneno yanayoruhusiwa katika mijadala ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 71(1)(i) na (j), Kanuni zetu za Bunge Fasili hizo nilizozitaja zinazuia kumsema vibaya Mbunge na matumizi yasiyo sahihi ya lugha ya kumdhalilisha Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hivyo, haikuwa sahihi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutamka kuwa ilifanyika dhuluma kwa wananchi. Endapo kuna dhuluma ilifanyika kuna vyombo vinavyoweza kuchunguza na kuthibitisha madai hayo na hatua stahili zikachukuliwa. Kwa mantiki hiyo Mwongozo wangu ni kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, maneno hayo hayaruhusiwi na hivyo haikuwa sahihi kwa Mheshimiwa Waziri kuyatamka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika maombi yake Mhehimiwa Kunambi aliomba kwamba iwapo maneno ya Mheshimiwa

Waziri hayaruhusiwi yafutwe kwenye *Hansard*. Hivyo naelekeza kuwa maneno yanayolalamikiwa yafutwe kwenye *Hansard* ya tarehe 21 Juni, 2022 kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020.

Waheshimiwa Wabunge huo ndiyo mwongozo wangu kwenye hoja hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa hapa kuna wageni lakini naambiwa hawajaingia bado watakapofika nitawatangaza.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo hapa muhimu kwa ajili ya siku ya Jumamosi na tangazo hili linatoka kwa Katibu wetu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Benki ya *CRDB* imeandaa bonanza la michezo kwa ajili ya Wabunge, sasa siku mbili tuseme kesho kwa maana ya Tarehe 24 lakini pia siku ya Tarehe 25. Sasa nianze na yale yatakayotokea siku ya Tarehe 24 kwa maana ya kesho. Saa Saba na Nusu mchana katika Ukumbi wa Msekwa kutakuwa na semina kwa Wabunge wote ambayo imeandaliwa na *CRDB* Benki na Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana kuhudhuria semina hii kwa sababu itazungumzia masuala ya uwekezaji hasa yale yanayoratibiwa na Benki ya *CRDB*. Kwa hiyo mnaalikwa wote Saa Saba na Nusu mchana kesho kuhudhuria Semina hii.

Pia kwa siku ya Jumamosi kutakuwa na bonanza la michezo kati ya Bunge, *CRDB* na wadau mbalimbali katika utaratibu ufuatao:-

Kwanza, Saa Kumi na Mbili Asubuhi mazoezi ya kutembea yataanzia Bungeni kuelekea Uwanja wa Jamhuri, halafu kutakuwa na mazoezi na ufunguzi rasmi wa michezo mbalimbali utakaoendelea katika Uwanja wa Jamhuri. Pia, kutakuwa na

mchapalo kwa Wabunge na washiriki wote utakaofanyika kuanzia Saa Kumi na Mbili Jioni katika viwanja vya Bunge hiyo ni siku ya Jumamosi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, inatarajiwa kwamba Spika atakuwa Mgeni Rasmi katika haya matukio yote. Kwa hiyo, mnaombwa sana Waheshimiwa Wabunge siku ya kesho msikose kwenye semina lakini pia siku ya Jumamosi kwenye michezo ila tangazo hili tutalirejea kesho pia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo tunaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu. Katibu!

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*Muswada wa* Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2022 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2022)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu malizia na huo mwingine.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 *(The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Miswada yetu imeshasomwa kwa mara ya kwanza na hivyo itapelekwa kwenye Kamati zinazohusika. Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH– KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhangama, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza kabisa niungane na Wabunge wote kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Taifa hili, pia nipongeze uandishi na uandaaji wa bajeti hii ya mwaka 2022/2023 ni wa kipekee na unajibu hoja nyingi sana za wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitajikita kwenye eneo moja tu na niombe sana Mheshimiwa Bashe aniazime sikio lake. Tunapoongelea kilimo kwangu mimi ninaongelea mambo mawili muhimu, kitu cha kwanza kilimo ni tija lakini kitu cha pili kilimo ni soko. Tunapoongelea kilimo ni tija tunamaanisha ufanisi katika kilimo, ni kiwango gani cha mahindi, ni kiwango gani cha

maharage, ni kiwango gani cha parachichi, mihogo, kahawa unaweza kuvuna katika eneo la ekari moja. Kiwango unachokivuna ukilinganisha na gharama ulizowekeza unapopata faida ndipo tunapozungumzia tija na faida zinapozidi kuwa kubwa ndiyo tija inakuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lini tunapata tija kwenye kilimo? Ni pale ambapo tunatumia teknolojia sahihi za kilimo, teknolojia sahihi za kilimo ni zipi nitaongea mambo manne. Kitu cha kwanza tunapoongelea teknolojia sahihi za kilimo ni mbinu bora za kilimo; Pili, tunaongelea dhana bora na sahihi za kilimo; Tatu, tunaongelea pembejeo bora na sahihi za kilimo; Nne, tunazungumzia huduma za ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili la tija mahsusi kabisa kwenye eneo la teknolojia za kilimo maeneo mawili tumefanya vizuri sana ukilinganisha na maeneo mengine, eneo la huduma za ugani tumefanya vizuri na hapa nimpongeze sana Waziri wa Kilimo amejitahidi sana na kutoa vitendea kazi, ikiwemo pikipiki, vifaa vya kupimia udongo, vishikwambi, amefanya vizuri sana na Bunge hili lazima limpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kudhubutu eneo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo tumefanya vizuri ni mbinu bora za kilimo. Kwenye mazao mengi na maeneo mengi ya nchi yetu tumefanya vizuri kwenye mbinu bora za kilimo. Leo Mikoa ya Mbeya, Songwe, Katavi, Rukwa, Kigoma, Kagera, Iringa, Njombe na Ruvuma huwafundishi kulima mahindi; wanajua *spacing,* wanajua aina ya mbegu ya kutumia. Wanajua aina gani ya mbolea waitumie kwenye uzalishaji wa kilimo. Kwa hiyo kwenye hayo maeneo mawili tumefanya vizuri sana na tunaendelea kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado tuna maeneo makubwa mawili ambayo tuna changamoto nayo sana, na Mheshimiwa Waziri hili anisaidie kulifanyia kazi. Moja, tuna eneo la zana bora za kilimo na eneo la pili pembejeo. Changamoto ni nini? Changamoto ya kwanza kwenye eneo la upatikanaji wa tija kwenye kilimo ni mitaji ya kilimo. Mitaji ambayo itamsaidia mkulima kupata dhana bora za kilimo. Kupata matrekta, kupata vifaa vya kilimo, kupata pembejeo na kadhalika; mitaji katika kilimo. Hili kwa upande wa Serikali tumejaribu kwa sehemu fulani, nadhani wote tunajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki yetu ya *TADB* ilikusudiwa kwenda kutatua tatizo la mitaji kwenye kilimo ili wakulima wadogo na wakubwa wapate mitaji, vitendea kazi, zana za kilimo na pembejeo. Hata hivyo, Benki yetu ya Kilimo ambayo ilikusudia kutatua tatizo la tija bado ina changamoto kubwa mbili.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwanza benki yenyewe haina mtaji wa kutosha. *TADB* hakuna mtaji wa kutosha. Nilikuwa najaribu kufanya *analysis* hapa, mtaji mzima wa *TADB,* ninaambiwa, kama nimekosea mtanirekebisha. Mtaji mzima wa Benki ya *TADB*, Benki ya Kilimo ni shilingi bilioni 268. Shilingi bilioni 268 hizi; na kama *assumption* zetu ziko sahihi, kwamba nchini Tanzania asilimia 60 ya Watanzania wanaishi kwa kutegemea kilimo, wanalima, *it means* kama kila Mtanzania atakopa kwa ajili ya kilimo kutoka kwenye benki hii atapata shilingi 7,000 tu kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, mtaji huu ni mdogo sana, huwezi kuleta mapinduzi ya kilimo kwa kutegemea mtaji mdogo kama huu kwa Benki ya Kilimo. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, mimi ninakuamini sana Mheshimiwa Bashe, wewe ni mpambanaji, ni mpiganaji; umeweza kutafuta fedha zaidi ya bilioni 600 kuongeza kwenye bajeti yako ya kilimo, kitu ambacho

hakikuwepo huko nyuma. Unaweza kwenda kutafuta fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye Benki hii ya Kilimo; inahitaji fedha nyingi, fedha zilizopo ni kidogo sana. Ukiweza kutatua tatizo hili, utatatua tatizo la tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo lina changamoto kwa benki yetu ni Sera ya Mikopo ya *TADB*. Hivi leo Sera ya Mikopo ya *TADB* kwa sehemu kubwa kwenye utekelezaji wake inafanana na *Commercial Bank,* inafanana na benki ya *CRDB, NMB* na benki zingine. Benki hii haikukusudiwa iwe benki ya biashara za kawaida, ilikusudiwa iwe benki ya uwekezaji. Kama ningeruhusiwa kubadilisha jina na kupendekeza jina ningependekeza benki hii iitwe *Tanzania Agricultural Investment Bank* na siyo *Tanzania Agricultural Development Bank* kwa sababu tunapoteza *focus. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda kuangalia mitaji, mikopo inayotolewa na benki hii ni mikopo ya muda mfupi sana. Pamoja na kwamba kwenye taarifa umeona kwamba wamesema, ni vizuri, wanatoa sijui zana za kilimo, wanatoa kwa maana ya matrekta, wanatoa kwenye pembejeo. Lakini ukienda kuangalia *volume* ya fedha zinazokwenda kwenye mikopo ni zile za muda mfupi zinazohusu kununua mazao leo, uyauze kesho. Hiyo haiwezi kuwa benki ya maendeleo ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo kinahitaji muda. Mimi naongea sitaki kutangaza maslahi yangu katika ujumla, lakini mimi pia ni mkulima kama wakulima wengi wa Tanzania. Kilimo kinaanza mwezi wa sita au wa saba, ndiyo maandalizi ya kilimo. Lakini mkopo kwenye kilimo unaupata mwezi wa 12 halafu unatakiwa ulipe mwezi wa sita. Hiyo haiwezi kuwa benki ya maendeleo ya kilimo. Uwekezaji kwenye kilimo unahitaji muda. Kwa hiyo, kama kuna kazi ya kufanya Mheshimiwa Waziri naomba ukafanye kazi

ya kubadilisha Sera ya Mikopo ya Benki ya Kilimo. Tafuta mtaji wa kutosha peleka kwenye benki ile ndiyo utapata *agricultural transformation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, peleka fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa zana, peleka fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa mikopo ya muda mrefu, wanunue matrekta miaka mitano waweze kurudisha,ndiyo hiyo inakuwa *investment*. Na kwa kufanya hivi Mheshimiwa Waziri utaweza kuleta majibu ya ajira nchi hii.

Mheshimiwa Spika, na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, amesema katika sekta hii ya kilimo amekusudia kuajiri vijana milioni tatu. Vijana milioni tatu unawaajiri vipi Mheshimiwa Waziri? Hautawaajiri kwenye kulima mahindi na maharage pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana hawa utawaajiri kwenye mnyororo mzima wa kilimo, na mnyororo mzima wa kilimo tunaongea kwanza uzalishaji wa kilimo. Vijana wakipata mitaji ya muda mrefu watazalisha mazao ya kilimo, hiyo ni sehemu moja. Lakini sehemu ya pili utawaajiri kwenye eneo la huduma za ugani, vijana wetu wengi wana ujuzi wa kilimo utawaajiri kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo utawaajiri hawa vijana milioni tatu, utawatengenezea ajira, ni kwenye eneo la usambazaji wa pembejeo. Eneo hili la pembejeo ni muhimu sana na ni sekta muhimu sana kwa kukuza kilimo. Kwa hiyo, kama sera haziruhusu sekta hiyo kukua huwezi kupata vijana hao milioni tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna eneo la *aggregation* ya mazao na *postharvest management*. Vijana wanaweza

kuwekeza kwa wingi kwenye eneo hilo. Pia tuna eneo la *value addition,* kwa maana ya *processing,* vijana wana *intrest* na eneo hilo lakini uwekezaji bado ni mdogo kwenye eneo hilo. Eneo jingine tungesema ni uendeshaji wa mifumo ya masoko, kwa maana ya maghala haya yetu tunahitaji ma-*operators* wa maghala, hayo ni maeneo mengi ambayo kama Mheshimiwa Waziri ataongeza umakini, na mimi uwezo najua anao, mkubwa; ukaongeza fedha kwenye Benki hii ya *TADB*, akabadilisha sera au uka-*implement* sera inavyotakiwa, kwamba mikopo itolewe kwa muda mrefu, ataweza kutatua changamoto ya ajira na atachangia kwenye utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia isiyopungua 40, sekta yako peke yako. Kama akikaa vizuri na Mheshimiwa Mashimba Ndaki watachangia takriban asilimia 100 kwa sababu ilani yetu inataka tuzalishe ajira zaidi ya milioni nane, na yeye tayari kwenye *stock* yake amekusudia kufikia asilimia 40 kwa maana ya ajira milioni tatu; hapo atafaulu. (*Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba niishie hapo na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge humu Bungeni kama nilivyosema, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi anayemgeni wake ambaye ni Mwenyekiti wa CCM, Kata ya Nyasho, anaitwa Fidelis Manyerere. Haya karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Stella Ikupa Alex atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia na mimi hoja iliyopo mbele yetu. Kabla sijaendelea naomba niunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya ulinzi wake kwangu lakini pia na kwa jinsi anavyoendelea kutulinda Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani na viongozi wetu wakuu pamoja na wananchi wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jitihada kubwa ambazo anaendelea kuzifanya katika kuvutia wawekezaji, kwa ajili pia mpango ulioletwa mbele yetu wa elimu bila malipo mpaka kidato cha sita pamoja na ongezeko la mishahara kwa watumishi. Pia kuendelea kuimarisha sekta ya usafiri wa anga kwa kuendelea kununua ndege.

Mheshimiwa Spika, mambo yakupongeza ni mengi ambayo yamefanywa na Mheshimiwa Rais wetu. Itoshe tu kusema ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi; na kubwa tuendelee tu kumuombea Mheshimiwa Rais afya njema lakini pia hekima pamoja na maarifa ya kuendelea kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kuchangia ninaomba niipongeze Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)*. Utabiri ambao umekuwa ukitolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania sasa hivi umekuwa ni utabiri ambao ni wa kuaminika na wakutegemewa sana tofauti na miaka ya nyuma. Hivyo wajibu wetu kama Watanzania ni kuutilia sana maanani utabiri huu wa hali ya hewa kwa sababu yale ambayo yemekuwa yakitabiriwa ndiyo ambayo yamekuwa yakitokea. Hasa

tukianzia kwa mwaka huu, utabiri wa hali ya hewa ulisema kwamba mvua zitakuwa chache kwa maeneo mengine lakini maeneo mengine hayatakuwa na mvua kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona wakulima wengi walilima mimi mwenyewe nikiwemo mazao yamekauka. Pale mwanzoni ilionesha kama kuna nuru kidogo ya mvua kwa hiyo, tukajipa moyo wakulima lakini mwisho wa siku mazao yamekauka.

Mheshimiwa Spika, nini nataka kushauri? Nataka niishauri Serikali kuendelea kuwaelimisha wananchi kuhifadhi chakula. Kwa sababu inavyoelekea ni kwamba kutakuwa kuna ukosefu wa chakula kwa sababu mazao yamekauka. Kwa hiyo, kwa yule ambaye ana chakula basi aendelee kukihifadhi na si kuuza chakula chote ambacho anacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kuchangia ninaomba niongelee masuala ambayo nimeombwa niyaongelee na kundi ambalo ninalisimamia, kundi la watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu wameniomba niiombe Serikali kupunguza kodi kwenye biashara wanazozifanya. Biashara ambazo zimeanzishwa kwa uwezeshaji wa Serikali kupitia mikopo ambayo inatolewa na halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini wanaomba wapunguziwa kodi? Wako wafanyabiashara ambao wanafanya biashara za bajaji lakini pia wengine wamefungua maduka. Kwa kuwa hizi biashara ni mkopo, wanajikuta wanashindwa kurejesha mikopo kwa wakati kwa sababu kodi imekuwa ikiwabana. Hivyo wameniomba niiombe Serikali iwapunguzie kodi katika biashara wanazozifanya ili basi waweze kufanya *serving* ya kulipa mikopo lakini pia kuendelea kuendesha maisha yao na kufungua biashara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wameniomba niongelee suala la matibabu. Wakati tunasubiri mpango wa bima ya afya kwa wote, wameniomba niiombe sana Serikali iweke utaratibu mzuri na utaratibu maalum wa kuweza kuwatibia katika kipindi hiki ambacho tunasubiri mpango wa bima ya afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wameniomba niongelee suala la elimu, kwa maana mikopo ya elimu ya juu. Ninaishukuru Serikali kwamba imeweka utaratibu wa elimu bila malipo mpaka kidato cha sita. Lakini tukiangalia kundi hili la watu wenye ulemavu ni wachache sana ambao wanapata fursa ya kufika mpaka elimu ya juu. Hivyo Serikali ina uwezo kabisa wa kuwapa mikopo hii badala ya kuwa mikopo iwe ni ruzuku.

Mheshimiwa Spika, kwa nini? Wanapomaliza vyuo na kuanza kazi maisha yanaendelee kuwaelemea kwa sababu upande huu wanadaiwa kodi, yaani ile kodi ya kawaida ambayo tunakatwa kwenye mishahara; lakini pia wakati huohuo wakatwe ile mikopo wanayodaiwa, wanunue vifaa saidizi ama kuwalipa wasaidizi wanaowategemea. Hivyo wameniomba sana niliongelee suala hili na kuiomba Serikali yetu iweze kuliangalia kwa kina jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niongelee suala la asilimia mbili. Mwaka huu kama ilivyo ada ya miaka mingine inavyofanyika pale *New York* Marekani ulifanyika mkutano mkubwa wa kujadili mkataba wa haki za watu wenye ulemavu *(Convention on the Rights of Persons with Disabilities)*. Miiongoni mwa mambo mengi yaliyojadiliwa, lilijadiliwa suala la uwezeshaji wa watu wenye ulemavu kiuchumi. Na Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi ambazo zimeridhia mkataba huu, iliweza kueleza ni kwa jinsi gani inawezesha watu wenye ulemavu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, asilimia mbili haikuweza kuachwa nyuma. Ilizungumziwa kwa kina kwamba ni kwa jinsi gani Tanzania inaliwezesha kundi hili na asilimia mbili ya watu wenye ulemavu ni kwa jinsi gani inawawezesha watu wenye ulemavu kumudu maisha yao na kuanzisha biashara mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu ni ukombozi, kwa sababu wengi tunaona wameweza kuachana na kuombaomba na kuwa tegemezi. Sasa kwa jinsi ambavyo ninamfahamu Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan na kwa jinsi anavyotupenda sana sisi watu wenye ulemavu, tumeshuhudia na tumeona kwa macho na kwa matendo, ni Mama ambaye anatupenda sana na kutujali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamuomba aliangalie suala hili kwa jicho la pili na jicho la tatu. Kwa sababu tunaona katika halmashauri na manispaa mbalimbali, mimi nimekuwa nikipigiwa simu mara kwa mara, watu wenye ulemavu wamekuwa wakiniomba nifuatilie mikopo ambayo wameiomba. Na unaweza ukaangalia, na ninapopiga simu *either* kwa Mkurugenzi ama Mkuu wa Wilaya unakuta naambiwa kwamba Mheshimiwa maombi ni mengi ya mikopo hii lakini fedha ni chache. Kwa hiyo, tunaweza tukaona kwamba kumbe hata hii asilimia mbili yenyewe haitoshi bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niiombe Serikali iweze kuona; na sina shaka na Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, na sina shaka na Mheshimiwa Rais wangu Samia Suluhu Hassan; kwamba jambo hili ataliangalia kwa jicho la pili na la tatu na kwa kweli ataendelea kuongeza tena uwezeshaji wa kundi hili la watu wenye ulemavu ili waendelee kujitegemea na

hatimaye kutegemewa na jamii ambayo inawazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache, ninaomba niunge mkono hoja tena kwa mara ya pili na pia ninaomba niipongeze sana hotuba ambayo iko mbele yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba hii nzuri ambayo kwa kweli inaenda kujibu changamoto nyingi za Watanzania, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo atafuatiwa na Mheshimwia Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ambayo ni bajeti kuu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa bajeti ambayo imewasilishwa kwetu ambayo inaleta matumaini makubwa sana kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na viongozi wote ambao wameshiriki kuandaa bajeti hii. Mimi nina ushauri kwenye maeneo machache. Nianze na hii mikopo ya halmashauri ambayo wanataka kupunguza.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali isiguse kabisa eneo hili na badala yake ikiwezekana iongeze. Mikopo hii imekuwa na tija sana kwenye maeneo ambayo inatolewa; na sera yenyewe inasema ni kuwainua wananchi kiuchumi na inafanya hivyo kweli maeneo ambayo yamesimamiwa vizuri. Lakini kwa mara mbalimbali tumeleta mapendekezo kuonesha kiwango hiki bado ni kidogo lakini ndiyo uwezo ulipofikia. Kwamba bado kuna kundi la vijana wa kiume ambao kuanzia miaka 35

hawapati mikopo hii kwa sababu kwenye kundi la vijana ukifika miaka 35 hauwezi kupata na kwa wanawake wanahamia kwenye kundi la akina mama. Sasa vijana hawa tulikuwa tumeleta mapendekezo waweze kupata mpaka angalau miaka 45. Vilevile bado kuna mahitaji ya mtu mmoja mmoja ambao wanahitaji mikopo ambayo mikopo hii ingeweza kuwakwamua kiuchumi. Kwa hiyo, mimi nashauri suala hili la kutoa ile asilimia pale Serikali isiifikirie kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nirudi hapo kwenye nia ya kuondoa. Nia ya kuondoa asilimia tano ni ili kwenda kusaidia miundombinu kwa wamachinga. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri aangalie ni wapi katika Tanzania hii machinga *complex* ilishawahi kufanikiwa? Kuwachukua wamachinga na kwenda kuwapeleka sehemu peke yao hawafanyi biashara yoyote na mitaji yao inakufa.

Mheshimiwa Spika, mimi baada ya zoezi lile la kuwahamisha nilienda na niliongea na wamachinga. Wanasema wao vitu vyao wanavyouza ni vitu ambavyo vinategemea chenji kutoka watu ambao wametoka kununua bidhaa kwenye masoko au amekuja na nauli zao au eneo lenye watu wengi. Siyo bidhaa kama dawa ambayo mtu ataifuata eneo la mbali mnaloenda kuwaweka. Kwa hiyo, wamachinga wanatakiwa tutengeneze miundombinu wawe karibu na eneo lenye watu wengi. Hii kuchukua hela kwenda kujenga miundombinu na kuwapeleka mbali haiwezi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni eneo la kuweka *TIN* kwa kila mwenye miaka 18. Kama nia ya Serikali ni kuweza kupata *record* za watu na kukusanya vitambulisho vile kuwe na kitambulisho kimoja hili ni sawa kabisa. Lakini kama ni kwenda kutoza kodi kama kodi ya kichwa kwa watu ambao hawana

kipato hili litakuwa janga la Taifa. Ni kweli kila mwenye kufanya kazi na alipe kodi, mwenye kipato na alipe. Lakini wale wasiokuwa na kipato watatozwa kodi kwa sababu labda wamepewa zawadi ya hela wamenunua kitu? Haitakuwa sawa. Kwa hiyo, kama ni kukusanya utitiri ule wa vitambulisho ili tuwe na kitambulisho kimoja cha *NIDA* ambacho ndicho kina *TIN* na ambacho baadae kitakuwa leseni kama nchi zilizoendelea itakuwa ni sawa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nimeona kwenye kujaribu kupambana na shida ya mafuta ya kula, Serikali imetoa mapendekezo tofauti. Kuna baadhi ya mapendekezo yanakwenda kukinzana moja kwa moja na jitihada za Wizara ya Kilimo za kuhakikisha kwamba tunalima kwa mfano alizeti ambayo kwa muda mfupi itaweza kuleta tija kwenye viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nimeona wameondoa kodi kwenye mafuta ghafi yanayotoka nje. Sasa nina angalia, kwa nini hizi hazijaunganishwa? Kwa sababu kule kwenye kilimo tayari tunatoa ruzuku yenye mbolea, tunakwenda kufanya utafiti kwenye mbegu, tunatoa mbegu nzuri. Sasa kwa muda mfupi, ina maana kwenye kilimo chetu tayari tutakuwa tuna mali ghafi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapotoa kodi asilimia *zero* kwenye mafuta ghafi, tunaenda kuumiza ule upande wa kilimo ambao tumeweka nguvu. Eneo lingine kwenye kuagiza mafuta kutoka kwenye nchi za Afrika Mashariki, tulishafikia *level* ambapo, mafuta yanayoagizwa yanayotengenezwa kwa *raw material* za ndani, basi yatozwe *zero tax,* lakini sasa bado ninaona pale tuna asilimia 25. Sijaelewa hii imekaaje? Namwomba Waziri atakapokuja kuhitimisha atufahamishe kwamba tayari tumeshafika kwenye *custom union,* lakini

yanatoka kwenye nchi jirani bado tunatoza. Yangepunguzwa kwenye *zero* sisi tungeweza kupata unafuu ndani.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la lumbesa. Wizara ya Kilimo imefanikiwa sana kwenye masuala ya nafaka, maharage na mengine, lakini kwenye mazao ya mboga mboga kama nyanya, karoti na vitunguu, wakulima bado wanauza kwa lumbesa. Kwa mfano, kwa Mkoa wetu wa Kilimanjaro yananunuliwa zaidi na watu wanaopeleka nje, hasa nchi jirani kama Kenya. Sasa wanakuwa wanapunjwa sana. Namwomba Waziri wa Kilimo aangalie namna ya kwenda kuondoa hii lumbesa, iishe kabisa na wale wakulima wapate tija.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la ardhi, nadhani kwenye mwongozo limeongelewa vizuri. Nami niangalie tu, ardhi ikipimwa na vile vitu ambavyo vimetajwa pale, maana yake tunaongeza pato. Nashangaa sisi Moshi Mjini tulishapitisha vikao vyote tangu mwaka 2016 kuongeza eneo. Nia yetu ni kuwa Jiji; hata hivyo siyo kuwa Jiji kwa sasa, lakini angalau eneo la kijiografia liongezwe kwa sababu maeneo hayo ya pembeni yanajengwa kiholela. Wizara imeendelea kuwa kimya pamoja na kwamba ile hati kwenye *GN* ilishasainiwa, lakini maombi yetu tumeshapeleka *TAMISEMI,* Wizara ya Ardhi na haijafanyiwa kazi. Tunaomba Waziri aliangalie hili kwa upande wa ardhi ili pale Moshi Mjini tuweze kupewa haki yetu ambayo tumeiomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Fedha waitizame mikopo inayotolewa na makampuni ya simu. Mikopo hii inatolewa kwa muda mfupi, riba yake ni kubwa na wakati mwingine unalipa riba hata mara mbili. Ile ni mikopo kama mikopo mingine. Kwenye semina ya *BOT* niliwauliza, mikopo hii inayotolewa na kampuni za simu kama *airtime* na kama hela wakati unapofanya uhamisho wa hela, wanaisimamia?

Sikupata jibu kamili. Naomba wakati wanahitimisha, watueleze na watuambie vile viwango vya riba kama vina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana kwenye mfumo wa *TRA*. Watu wengi ambao wanarudisha marejesho ya *VAT* wanaanza tarehe 1 - 20 bado mtandao ule una shida na baadaye wanaingia kwenye *penalty*. Tunaomba sana Serikali iende ituambie. Mheshimiwa Waziri alisimamie na atuambie ni nini kinawashinda kwenye mtandao huu ambao unakusanya hela? Kwanza wao wanachelewa kupata hela, halafu wafanyabiashara wanachelewa, wanaingia gharama kubwa na baadaye wanapigwa *penalty*. Tunaomba sana hili liweze kusimamiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la mapato, nilichangia wakati wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Tukiweza kuwa wabunifu kusimamia vizuri *TPA* kwa maana ya kwamba bandari tulizonazo, *TRA* kwa maana ya kwamba mtandao huu wa reli, tunaweza kutengeneza fedha nyingi sana. Mimi nikasema kwa mfano, tukiwatafuta wadau kama *Dubai Port,* ambao wana-*operate* kwenye nchi nyingi, wana uwezo mkubwa, wana fedha za uwekazaji, tija itaongeza na sisi tutakuwa kama *hub* ya ku-*re-export* mizigo kutoka maeneo mengine kwenye nchi hizi ambazo ni *landlocked* ambazo ninatuzunguka. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niishie hapo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wageni wetu kutoka *CRDB Bank* wameingia humu ndani. Yupo Mkuu

wa matawi yote ya *CRDB Bank Tanzania,* Ndugu Bonaventura Paul, karibu sana; yupo pia ndugu Chabu Mishwaro ambaye ni Meneja wa Kanda ya Kati. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nipatia nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia wote tukiwa hapa katika afya njema na kuteleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya hasa kusimamia majukumu ya Kitaifa, na kwa kweli inabidi apate pongezi za kutosha kutokana na kazi anayoifanya ni kubwa, na Mwenyezi Mungu amjalie kumpa afya njema na amani na utulivu ndani ya nafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Fedha, Naibu wake, Katibu Mkuu na viongozi wote katika Wizara ya Fedha pamoja na Mkurugenzi wa *TRA* kwa kazi kubwa wanayoifanya. Naona hapa makusanyo ya *TRA* peke yake tumepata Shilingi trilioni 17.2, haya ni makusanyo makubwa. Naomba Mwenyezi Mungu azidi kuwaendeleza hawa watu watukusanyie pesa nyingi, ziweze kufanya kazi za kusaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepiga kilio kingi sana kutaka meli ziwe zinapokea au zinachukuwa mazao kutoka katika Bandari ya Mtwara. Jana tarehe 21 kwa mara ya kwanza meli kubwa imeweza kuchukuwa tani 15,000 za korosho katika Bandari ya Mtwara. Haya ni maendeleo makubwa sana katika mikoa ya Lindi Mtwara na Ruvuma kuhakikisha mazao yanayotoka katika

mikoa hii yanapita katika Bandari ya Mtwara. Hii itatusaidia kuleta ajira na kuongeza uchumi katika mikoa ambayo inaonekana iko nyuma, lakini ni mikoa ambayo ni ya kitajiri sana.

Mheshimiwa Spika, hongera sana kwa kusimamia humu ndani, nasi Wabunge tuko pamoja nawe, kwa kazi kubwa tunayoifanya kuhakikisha mikoa ya Lindi, Mtwara na Tanzania kwa ujumla inatoka kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni mlezi wa watu wenye ulemavu, vilevile Waziri wa Fedha ni Balozi wa Watu Wenye Ulemavu. Tarehe 16/6/2022 Umoja wa Mataifa umeridhia mpango mkakati kwa watu wenye ulemavu ikiwemo, wamezungumza kwa Kiingereza, lakini nami nitanukuu.

Mheshimiwa Spika, moja, ilikuwa *innovation and technology advancing people with disability;* namba mbili, *economic empowerment and entrepreneurship for the people with disability*. Kwa kweli lazima tushukuru sana. Maridhio haya ni lazima yarudi tena ndani ya Bunge letu tuweze kuyatekeleza ili walemavu wanaotaka kufaidika na mapato na uchumi katika nchi hii, nao wawe wanajumuika katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nazungumza hivyo? Walemavu wengi wanakosa ajira. Katika kukosa ajira, sheria hii ya kuwawezesha kiuchumi katika biashara na ujasiliamali unawafanyisha walemavu wale ambao hawajapa ajira wakiweza wenyewe kujisaidia. Hapa tunahitaji Wizara ya Fedha isimamie. Namwomba Mkurugenzi wa *TRA* tukae na Wabunge na taasisi mbalimbali zinazosimamia haki za walemavu, kuwepo na *desk* maalum la kuwasimamia walemavu hawa ili waweze kupata *exemption. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walemavu ni kundi maalum na linahitaji matumizi maalum. Leo tunakwenda katika elimu ya juu. Mlemavu haoni, anahitaji *computer* na zile *computer* zina *devices* mbalimbali na *application* mbalimbali, leo unavyomfanya mlemavu huyu anunue kifaa cha bei kubwa sana, ina maana una m-*paralyze*. Kwanza ni masikini; pili, hana ajira na hata akimaliza elimu yake, hana pa kwenda. Hivyo naiomba Wizara ya Fedha iwaangalie watu wenye ulemavu kwa mapana yao, kuhakikisha vifaa wanavyohitaji, iwe vya usafiri, matumizi ya shuleni, kutembelea kama fimbo, vipewe misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wangu, tuwe na *desk* maalum ndani ya *TRA*. *TRA* watuwekee *desk* ambalo litakuwa linaangalia na kufanya *monitoring* kwa vifaa vya watu wenye ulemavu, ili watu hawa wasiwe wanahangaika kwa ajili ya mahitaji yao. Maana yake itakuwa kama tunamkoma mlemavu. Kwa vile ni mlemavu, basi anazidishwa katika masuala yake ya ufanisi, inakuwa haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina suala langu la pili, ni wafanyakazi wa *TAZARA*. Kwa kweli kwa masikitiko makubwa napenda kutangaza kifo cha Mwenyekiti wa *TAZARA* ambaye ni mstaafu, alikuwa anakuja kusimamia mafao ya wastaafu ya toka mwaka 2010 mpaka leo hawajalipwa. Hii inatokana na mahusiana yalikuwepo kati ya Tanzania na Zambia yalivunjwa, lakini watu hawa 480 hawajalipwa mafao yao mpaka leo. Yule baba amekuja hapa, nimempeleka kwa Waziri wa Fedha, kwa Naibu Waziri wa Fedha, nimempeleka kwa Katibu Mkuu, nimempeleka kwa Waziri wa Ujenzi na Naibu Waziri wa Ujenzi ili walipwe hela zao toka mwaka 2010 mpaka leo hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, yule baba amepata mfadhaiko, mpaka amepata *pressure* amefariki. Kwa kweli inasikitisha.

Haiwezekani Watanzania wamefanya kazi wale, wengine miaka 40 wanastaafu, leo hii mwaka wa kumi na kitu hawajalipwa hata senti tano yao. Je tujiulize humu ndani Bungeni, tukimaliza Bunge hatulipwi hela zetu tunakubali? Kama hatukubali, kwa nini wafanyakazi wa *TAZARA* wanaendelea kunyanyasika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kaeni chini, Wizara iwaangalie wafanyakazi wa *TAZARA*. Hawa watu wamestaafu, mpaka sasa hivi watu 137 wameshakufa bila kupata haki zao. Haileti furaha katika nchi kama hii. Najua mama hana taarifa hii. Mheshimiwa Rais angelijua hili, tusingekuwa mpaka leo tunahangaika. Wanakwenda huko wananyanyasika, naomba...

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Lulida, sijui taarifa inatokea wapi? Mheshimiwa Ally King.

**T A A R I F A**

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba siyo *TAZARA* tu, pia kuna wastaafu wa *NASACO* ambao mmoja amezikwa juzi, nao pia hawajapata stahili zao. Kwa hiyo, nampa taarifa hiyo Mheshimiwa Riziki Lulida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Lulida, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwa heshima kubwa aliyonipa, kwa vile na yeye vilevile anaguswa na wenzetu wanaostaafu, na sisi wenyewe tunastaafu humu. Tukikosa mafao yetu yatatuhuzunisha hivyo hivyo. Ninakupenda sana kwa kauli hiyo na ninaikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hiki kitu lazima tukifanyie kazi. Nina Imani, tuipe muda mpaka mwezi wa Tisa Serikali iwe imeshawalipa hawa watu hela zao. Wafanye *verification,* kila kitu kiko wazi, ni urasimu tu. Mimi nasema nina imani kuwa hii kazi itamalizika na wale watu watafarijika.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni Sheria ya Manunuzi. Sheria ya Mwaka 2013 ni mwiba katika nchi yetu. Unaona hapa, *TRA* wamekusanya mapato kwa wananchi, kwa halmashauri lakini kuna kundi dogo linakula hela hizi zote ambazo tumezikusanya kwa faida yao na kuifanya nchi iwe inapata taabu kwa kuratibu hela ambazo wamezichukuwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano. Mfano huu wamekuja kutuletea elimu watu wa *GPSA*. Watu wanaouza magari wametu-*block* kule Japan, nchi isinunue magari ili tupitia kwao. Gari linalonunuliwa Kenya, Tanzania ni mara mbili; East Afrika hii hii moja. Gari inayonunuliwa Uganda, Tanzania kwetu ni mara mbili. Tumefika wapi? Tujitambue. Kwa nini tuendelee kuchezewa namna hii?

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nataka ni-*declare interest,* mimi mwenye ni mwathirika wa kununua magari ya Toyota *brand-new,* lakini gari ninalonunua Tanzania na Kenya ni vitu viwili tofauti. Nataka Waziri mwenye dhamana ajiulize, kuna nini ndani ya Toyota kuhusu ununuzi wa magari?

Mheshimiwa Spika, *UNDP* ni taasisi ambayo ilikuwa inaleta magari Tanzania kwa ajili ya miradi yake, lakini cha kusikitisha hata *UNDP* nao wamezuiwa, hawaruhusiwi kuleta gari yoyote *zero mileage* Tanzania kwa vile, wale watu ambao wanainyonya nchi hii wanataka kuendelea kuifyonza mpaka tudhalilike. Haikubaliki! Tukae chini na hii sheria ya mwaka 2013 ibadilishwe, wasifikie watu kutuona tunaangaika, wakulima

wanalima, huku mwisho mtu mmoja anachukuwa donge lote anakaa nalo pembeni, anatufanya sisi kama shamba la bibi. Muda wa shamba la bibi Tanzania umepitwa kabisa na wakati. Watanzania sasa tumefunguka, tunataka tuhakikishe maonevu yote yanayofanywa yanashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni *MSD*.

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Lulida. Kabla hujahama kwenye hiyo hoja. Kwa maana ya kwamba magari mapya hayaruhusiwa kuingia nchini?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Magari mapya katika *zero mileage* huruhusiwi mpaka upitie Toyota, lakini nchi nyingine zinaruhusiwa *directly* kwenda Japan. Hii siyo magari tu, hata katika ununuzi wa madawa, wameyafunga makampuni ya nje, wameingia nao mkataba kuwa hakuna mwingine yeyote kwenda kuchukua kule mpaka wao. Matokeo yake dawa hizo hizo, tutafukuza ma-*DG,* lakini bado hao Mawakala wakubwa ndio wanaichezea hii nchi. Tunafanya kazi kubwa, wao wanachukuwa wanaondoka nayo. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji. Kwa mfano halisi, leo ukitaka kuagiza Toyota, hii mpya kama anayotumia Waziri wa Fedha, inauzwa dola 143,000 pamoja na ushuru; lakini mimi nikiiagiza hiyo gari, ushuru wake tu ni shilingi milioni 210. Halafu kuinunua ni Dola 140,000. Yaani ushuru umewekwa mara mbili ili lazima ukapitie Toyota. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilimrejesha Mheshimiwa Lulida kwenye hoja hiyo ili kama sivyo ilivyo Waziri atatoa ufafanuzi kuhusu hoja hii. Kwa sababu Waziri hawezi kupata nafasi ya kujibu hoja zote, lakini hii tutataka kuisikia, kwamba yaani nchi hii nzima...

**MHE. YAHAYA O. MASSARE**: Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA: …**inatokea sehemu moja tu, yaani kwamba Toyota ndio anaruhusiwa kuleta magari yenye *zero mileage!* Hilo litakuwa jambo la ajabu sana. Haya Mheshimiwa Massare.

**T A A R I F A**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lulida anashindwa tu kuifafanua vizuri, kwamba Toyota Tanzania ni *agent* wa *manufacture* kule Japan. Sasa ame-*monopoly* soko kiasi kwamba wewe huwezi kwenda kule kwenye soko kwa mtengenezaji moja kwa moja. Sasa hoja iliyopo hapa ya Mheshimiwa Lulida ni kwamba kuna uvivu tu wa watu wetu, wamekubali kuingia kwenye mtego wa *Toyota Tanzania* ambaye ni *agent* wa mtengenezaji. Kwa nini tusiende moja kwa moja kwa mtengenezaji? Yaani Serikali iagize kiwandani moja kwa moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimesema hivyo kwa sababu hoja hii haina tofauti sana na yale tuyayolalamika kuhusu mafuta. Haina tofauti sana. Ni bidhaa tofauti, lakini haina tofauti sana. Kwa sababu gani? Yale makampuni ya mafuta, wewe kwamba utapitiliza kule kwenye *refinery,* inaweza ikawa mtihani, lakini ni mambo yanayoendana hivi. Kwa hiyo, ufafanuzi ni muhimu, ili kama ziko fursa, basi wananchi wachangamkie hizo fursa, Mheshimiwa Lulida ulikuwa unaingia kwenye hoja yako ya pili.

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Spika, hii siyo kwa ajili ya wananchi, hata Serikali inaagiza kila mwaka zaidi ya magari 400, lakini kwa mfumo huu Serikali inakula hasara kubwa sana ya fedha katika kununua magari. Leo tujiulize, Wizara zote wanatumia V8, *Landcruiser,* sasa kama utaendelea kununua magari katika bei kubwa kama hivi, ina maana bado uchumi huu tunaupeleka sehemu moja, tunakokotoa hela zetu ambazo tunaangaika kwa wakulima, wafugaji, wao wanakuja kuchukua hela ya mwisho kwa kutuonea na kutufanya sisi kama shamba la bibi. Tujifunze kwa wenzetu wa Kenya na tujiulize sisi kwetu kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya mwisho, kuna suala la mafuta. Sisi Tanzania tuna *shortage* ya mafuta, lakini nashangaa ufuta wote tunaupeleka nje, unakwenda kuwa *processed* nje, badala yake mafuta yanaletwa Tanzania katika bei kubwa. Tujiulize, kama ufuta unalimwa Lindi, Singida, Kondoa, Kilwa na wote mnausafirisha halafu mnaagiza mafuta. Urasimu huu unakujaje? Kwa nini hivi viwanda mmevifunga? Tunajikuta tunafunga viwanda na mafuta mnaagizia kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tukae chini tujiulize, tunajitambua, tunajifafanua, au tunajielewa? Inaleta kigugumizi. Hili jambo la kupeleka kila kitu nje, ufuta nje; karanga nje; halafu matokeo yake, hata sasa hivi baadhi wanasema tutapeleka mashudu nje; hakuna kupeleka mashudu, zinapelekwa alizeti mbegu, halafu baadaye tunaletewa mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, Wewe ni mlezi wetu kwa walemavu. Mungu akubariki sana na aendelee kulinda katika kiti chako. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba na Mheshimiwa Zaitun Sief Swai ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Nitazungumza suala la wachimbaji wadogo. Mwaka 2016/2017, tukiwa hapa Bungeni wachimbaji wadogo Tanzania walikuwa wanachangia milioni 81 tu kwa mwaka, lakini baada ya kumshauri Waziri wa Fedha ambaye sasa ni Makamu wa Rais Mheshimiwa Mpango alitusikiliza na wakawaita wachimbaji wadogo wakawaeleza sababu zinazowafanya watoroshe dhahabu na Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na mambo mengine, baada ya kuwasilikiza wachimbaji wadogo iliamua kupunguza kodi, kodi zote kutoka kodi 54 ikarudi mpaka kodi asilimia saba. Matokeo yake tumeyaona, tulikuwa tunachangia milioni 81 leo tuko kwenye bilioni 500, hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimemwona Mheshimiwa Waziri amepunguza kodi kwenye *refinery* alafu ameongeza asilimia mbili kwa wachimbaji wadogo, kama ukiweza kuipata ile *clip* tulivyokaa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano wakati tunamwomba apunguze ili tuache kutorosha dhahabu, angejifunza kutokea hapo. Sasa matokeo yake ni nini? Utoroshaji wa dhahabu hauhitaji kuwa na *barrier* wala Serikali haina Polisi wa kuweza kuzuia kutorosha dhahabu, dhahabu ina namna nyingi, hata kwenye nywele, hata kwenye kwapa, zinatoroshwa dhahabu kama anavyoingia mfungwa gerezani unakuta anavuta sigara imeingiaje? Utajua mwenyewe baada ya kumgundua anavuta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, suala la kuongeza asilimia mbili kwa wachimbaji wadogo

aliache, hata kwenye Kamati yetu sisi tumeomba, bado hata hiyo asilimia saba ukifuata ukweli mpaka sasa bado wanatoa karibu asilimia thelathini na kitu. Kwa hiyo tuliomba pia ipinguzwe, kwa sababu mtu kutoa dhahabu chini mpaka kwenda kuuza dukani ameshatoa asilimia saba karibu mara nne. Kwa hiyo niombe sana suala la wachimbaji wadogo tumeona walivyochangia kwenye pato la Taifa, ilitakiwa tuwapunguzie kutokana na ugumu wa kazi yenyewe ilivyo ili waweze kuchangia zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala la machinga, hapa nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Mtaka na tukizungumza humu wanatuona kama *slack*, lakini nadhani wamejionea kwamba tuliwa-*disturb* wamachinga, wamefilisika tumeachiwa mabanda, halafu sasa hivi tena tunawapelekea bilioni 45.

Mheshimiwa Spika, bilioni 45 wakizitoa watakaofaidika labda ni machinga wa Dodoma kwa sababu gani, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma baada ya kupokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba watengenezewe mazingira, halafu wahamishwe ndiyo anaandaa mazingira mpaka leo hajapiga machinga mpaka leo, anamaliza soko na amekaa nao na wakamwambia sehemu sahihi ni hapa, anatengeneza soko la mfano, watu watahamia pale. Hao watu hata ukiwapa mkopo ni sahihi wataenda kufaidika nao, lakini wajifunze kwenye mikoa mingine ambayo tulikurupuka kupiga bila maandalizi.

Mheshimiwa Spika, tuchukue mfano Mwanza hapo kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mabula, tumewapeleka dampo, leo nenda pale dampo, yamebaki mabanda ya mabati watu wote wamefilisika wamerudi kijijini, wamekimbia madeni ya *SACCOS* wamekimbia madeni wanapokopesha madukani. Hapo ukitumbukiza bilioni 45 nani atazichukua? Ukichukua maana

yake tunakwenda kulipa machinga waliofilisika. Kwa hiyo niombe sana haya mambo Mheshimiwa Rais anapokuwa anawaelekeza Waheshimiwa Mawaziri yaani waende mbele zaidi haina maana ya kumchanganya na kuvuruga watu. Viongozi waongeze wigo sasa huko mbele tunawawekaje hawa watu wabaki salama na mitaji yao na waendelee kuipenda Serikali yao bila kuona kwamba sisi tunawanyanyasa. Ningependa na Wakuu wa Mikoa wengine waje wajifunze kwa Mtaka hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nimewekeza Dodoma, Mheshimiwa Mtaka hakusumbua mtu yoyote mpaka leo na watu wako safi na sasa soko linaisha, wahame waende sehemu sahihi ambayo hata watu wenyewe wameona kumeandaliwa, siyo kupeleka zimamoto ya mabanda, matokeo yake watu hawauzi, mwisho wake wanaanza kuyachoma tu bora lichomwe tufe wote tukose kila kitu.

Mheshimiwa Spika, nizungumze suala la elimu bure, Serikali imefanya jambo kubwa sana kuweka elimu bure, lakini hapa niulize swali dogo na Waziri aje anijibu, wakati anatangaza elimu bure kidato cha tano na sita tayari wananchi wengine walishalipa ada za watoto wao kwa mwaka huu. Je, hizo fedha zinarudi au zinaingiaje sasa kwenye utaratibu. Tayari wameshalipia watoto wao, msamaha wa Serikali umetoka, zitakapoenda zile ruzuku zitarudishwa kwa wananchi ambao walikuwa wameshalipa au namna gani. Mheshimiwa Waziri naomba aje na hayo majibu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Nishati ya Madini na sisi kama Kamati tumekwenda mara nne. Unajua huu mradi ni mkubwa sana, ningekuomba ili kupunguza haya maneno ya kusikia mitandaoni, siku moja ikikupendeza utoe

magari hawa Wabunge waende wakaone, huo mradi ni mkubwa sana mimi mwenyewe nilipiga kelele hapa, lakini ulitupa ruhusa tumeenda tumekagua mradi uko mbali mno, lakini unapoingia kwenye Bunge tunasema mradi upelekewe Tume, tunatuma kitu gani, tusikatishane tamaa huu mradi ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, siku moja kwa heshima hata kama ni kutumia mabasi, hebu twende Wabunge wakaone kinachofanyika ili haya mambo ya kukatishana tamaa mradi huko vizuri na hatuhitaji mambo ya Tume, unatuma nini wakati Tume tupo sisi Kamati ya Nishati tumeenda na tumekuja tumeeleza kwenye taarifa. Tusimkatishe tamaa Mheshimiwa Rais kwa sababu huu mradi ni mkubwa sana, hata ungekabidhiwa wewe, hakuna mradi umekwama leo kwenye hii Serikali ya Awamu ya Sita, hata kama amerithi miradi mikubwa. Sasa tukisimama humu kuponda mara mwingine anaponda sijui *single source*, iwe namna yoyote sisi tunayotaka ni miradi ikamilike, tusimkatishe tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuchukua nchi kwenye janga kama lililoipata Tanzania na leo miradi ya matrilioni ikaendelea ku-*survive,* huyu mama anastahili kupongezwa sana Waheshimiwa Wabunge, siyo jambo dogo. Kuna watu humu ndani akifiwa mke tu, anakuwa kama chizi na analea tu watoto wawili mtu na bibi yake na shangazi, leo mradi wa matirioni na miradi inapigwa inaenda halafu unakaa kupiga majungu.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo mengi kwenye majimbo yetu, tujikite kuongelea majimbo yetu, tuachane na kukatishana tamaa kwenye miradi, tunaonekana kama sisi Wajumbe wa Kamati ya Nishati na madini hatuna akili, watu wengine wakisimama wanasema tupeleke tume, unatuma kitu gani, wengine kwenye Kamati zao wapo hoi, Kamati ya Nishati

na Madini ulichagua taaluma zote, tunaye *engineer* wa *TANESCO* hapa na sisi wenyewe watu wakabaji tunaojua fedha tumo.

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Musukuma Kamati za Bunge zote ziko vizuri, hakuna Kamati yoyote ambayo iko hoi. Hapo tu Mheshimiwa, haya endelea na mchango wako, Kamati zote ziko vizuri, Waheshimiwa Wabunge wote wako vizuri. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana ndiyo maana nasema ni vizuri tukaendelea kumtia moyo Mheshimiwa Rais hasa kwenye miradi mikubwa ya kimkakati, tukaiacha ifanye kazi, maneno mengine tutazungumza baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine naunga mkono suala la kufanya mikutano. Wakurugenzi na Wizara kwenye mitandao ni zuri. Hivi niwaulize anayepinga hiyo kazi yetu sisi Wabunge ni nini kule kwenye halmashauri, si ni kuisimamia Serikali na tukija humu tunasema kuna mapungufu, kuna nini tunasema, hii kila siku mawarsha, semina, hawa watu wote wasomi, tunachezea fedha, tunachezea mafuta, hivi leo nikuulize ingetokea *corona* bado inaendelea wasingefanya mikutano ya mitandao si tulikuwa tumeshaanza kwenda mitandao ka-*corona* kameisha tunataka mawarsha na makongamano, Hapana, hiki kitu na naunga mkono kabisa Serikali ijipange turudi kwenye mtandao, ndiyo maana ya maendeleo hata ukiyakataa leo huko mbele tutafika tu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ushuru wa vitenge. Tatizo letu Tanzania yaani kitu kikiharibika ndiyo tunakaa kujadili ku-*risk situation* kwa sababu gani? Nimeona hata kwenye kitabu cha Waziri anafuta kodi zote za nyavu ziwani, lakini sasa ukifuta leo tuliwashauri humu wakati wanaanza kuvuruga tanisia

ya uvuvi hawakutusikiza, leo watu wote kule wameshafilisika hawakopesheki, ukifuta kodi hiyo mitego anayoinunua ni nani au basi Serikali walete mitego wawakopesheni wavuvi tuanze upya maana ndiyo wenyewe waliwafilisi wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana, suala la vitenge ni la muhimu sana kukaa na kulifikiria, turudi kwenye utaratibu, leo Tanzania hatuingizi vitenge, lakini ukienda kwenye ma-*godown* ya Dar es Salaam yamejaa vitenge, hawajiulizi wenzetu vinaingiaje? Wafanyabiashara ni wanjanja wanaandika *transit* wamefika ngambo kule, wabongo hawa hawa wana maduka Malawi mpakani halafu wanarudisha hata kwa bodaboda, kila siku *godown* zimejaa, sasa nani anayekula hasara? Tunapeleka kodi Malawi badala ya kulipa kodi hapa Tanzania. Kwa hiyo ni vizuri sana, Serikali ione namna gani tulikosea kupandisha ushuru wa vitenge, tuone na hali yenyewe kwamba tumepandisha, tumekosa kabisa anayepata ni Malawi, sasa faida yake nini? Ni vizuri tukarudi kwenye utaratibu wa kawaida ili wafanyabiashara wetu waweze kui-*enjoy* na Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, suala la kitambulisho cha *NIDA,* mimi najaribu kuuliza kwamba tulivyoambiwa tunaenda kwenye *NIDA* nikaona pengine tutapunguza kutembea na makorokoro kwenye pochi, lakini leo hii una kadi za benki sijui nane, bado tena ukienda kukata leseni unaombwa utoe *TIN number.* Unaona hii pochi, humu hakuna hata buku, yote ni makorokoro yamejaa. Sasa wasomi wetu watengeneze kitu kimoja, kwa mfano kwenye *NIDA,* mbona tukienda Ulaya tunaona, ukitoa kadi moja inaonyesha mpaka watoto ulionao, hata wakifa inaonesha. Watengeneze kitu kimoja, sasa kila mwaka wanakuja na staili mpya, walituambia kitambulisho cha Mpiga kura kitakudhamini benki, leo ukienda na kitambulisho cha mpiga kura wanasema hakitakiwi lete *NIDA*, ukiwaambia tena

*NIDA* sijapata unaambiwa lete barua ya Mwenyekiti, mara lete *TIN Number* yaani pochi humu ingekuwa na Kisukuma kwamba nimeweka na hirizi aibebeki

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nani amesimama taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, sasa wasomi wetu waende mbali watengeneze kitambulisho kimoja…

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Musukuma kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, mzungumzaji amesema wasomi wetu, sasa ninachotambua ni kwamba yeye ni Daktari sasa hivi, sasa na yeye ni mmojawapo wakufanya hizo *changes. (Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii taarifa aliyoisema tena nimeshaletewa malalamiko, naendelea na tutatumia utaratibu gani mzuri. Udaktari wa Musukuma si udaktari wa kisomo, lazima tutofautishe mambo hayo, kwa sababu nimeletewa malalamiko kama Spika kwamba kuna watu sasa watataka kuacha kabisa kuitwa Madaktari kwa sababu sasa kila mtu ni daktari. Sasa Musukuma udaktari wake si wa kisomo. Kwa hiyo akisema wasomi anamaanisha wenye kisomo, yeye si wa kisomo, ni wa heshima.

Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ndiyo tofauti sasa ya madaktari kama sisi wa heshima, hiyo ndiyo tofauti aliyoiuliza mtoa taarifa hiyo ndiyo faida ya kuwa na madaktari wa heshima kwenye nchi kama

mimi, kwa sababu naona makosa tunayokosea nawarekebisha ili wakae vizuri. Ndiyo maana heshima haiji hovyo lazima uigharamie. Sasa nina heshima ya kimataifa, Bunge linatakiwa linipigie makofi kwa sababu mimi ni Mtanzania wa kwanza wa darasa la saba kuwa na *doctorate* ya heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo siyo siku ya kuelezea hayo, lakini ile siyo *doctorate,* ndiyo maana anaitwa *Honoris* Causa, kwa hiyo leo siyo siku ya hayo masomo, siyo umepewa kwa stahili hiyo.

Waheshimiwa Wabunge tuendelee nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Zainabu Athman Katimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Serikali. Kwanza nitangulize pongezi nyingi sana, pongezi kubwa sana kwa bajeti hii ambayo ni ya kimapinduzi na bajeti hii unaona imesheheni masuala au mikakati ya kuhakikisha kwamba Serikali inabana matumizi, lakini mikakati ya usimamizi wa fedha za umma na ndiyo maana tunaona kwenye bajeti hii *CAG* ameongezewa fedha, ameongezewa nguvu, lakini pia tumeona mikakati ya kuimarisha Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaona kwamba bajeti hii imejielekeza katika kuimarisha sekta za uzalishaji ambayo ni kitu muhimu sana kinaenda kuwagusa wananchi wote, lakini tunaona kuna mapinduzi makubwa sana ya kilimo na ndiyo

maana kwenye hotuba ya bajeti hii tunaona kwamba bajeti ya kilimo imetoka bilioni 294 mpaka kwenda bilioni 954. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa na chenye umuhimu pia tunaona kwamba kuna mkakati mkubwa sana au tuseme ni mapinduzi pia katika sekta ya elimu na ndiyo maana tunaona Serikali sasa inahakikisha kwamba wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita wanasoma bila ada. Haya ni mambo makubwa sana, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anahitaji pongezi kubwa sana kwa bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sivyo hivyo tu sisi tuna imani kubwa sana bajeti hii itatekelezwa, kwa sababu tunaangalia bajeti iliyopita utekelezaji wake ulikuwa ni mkubwa, fedha zilitolewa, mikakati mikubwa, miradi ya kimaendeleo haijakwama, inaendelea. Kwa hiyo, tuna imani kubwa sana katika utekelezaji wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Kigoma tuna imani sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, tuna imani na Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango, tuna imani na Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu, lakini pia tuna imani na Serikali kwa ujumla na ndiyo maana ukisoma aya ya 53 katika ukurasa wa 46 wa hotuba hii Serikali imeahidi kumalizia ujenzi wa barabara zinazounganisha mikoa na tumeona kwamba kipande kile cha Tabora – Kigoma na kipande cha Nyakanazi – Kigoma, Serikali imeahidi kwamba kwenye bajeti hii kinaenda kutimia, kinaenda kukamilishwa. Sisi watu wa Kigoma tuna imani kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye aya 55 ukurasa wa 47 tunaona kwamba Serikali imeahidi kwamba kwenye bajeti hii inaenda kujenga meli mbili katika Ziwa Tanganyika, lakini pia Serikali imeahidi ukaguzi wa kina katika Meli ya *MV* Mwongozo. Pia ukienda kwenye ukurasa 49, Serikali imeahidi ujenzi na

upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma. Tumeona kwenye bajeti ya mwaka zilitengwa bilioni nane, lakini kwenye bajeti ya Wizara ya Uchukuzi mwaka huu imetengewa bilioni saba. Sasa hatukuona utekelezaji, lakini tuna imani kwa kuwa Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba hii tena ameandika kwa maandishi yaliyokolezwa rangi nyeusi kwamba watahakikisha kwamba kuna ukamilishaji wa upanuzi na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma, basi sisi watu wa Kigoma tunaimani kubwa sana kwamba haya mambo yataenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 44 aya 51, Serikali imezungumzia suala la kuendeleza ujenzi wa reli ya kati na kipande kile cha Tabora – Kigoma chenye kilometa 514 ambacho kimetengewa *USD* bilioni 2.1, lakini kipande cha Uvinza - Malagarasi – Msongati – Gitega – Kindu na chenyewe kipo katika mikakati ya kuhakikisha kinapatiwa mkandarasi ili ujenzi uanze. Sisi watu wa Kigoma tunasema tuna imani kubwa na Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya afya, ukiangalia kwenye ukurasa wa 53 aya 63, Serikali imeahidi kuanzisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi na sisi watu wa Kigoma tunasema eneo lipo, michakato yote, taratibu zote zimeshakamilika kwa upande wetu. Kata ya Machinjioni, eneo la Kichangachui limetengwa la kutosha kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa hospitali hii ya Rufaa ya Kanda.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iweke kipaumbele kikubwa zaidi katika utekelezaji kwa sababu ujenzi wa hospitali hii ya Rufaa ya Kanda utasogeza huduma ya afya kwa wananchi kwa Kanda ya Magharibi ambayo kanda ile haipo karibu na Hospitali yoyote ya Rufaa ya Kanda. Kwa hiyo itasogeza huduma kwa wananchi wa maeneo ya kanda, lakini pia itakuwa ni utalii wa afya kwa sababu sisi kwetu kule Kigoma

lakini Kanda ya Magharibi kwa ujumla au tuseme tuzungumzie tu Kigoma, kuna majirani zetu watu wa Congo, watu wa Burundi ambao ni watu wa Afrika Mashariki, wanaweza kusafiri kuja Kigoma au kuja kwetu kule kupata huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa Serikali pia itakuwa imepata sehemu ya kupata mapato kwa sababu sisi tunaona tunaweza kusafiri nje ya Nchi ya Tanzania, tukaenda India kwa mfano kupata matibabu tunawaingizia wao mapato, lakini sasa kumbe sisi wenyewe tunaweza kupata huduma nzuri za afya, watu na wenyewe wakatoka kwenye nchi za jirani kuja kupata huduma kutoka nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala zima la vyuo vya *VETA*. Kwenye hotuba hii ya Bajeti Serikali imetenga Bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika ngazi za Wilaya, nasi kwetu kule Kigoma kuna Wilaya ambazo bado hazina vyuo vya *VETA* kama Wilaya za Kibondo, Kankonko, Uvinza. Kubwa kuliko yote ninayoweza kusema katika eneo hili ni kuiomba Serikali sasa, pamoja na kwamba tunajenga vyuo vya *VETA* tunaona mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu kwa maana sasa vijana wa *form five, form six* watasoma bila ada. Ukienda kwenye vyuo vya *VETA* wanalipa ada, lakini ukienda kwenye kada ya kati wanalipa ada, lakini kwenye vyuo vya Elimu ya Juu unakuta kwamba kuna Bodi ya Mkopo. Sasa naiomba Serikali iwaingize wananfunzi wa kada ya kati pamoja na vyuo vya ufundi wawe wanufaika wa Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunajenga uchumi wa viwanda, uchumi wa viwanda unahitaji kada ya kati, kwa hiyo tunaomba Serikali pamoja na hayo mambo makubwa yote ambayo sisi tunayapongeza lakini tunaomba Serikali ilibebe hili suala ili hawa vijana wetu na wenyewe waweze kuwezeshwa, waweze kuwa wanufaika wa Bodi ya Mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa manufaa ya muda nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, ajiandae.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia na kutoa maoni yangu kwenye Bajeti hii ya Serikali ya Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuipongeza Serikali kwa bajeti hii ambayo inayonesha ubunifu mkubwa lakini vilevile inaakisi maendeleo ya wananchi wengi hususan kwenye kujenga uchumi, kuondoa umaskini, na kwenye kutatua tatizo la ajira hususan kwa vijana, haya hasa ndiyo malengo makuu ya Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Arusha wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwenye bajeti ya Mwaka 2021/2022 tumeweza kuona miradi mbalimbali hususan ile yenye kugusa maisha ya wananchi mmoja mmoja. Tumeona miradi mikubwa ya maji, miradi ya afya, miradi ya elimu, miundombinu ya nishati, vilevile tumeona ametuwezesha kwenye masuala ya utalii ambayo yanachangia kwa kiasi kikubwa kwenye uchumi wa Mkoa wa Arusha. Kwenye hili vilevile naomba niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kuondoa ada kwa wanafunzi wetu wa kidato cha tano na sita, kwa kweli hii tutawapa fursa wanafunzi wetu wengi waendelee na elimu ya kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri kidogo Serikali kwenye hili iweze kuangalia umuhimu wa kupunguza au kuondoa kabisa ada kwenye vyuo vyetu vya kati ili basi kuwapa fursa wanafunzi hawa watakaomaliza kidato cha tano na sita waweze kujiunga na vyuo hivi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa 160 wa hotuba ya Waziri, ambayo inaonesha sura ya bajeti kwa mwaka 2022/2023 utaona kati ya shilingi trilioni 41.48 tunatarajia kukusanya zaidi ya shilingi trilioni 23.6 kutoka kwa Mamlaka ya Mapato. Hii ni zaidi ya asilimia 56 ya bajeti nzima ya Serikali. Ukiangalia hii utaona umuhimu wa Mamlaka yetu ya Mapato kwenye kutekeleza bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutimiza malengo haya ni lazima Mamlaka yetu ya Mapato iweze kujipanga sawasawa ili tuweze kutimiza malengo haya ya Serikali yetu. Kwanza kwa kuimarisha taratibu za kiutawala, vilevile kwa kuboresha mifumo ya makusanyo na kupanua wigo wa kodi. Kwenye hili la wigo wa kodi tumezoea kila mara Mamlaka yetu ya Mapato inaongeza kodi kwenye bidhaa zilezile, hii si sawa. Naomba Mamlaka ya Mapato ya *TRA* iweze kuwa na ubunifu zaidi kwa kuongeza vyanzo vipya vya mapato ili tuweze kutimiza malengo haya ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu huohuo wa Mamlaka yetu ya Mapato bado tuko nyuma sana kwenye matumizi ya mifumo. Ukiangalia tu kwa hivi sasa wafanyabiashara wengi bado hawana mashine za *EFD* na wale ambao wanazo hizi mashine hawatoi risiti za kielektroniki kwa sababu mbalimbali na visingizio. Nashauri Serikali kwenye hili iweze kugawa mashine hizi za *EFD* bure kwa wafanyabishara wote waliofika vigezo ili kuweza kuongeza makusanyo yetu na vilevile tuweze kudhibiti makusanyo yetu tunayopata.

Mheshimiwa Spika, katika hili Serikali iangalie njia ya kuweza kufidia gharama hizi za mashine wakati biashara hizi zinaendelea, pia naomba Serikali iweke msisitizo kwa Mamlaka ya Mapato ili iweze kuboresha mifumo yake. *TRA* ina mifumo mingi ambayo ni mizuri, kama *TANCIS, E-tax* na *E-filing* lakini tumeona mifumo hii bado haisomani, kutokusomana kwa hii mifumo tunaipa mwanya Serikali yetu kupoteza mapato kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, utakuta kuna baadhi ya mifumo hapa imeanzishwa kuanzia mwaka 2016, lakini mpaka leo mifumo hii bado ipo kwenye *process* za kuhuishwa. Naomba Serikali wakati inahitimisha hapa ituambie ni mikakati gani iliyonayo ili *TRA* iweze kuhuisha hii mifumo ili tusiweze kupoteza mapato yetu. Kama sekta binafsi, makapuni binafsi yanaweza ku-*roll out system* kwa mwaka mmoja tu nchi nzima, Serikali tunashindwaje ku-*roll out* mifumo na kuihuisha kwa muda wote huu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo kuhusiana na suala la misamaha ya kodi. Tumeona jitihada mbalimbali za Serikali kwenye kutoa misamaha ya kodi kwenye bidhaa mbalimbali ili kuwapa unafuu wananchi wetu wa kuzipata bidhaa hizo. Mwaka jana tuliona Serikali iliondoa *VAT* kweye simu janja ili kuweza kuwapa unafuu wananchi wetu wa kuzipata simu hizi. Lakini tuliona kwamba kwenye bei ya soko, bidhaa hizi hazikupungua bei na hivyo mwaka huu Serikali iomeondoa msamaha ule wa kodi. Mwaka 2018 Serikali ilitoa msamaha wa kodi kwenye taulo za kike, vilevile tuliona bei ya soko haikupungua na Serikali iliondoa ule msamaha wa kodi. Kuondoa misamaha hii ya kodi ambayo tuliiweka kwa madhumuni mahsusi sizani kama ni sawa kwa sababu tu tumeshindwa ku-*regulate* bei ya soko. Kama Serikali ni lazima tuwe na mipango madhubuti ya kuweza kudhibiti bei ya soko pale misamaha ya kodi inapotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala moja la taulo za kike. Inasikitisha sana wanafunzi wetu wanakosa masomo takribani siku 40 hadi miezi miwili kwa kukosa taulo hivi za kujihifadhi. Hii inawanyima fursa sana mabinti zetu kwa kufanya vizuri kwenye masomo yao. Nashauri kwenye hili kama Serikali imeshindwa kudhibiti bei ya soko, kwa kuweka misamaha ya kodi hii basi tuweze kugawa taulo hizi za kike bure kwa wanafunzi wetu wote wa shule za Serikali hususan, kwenye ngazi za msingi na sekondari ili basi tuweze kuwapa fursa wanafunzi wetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini inaonesha tukiweza kugawa taulo hizi bure kwa wanafunzi wetu wenye mahitaji, Serikali itagharamika takribani Shilingi Bilioni 50 kwa mwaka na hii ninaamini tukiamua tunaweza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie suala langu la mwisho ambalo ni kuhusiana na msamaha wa kodi kwenye hudumu za kukodi ndege *(Air Charter Services)*. Ukiangalia ukurasa wa 96 wa hotuba ya Waziri alitoa mapendekezo yake ya kufuta msamaha wa kodi kwenye huduma za kukodi ndege. Zaidi ya asilimia 70 ya huduma za ndege hizi zinatumiwa na watalii. Utakumbuka kwamba sekta hii ndiyo kwanza inajikongoja kutoka kwenye athari za UVIKO-19, tukiongozea mzigo huu wa *VAT* kwenye hizi *Air Charter Services* tutakuwa tunaiumiza hii sekta. Naomba kama Serikali tuweze kuunga juhudi za Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwenye kuinyanyua sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Spika, tukiweka *VAT* kwenye huduma hizi itaathiri sekta ya utalii vilevile itaathiri sekta ya *Aviation* ambayo yenyewe pia inajikongoja kutoka kwenye athari za UVIKO. Hivyo sidhani kama lengo hili la Serikali la kukusanya hizi Bilioni 36 litafikiwa. Kwenye hili tukumbuke kwamba kuna *booking* tayari

zimeshafanyika kwa watalii wetu ambao wanatarajia kuja nchini baada ya Julai, Mosi. Kwa hiyo, hapa tunaenda kuharibu soko letu kwa watalii wetu kwa kuongezea hizi gharama na pengine tukiwajulisha kwamba gharama zimeongezeka wanaweza waka-*cancel booking* hizo na tukawapoteza watalii hao. Kwenye hili pia nashauri Serikali mabadiliko ya kodi zote ambayo zinahusu sekta za utalii basi yaweze kutolewa mapema labda mwaka mmoja au miaka miwili kabla ili waendeshe utalii hawa na makapuni ya utalii waweze kujipanga vizuri na kuwajulisha watalii wetu ili tusiweze kuharibu soko hili la utalii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, atafuatiwa Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, Mhesimiwa Latifa Juwakali ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, naungana na watangulizi ambao wamechangia katika eneo hili la bajeti kuishukuru sana Serikali kwa nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba inatuletea maendelea na kutatua changamoto nyingi ambazo ziko kwetu wananchi kwa nia ya dhati na suala zima likiwa linaonekana katika mpango wa bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi kwa niaba ya wananchi wa Misenyi kwa Mheshimiwa Rais ambapo Tarehe 09 alikuwa na ziara ya kikazi katika Wilaya ya Misenyi, Jimbo la Nkenge, katika ziara hiyo Mheshimiwa Rais alizindua mradi mkubwa wa maji wa bilioni 15.7 ambao mradi huo unahudumia

wananchi zaidi ya 65,000. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na mradi huo ni wa kihistoria ambao ni mradi wa kwanza kutoa huduma ya maji kutoka Mto Kagera. Tunashukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Mheshimiwa Rais bado wana Misenyi wanaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri pamoja na kuja lakini aliweza kupita katika barabara ambayo itatengenezwa kilometa 25 kutoka Bunazi kwenda mpaka daraja la Kitengule, lakini pia tunaona barabara ya Minziro kwenda Mtukula imeanza kufunguliwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia kwenye bajeti pamoja na ziara hiyo Mheshimiwa Rais alipewa maombi kutoka kwa wananchi wa Misenyi na aliyapokea akasema anayafanyia kazi. Sasa niombe kupitia Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Mawaziri ambao wanamsaidia kazi wasije wakasema hatukusikia vizuri, naomba nipaze sauti kwa mara nyingine ili sasa wakati tunakumbushia na Mheshimiwa Rais nayachukua tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ilikuwa ni kuongeza kiwango cha lami kutoka Katoma, Bukwali kilomita 17 angalau mwaka unaokuja wa bajeti na mwaka unaokuja umaliziwe. Ombi la pili ilikuwa ni ujenzi wa uwanja wa Kimataifa wa Omukajunguti. Ombi la tatu ilikuwa ni kutengeneza barabara ya Bwanja kwenda Kaja kilomita 4.6 ambayo Mheshimiwa Rais aliyachukua na alisema anayafanyia kazi. Kwa hiyo, kwa kuwa nitaendelea kuyaongea haya niombe yaingie kwenye *Hansard* ili na Mawaziri waende kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la bajeti yetu naomba na mimi nijikite kushauri kidogo kwenye eneo la mikopo ya

wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Mahsusi Serikali ilikuwa na nia ya dhati kuhakikisha kwamba mikopo hii inafikia makundi lengwa na kwa mahsusi hayo mwaka 2018 ikatunga Sheria Na. 4 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sasa eneo hilo siyo la kufanyia mzaha, mtu yeyote kama hajatekeleza maelekezo ya Serikali anakuwa amekiuka sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hayo ikaweka uwiano wa 4-4-2, pamoja na hayo ikaelekeza ifunguliwe akaunti maalum ambayo katika akaunti hiyo mahsusi inapokea hela za aina mbili, hela za kwanza inapokea fedha zile ambazo Halmashauri kila mwezi katika makusanyo yake asilimia 10 inaingia katika akaunti hii. Fedha nyingine zinazopokelewa katika akaunti hiyo ni fedha ambazo ni za marejesho kutoka kwa vikundi nufaika ambapo wanarudisha zile fedha zinaingia mle ndani na hizo zinakuwa ni *revolving fund*.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili sikuona kwa nini Serikali ilijikita katika kutaka kumega asilimia Tano ya makundi haya wakati katika Mfuko huo zipo fedha katika *revolving fund* ambazo ukitoa Milioni 400 mwaka huu, mwaka ujao zinakuwa zinarejeshwa zinarudi. Kwa hiyo, maana yake katika Mfuko huo katika akaunti hiyo ukiangalia kwa mfano Manispaa ya Dodoma ambayo makusanyo yake kwa mwaka ilikuwa ni Bilioni 50, kwa hiyo maana yake asilimia 10 ni Milioni Tano. Ikikopesha Milioni Tano, mwaka unaofuata Manispaa ya Dodoma zinarudi katika akaunti hivyo hivyo katika *accumulation* ya namna hiyo. Kwa hiyo, katika fedha hizo Wizara ya Fedha haikuzigusa.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu katika eneo hilo, nilikuwa naona Wizara ya Fedha badala ya kuingia katika kugawa hii asilimia Tano na kubakiza sasa asilimia zikawa *ratio* ya 2-2-1, tuiache ile asilimia iwe asilimia 4-4-2 kama awali, lakini katika zile hela ambazo ziko katika Mfuko wa *revolving fund* na

kila sehemu hizo fedha zipo, kila Halmashauri inazo, hata mimi Wilaya ya Misenyi leo nikipiga simu pale kuna hela zaidi ya Milioni 500 za nyuma. Kwa hiyo, tunaweza tukaelekeza kama Serikali mkiona inafaa mkasema, katika mwaka husika basi itengwe fedha ambayo inalingana na asilimia Tano ya bajeti ya mapato ya ndani itoke katika Mfuko wa *revolving fund* ambayo ni unawezesha vikundi, vile vikundi viendelee kupata ile asilimia 10 ileile katika bajeti ya mwaka husika. Mimi nafikiri mngepata fedha na kutokutuletea tafaruku.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo tulindelea kuleta maoni mengi katika mfuko huu, sasa badala yake Serikali naona haikuitilia maanani. Mapendekezo yenyewe ambayo tulikuja nayo, tunao wananchi wanaotutuma, tunalo kundi la wanaume ambalo kila mwaka limekuwa likiomba na lenyewe lihusishwe katika mikopo hii, lakini kila mwaka tunaona Serikali kama inaweka pembeni badala yake inaleta kitu kingine. Mimi niwaombe hao wanaume ni sisi wenyewe, vijana wa kiume wakifikisha miaka 35 wanakoma kuwa vijana maana yake hawana msaada tena mbele. Kwa hiyo, tungeiomba Serikali iangalie na hili kundi la vijana ambao wanahitimu miaka 35 basi huo mwendelezo waweze kupata mikopo katika kundi la wanaume.

Mheshimiwa Spika, katika eneo langu la pili, ninaomba kwamba Serikali imeona kwa *case study* iliyopita katika bajeti hii ilielekeza Halmashauri zetu ziweze kujenga vituo vya afya kupitia mapato ya ndani. Nikiongelea uzoefu katika Halmashauri yangu katika Jimbo langu la Nkenge, tumejenga Kituo cha Afya kwa Milioni 500 kimekamilika, lakini ni wapi Halmashauri hizo zinapata hizo *financial muscles*, zinapata uwezo bila Serikali kuziwezesha?

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuja na mkakati wa awali wa kuwezesha Halmashauri zetu kupitia miradi ya kimkakati. Miradi hiyo ilikuwa ni mahsusi kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kuwa na uwezo wa kifedha na pale Serikali inapokuwa na suala ambalo ni mtambuka nchi nzima inazielekeza na zinatekeleza kwa sababu fedha zipo. Katika maeneo haya nikitolea mfano Wilaya ya Misenyi, mwaka 2019 maombi rasmi kutoka TAMISEMI yalienda Hazina na Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu nakuaminia na taarifa hizi unazo. Tukiomba kujengewa maghala katika mpaka wa Mtukula, maghala nane, tukiomba kujengewa stendi ndogo, tukiomba kujengewa soko.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo ni sehemu ya kibiashara, ukiangalia upande wa jirani zetu wa Uganda, biashara inayoendelea upande wa Tanzania unaona kweli hakuna msukumo, lakini hizo fedha ingeziwekeza katika eneo hilo tunao uhakika *return on investment* ingeweza kupatikana ndani ya muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo bado niendelee kusisitiza kupitia Waziri wa Fedha Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, bajeti iliyopita nilichangia ukasema unakuja Misenyi nikukaribishe na mara hii, niombe kwamba uje uangalie tuweze kuangalia kupata hiyo miradi ya kimkakati ambayo itakuwa ni kwa ajili ya kuboresha uchumi wa Wilaya ya Misenyi pamoja na hayo itasaidia sana kuboresha uchumi.

Mheshimiwa Spika, suala langu la mwisho ambalo ilikuwa ni kutoa shukrani za dhati kwa Serikali kuwa na nia ya dhati kuwasaidia wamachinga. Tumeona imetenga Bilioni 10 kila Mkoa kuimarisha uongozi, pia katika lile eneo ambalo inataka kujenga miundombinu ni kama nilivyoshauri. Katika Mfumo wa *revolving fund* wa Wilaya, Halmashauri zote upo, kujenga miundombinu ya machinga ni muhimu sana kwa sababu hili ni

kundi ambalo ni la muhimu sana linatusaidia wananchi wenyewe pia linainua uchumi wa wananchi mmoja mmoja. Kwa hiyo, niendelee kusisitiza na kuomba lengo kubwa la Serikali ile ambayo imeanza nalo isiliache ila itafute chanzo kizuri cha fedha ambacho kitakuwa hakiathiri malengo mengine ambayo yalishatangulia ili sasa Serikali iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa machache mengine niendelee kuipongeza Serikali kwa kutupatia elimu bure kwa kidato cha tano na kidato cha sita. Hili lilikuwa ni eneo ambalo lilibaki katika elimu ya sekondari. Tulishaanza kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne sasa Serikali inamalizia na kidato cha tano na sita. Niendelee kupongeza Serikali na kuomba sasa Serikali, kama wengine walivyoshauri tuangalie basi na michango mingine ikipungua, amani itakuwepo wananchi wataendelea kuwa na imani sana na Serikali yao na vijana wetu watasoma bila kuwa na bughudha na wale ambao hawana uwezo wote wataweza kuhudhuria masomo ya sekondari bila shida, na hatimaye tupate viongozi bora wote katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo natumaini muda wangu umekamilika nikushukuru kwa nafasi na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hatujaendelea na michango ya Waheshimiwa Wabunge yako makundi mawili ya wananchi waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 100 kutoka Chama cha Skauti Tanzania Tawi la Ubungo Dar es Salaam. Sijui wako upande gani; mkiitwa mnasimama wote pamoja. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 95 wa Shahada ya *Environmental Disaster Management* kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba atafuatiwa na Mheshimiwa Latifa Juwakali na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ajiandae.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuungana kwenye kuchangia bajeti yetu hii ya 2022/2023. Mimi nami naungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Baraza zima la Mawaziri na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, niendelee kulia kwa kilio kwa ajili ya tatizo kubwa kwenye Mji wangu wa Kahama, hasa barabara. Mji wangu wa Kahama ukiondoa Mji wa Mwanza Mji wa Kahama ndio unaofuata kwa ukuaji wa haraka na maendeleo na kibiashara na Serikali inakusanya mapato. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuongezee fedha kwenye eneo hilo kwa wananchi wetu hasa kwa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya bajeti yalikuwa mazuri sana lakini kwa wananchi wa kawaida mara nyingi wanatarajia vitu ambavyo vinawagusa. Kwa hiyo, ilikuwa inafika mahali wakiwa wanaangalia wanaona mbona haendi sawa haendi sawa, lakini alipofika kwenye suala la kuondoa karo kwa *form five* na *form six* wananchi nafikiri hapo waliona; lakini huku kwingine kwenye *H-code* sijui nini ilikuwa ngumu sana kwa wananchi. Kwa hiyo, *trip* nyingine labda wajaribu kidogo kuipamba bajeti ili wananchi *wai-feel* ile bajeti hasa wa hali ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli Wabunge wengi sana humu wameendelea kulalamika kuhusu upotevu wa fedha; lakini wanaolia sana wakati tunalalamika ni wananchi. Ni ukweli usiopingika kwamba fedha zote tunazokusanya, trilioni mbili, kwa mwezi zinatoka kwa wananchi asilimia 100. Sisi wote humu ndani ni waajiriwa na Serikali imeajiriwa na wananchi hao. Sasa, wananchi wanachojaribu kujiuliza; kwa nini Serikali haitengi asilimia 10 baada ya kupata shilingi trilioni mbili ili fedha hizo ziende kwenye matibabu na dawa? Suala la matibabu Serikali itake isitake tukubaliane lazima liwe bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani; wewe ni mchungaji wa ng'ombe na haikataliki mchungaji kula vizuri lakini inapofika kwamba sasahivi mwenye ng'ombe anaumwa unamwambia haiwezekani bwana ngoja ng'ombe zizae kwanza ndipo wewe utibiwe, haiwezekani. Serikali isikwepe, na Serikali haina *research,* kwamba kama itatibu watu wake bure *ina-research,* kweli kwani kuugua kuna *ratio*? Kama tumesamehe watu kusoma bure mpaka sekondari, tunakopesha *university,* kwa niniunakataa kuwatibu watu wako bure? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwa huumwi ukaenda hospitali, huwezi kwenda kuchoma sindano kama huumwi. Kwa hiyo hakuna *research* yoyote ambayo Serikali inayo inayoonesha kwamba kama itatibu watu wake bure Serikali itafilisika, haiwezekani. Itenge asilimia 10 badala ya sasahivi tunatenga fedha zinakwenda kuliwa; wananchi wanaona Wabunge tunalalamika kwenye TV, kwa nini tunawanyima dawa? Lakini Serikali ni ya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ni ya wananchi, sasa, inawezekanaje ukamnyima matibabu mwenye mali kweli anapokwenda hospitali? Hali ya maisha baada ya vitu kupanda ni ngumu sana. Leo gunia la mahindi ni shilingi

100,000, mchele ni shilingi 2,500; atapata wapi huyu mtu fedha ya kwenda kutibiwa?

Mheshimiwa Spika, Serikali haiingilii bei ya dawa wote tunaingilia bei ya mafuta, tunaingilia bei ya *cement*. Serikali imewatelekeza watu jamani kwenye matibabu. Kwa hiyo, tunamuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie kwa makini sana suala la matibabu, hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wakati mwingine tuwaombe na Serikali watoe takwimu zinazoonesha kwamba watu waliofariki pale hospitali kwa kukosa fedha ya kununua dawa ni wangapi ili hata tunapokuja kulalamika na Serikali iwe inapata. Tuwaombe na viongozi wa dini wakati wanasalia maiti waeleze kwamba marehemu huyu Mungu alimpenda lakini alifariki hospitali akiwa hana fedha ya kununua dawa. Na marehemu huyu Mungu alimpenda lakini alifariki. Madaktari walijitahidi kwa kila uwezo lakini Mungu akampenda zaidi, akaenda, kusudi iwe wazi; kwa upande huo watakuwa wametusaidia sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea suala la mkaa na kuni. Kwenye majimbo yetu, hasa Kahama mkaa na kuni ndiyo matumizi yetu makubwa. Lakini najaribu kujiuliza, ingawa wakati mwingine wasomi wanasema tusiwaulize. Hivi unaporuhusu mbao, ukaruhusu na magogo ukakataza kuni na mkaa tofauti yake nini? Inawezekana sisi elimu yetu ni ndogo, lakini wewe umeruhusu mbao na magogo, ukakataza kuni na mkaa inaingia kweli akilini? Je, mimi nikichukua mbao nikaifanya ikawa kuni utanikamata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kitu ambacho hakiingii akilini. Ni nini tatizo hasa? Je, akiruhusu mkaa ukaenda sokoni wananchi watapika zaidi? Kuna mtu ataamua kula zaidi? Haiwezekani.

Kwa nini asiruhusu kama alivyoruhusu mbao aruhusu na mkaa uende sokoni ili bei ya mkaa ipungue? Gunia la mkaa leo kutoka kwa mtu anayekata mkaa ni shilingi 10,000 porini. Likija huku sokoni mpaka inafika kununuliwa ni shilingi 80,000. Hawa wananchi wataweza? Hawawezi maisha ni magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba labda siku nyingine hizi Kamati zetu turuhusiwe na sisi Wabunge tupewe shilingi 150,000 tukakae Mbagala mwezi mmoja, upewe na watoto wanne tuone kweli inawezekana? Ili hawa wenzetu nao wawe wanajaribu kupata muda wa kufikiri. Ruhusu mkaa uje sokoni ili mkaa upungue bei.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia tu; mimi nimehudhuria hudhuria kidogo kwenye vyuo kwenye makongamano; nilichokiona elimu yetu haiunganishi biashara, ni ukweli usiopingika. Hakuna mahali ambako elimu mtu anasoma inaunganishwa na biashara. Nafikiri ndio maana unaona tukiongea tunaongea vitu ambavyo hata nyie mnashangaa ila wote tunaviona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninapoongea bei ya mkaa leo duniani ni *dollar* 1,000 ambayo ni sawasawa ni shilingi 2,300 kwa kilo, mkaa wa kuni. Nchi inayoongoza kwa *ku-export* mkaa kwa Afrika ni Namibia ikifuatiwa na *South Africa*. Lakini Namibia asilimia 85 ya nchi ni jangwa. Sasa inawezekanaje nchi yenye asilimia 85 jangwa ikaongoza kwa *ku-export* mkaa ilhali hii yenye asilimia 60 na ina miti inalima ina kijani ikazuia watu wake kula kupitia mkaa? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnunuzi wa kwanza anayeongoza duniani wote mnasimu za *WhatsApp m-google* tu; anayeongoza duniani kwa kununua mkaa, wa kwanza ni

Ujerumani akifuatiwa na Japan na hao hao ndio wanaotuambia sisi tusikate miti na hao ndio wanaonunua mkaa. Sasa inakujaje hiyo *model?* Nafikiri labda wasomi wetu wajaribu kufikiria, ni kweli inawezekana. Mjerumani ananunua mkaa *anau-refurbish* ule mkaa anauuza tena yeye ni watatu kwa kuuza mkaa. Hana miti, tena ni wa kwanza kununua n ani wa tatu kuuza tena duniani. Sasa *mnapo-google* mnaangalia hakuna uwezekano wa kujiuliza, yaani kwamba kwa nini sisi tunazuiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiruswa hebu sema ni taarifa, kuhusu utaratibu ama?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hapana ni Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kishimba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Kiruswa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe mzungumzaji rafiki yangu Profesa Jumanne Kishimba taarifa kwamba, hali ya dunia sasa hivi inaendelea kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. Sasa, ku-*promote* biashara ya kukata miti na kuchoma mkaa sio suala rafiki katika zama tulizopo. Hata hivyo kuna mbadala. Makaa ya mawe ambayo sisi Tanzania tuna akiba kubwa ya kuweza kutusaidia hata kwa zaidi ya miaka 100 kama biashara itaendelea kuruhusiwa duniani, ipo na tumeanza mkakati sisi kama Wizara ya Madini wa kuleta nchini mitambo ya kuchakata makaa ya mawe na kutengeneza makaa ya mawe ya matumizi ya nyumbani ambayo itakwenda kutuondolea adha ya kuharibu mazingira

haya ambayo tayari yanaharibiwa na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jumanne Kishimba unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, siipokei kwa sababu; wasomi msifanye kama sisi ambao hatukusoma hatuna uwezo wa kufikiri, hilo tukubaliane kabisa. Maana yake kinachofanyika hapa, huyu Mjerumani na Mjapani anayetuambia sisi; na ndiye aliyetoboa dunia, na aliyeharibu hali ya hewa ni nani? Si ndio wao wametoboa dunia? Ndio wakatajirika? Ndio wakatuletea sheria tena sisi? Sasa inawezekana kweli? Kwa nini sisi tuzuiwe? Haiwezekani watu wetu…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, kuchimba dhahabu leo yeye ni Naibu Waziri wa Madini…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, atuambie kuchimba dhahabu leo ni kazi ngumu zaidi kuliko kupanda mti wa mkaa na kukata mkaa. Tunakatazwaje sisi kwenda kwenye uchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kishimba kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

**T A A R I F A**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa mchangiaji Mheshimiwa Profesa Kishimba, *TFS* ambao ndio wanaongoza kwa kukamata wauza mkaa na ndio wanaoongoza kwa kupakia mkaa kwenda nayo nyumbani kwa matumizi yao na familia zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jumanne Kishimba unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, ndio naipokea kwa mikono miwili. Kama tutakubaliana na maneno haya tutaendelea kuwa masikini. Haiwezekani, tumuulize Balozi wetu, kwamba wewe Namibia inaasilimia 85 jangwa kwa nini wanaongoza kwa kuuza mkaa na kuni? Ili atupe maarifa yale tuje tutumie sisi. Sasa wao wana asilimia 85 hawaogopi wao kweli nchi yao kuisha ikawa tupu? Sisi ambao tuna asilimia 60 lakini hata mimi nakwenda shule kuanzia mwezi wa Oktoba Tanzania nzima inalima mazao mpaka mwezi Julai si ni kijani hiyo? Hampati kijani? Miti iliyopo mjini imefanyiwa *assessment*. Baada ya mchango wangu... *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja tu nimalizie. Kwamba ni vizuri, mimi kwangu hapa ninapoongea *TFS* wakikimbizana na mtu wa mkaa mwaka jana, nimepoteza wanafunzi wawili wa sekondari wamegongwa na gari ya *TFS,* ndiyo maana nalia kwa uchungu. Kwamba haiwezekani, wote tunakula chakula cha mkaa, tatizo hasa liko wapi? Ndio hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Anatropia Rwehikila Theonest ajiandae.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kwa wananchi wa Tanzania, tunampongeza sana. Pia nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Mipango kwa bajeti hii aliyoisoma kwa ueledi mkubwa, bajeti ambayo inaakisi mazingira na maono ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze mchango wangu katika Wizara ya Elimu. Naomba nimpongeze sana, kwa dhati ya moyo wangu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa fedha nyingi ambazo zinatolewa kupitia Bodi ya Mikopo ya Tanzania. Tukiri, tukiwa kama vijana, sasa zogo la mikopo limepungua kwa asilimia fulani tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuamua kwa dhati kabisa kwamba sasa kuanzia kidato cha tano na kidato cha sita kuwa ni elimu bure, tunamshukuru sana na tunampongeza sana. Niendelee katika hoja yangu ya Wizara ya Elimu. Sasa Wizara ya Elimu wanakwenda kufanya mapitio na maboresho ya mtaala wetu, na ni jambo jema sana.

Tumelizungumza sana na Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza sana kwamba elimu yetu ya Tanzania bado inahitaji maboresho inahitaji kuongezewa mambo fulani ili kuweza kuendana na ari lakini kuweza kuendana na mahitaji ya wananchi na vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nielezee au nichangie katika suala hili la vijana wetu wa vipawa maalum ambao wanaitwa *gifted or talented.* Bado kuna changamoto kwenye vijana hawa. Utaona mwanafunzi anasoma kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba, anafaulu anapelekwa katika vipawa maalum. Akipelekwa katika vipawa maalum tunategemea na tunatarajia sana anapokwenda katika zile shule akutane na vitu vya tofauti. Kuwe kuna utofauti baina ya shule ambayo ametoka ama zile shule za kawaida na shule za vipawa maalum. Hata hivyo, cha kushangaza bado katika mtaala wetu hasa katika *curriculum* yetu *haija-identify* moja kwa moja ni nini yule mwanafunzi wa vipawa maalum anapimwa ili kuweza kutofautishwa sasa baina yake yeye na mwanafunzi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mmoja. Tumetembelea shule nyingi sana lakini ukifika katika zile shule moja ya changamoto unaambiwa kwamba hawa ni wanafunzi wa vipawa maalum, lakini walimu wanaowasomesha wale wanafunzi wa vipawa maalum; sijui nitumie lugha gani ambayo itakuwa ni nzuri zaidi; yaani mwalimu sio wa kipawa maalum lakini mwanafunzi anayesomeshwa yeye ni *gifted*. Je, vipi tunaweza tukawaoanisha hawa baina ya mwalimu na mwanafunzi huyu? Naomba sana, naiomba sana Serikali wawaangalie walimu hawa wanaokwenda kusomesha katika wanafunzi wetu hao wa vipawa maalum na wao wawe *relevant*. Wakiwa *relevant* maana yake watakwenda kuwasaidia wale *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani wewe haujapata *first class,* lakini mwanafunzi ambaye unakwenda kumsomesha maana yake atakuwa amekutangulia kwa namna moja ama nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linanifanya nijiulize maswali; tunayo hii *National Strategic for Inclusive Education* 2021, 2022, 2025, 2026. Hii tunatarajia iwe ni miongoni mwa miongozo yetu katika kuisaidia elimu ya vijana wetu wa Tanzania. Cha kushangaza, naomba ninukuu *page number 17,* inasema; *"Learners, currently, there is also know clarity of standard to health harmonize teachers perception of giftedness or talentedness in their context."*

Mheshimiwa Spika, ikiwa wao wenyewe, yaani Wizara au Serikali hatujaonesha kwamba tunaweza kuwasaidia na tukaweka mfumo maalum kwa hawa wanafunzi, tunatarajia nini kwa hawa wanafunzi ambao ni *gifted? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natarajia sana Mheshimiwa Waziri au Serikali kupitia Wizara ya Elimu waje na kitu cha tofauti. Maana yake mtoto aliyefaulu katika shule hii akienda kule, kuwe kuna *curriculum* maalum ambayo inaweza kumsaidia akawa wa tofauti. Haiwezekani umefaulu Darasa la Saba unasoma katika Shule ya *Tabora Girls* au *Tabora Boys,* lakini *curriculum* yako inaendelea kuwa ni ile ile. Haiwezekani, lazima tuwaandalie *curriculum* yao.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mdogo kwa wenzetu wa Kenya. Wenzetu wa Kenya wanayo *curriculum* yao na wameweza ku-*identify* vizuri tu, wamesema, *special needs education curriculum…* Waka-*identify* wakasema hasa, *gifted and talented,* maana yake wamewa-*identify* watu hawa wa

vipawa maalum lazima watakuwa wana-*specific issue* na *curriculum* yao maalum ili iweze kuwatofautisha wao na wale wenzao. Pia wakaenda mbele wakaelezea vitu mbalimbali na *curriculum* yao. Naomba sana Serikali yetu kupitia Wizara hii ya Elimu walichukue hili ili tuweze kuwaboresha vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nilikuwa natarajia sana kwamba ikiwa mwanafunzi kafaulu Darasa la Saba kipawa maalum, kaenda *Form One,* kaenda *Form Three,* nilikuwa natarajia hata leo tukiuliza hapa mwanafunzi wa *engineering* ambaye ni *First Class* tunampata katika eneo gani? Nikisema mwanafunzi wa kilimo ambaye ni *First Class* mzuri ambaye anaweza kufanya *practice* vizuri, tujue tunampata katika eneo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni nini hapa kwa Serikali? Lazima Serikali iweze kufanya *mobilize,* na pia iendelee kuwafuatilia hawa wanafunzi wetu mwisho wao ni nini? Vile vile muwe na *database* yao, mjue wanafunzi hawa wamefaulu katika suala la biashara, wameenda *Form Six,* wanapomaliza *Form Six* tuwa-*mobilize,* tuwashajihishe waende katika vyuo vikuu maalum, halafu baadaye hao tuwajue tuwe tuna *data base*. Tukihitaji mwanafunzi wa aina fulani tunampata katika eneo Fulani.

Mheshimiwa Spika, hii itatusaidia hata kutokuporwa wale wanafunzi wetu wa vipawa maalum. kwa sababu, uzoefu unaonesha kwamba, mwanafunzi anapomaliza *Form Six* anajichagulia tu yeye mwenyewe kitu cha kusoma. Anaamua tu kwenda katika chuo gani? Akishafika kule tayari Serikali tunakuwa tumewapoteza, hatujui nani tutampata wapi? Nani aende mahali gani? Hii Mheshimiwa Waziri naomba sana kupitia Wizara hii tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze katika suala hili la vyuo vya kati. Naomba nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga fedha nyingi mno kwa ajili ya kujenga vyuo hivi vya kati. Nataka niseme tu kwamba vyuo hivi ni muhimu sana kwa sababu, ndivyo vinavyowasaidia vijana kujiajiri wenyewe na hata kusaidia kupunguza hili wingu kubwa la vijana ambao wanaomba ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisemi hivi nikiwa na maana kwamba, vijana wa elimu ya juu waliomaliza *Form Six* wasipate mkopo, la hasha. Wao wapate mkopo, lakini na hawa tunaomba sana wasaidiwe kupata mkopo kama wanavyopata vijana ambao wamemaliza elimu ya juu. Naomba tu Mheshimiwa Waziri, ikiwezekana hii Bodi ya Mikopo sasa hivi hata ingebadilishwa jina ikaitwa Bodi ya Mikopo tu, siyo inaitwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima na amani ambayo anaendelea kulijalia Taifa letu. Kipekee nimpongeze sana

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sambamba naye, nimpongeze Makamu wa Rais kwa usaidizi mzuri; na kipekee kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye Mratibu wa Shughuli zote za Serikali. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango pamoja na Naibu wake, pia wataalamu wote wa Wizara walioko katika Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kabla sijaanza mchango wangu nitoe pole kwa wakazi wa Jimbo la Mlalo, hasa Kata zile ambazo zinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi kwa namna ambavyo tembo wamekuwa wakivamia vijiji ambavyo vimezunguka pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa Mkomazi. Tembo wamekuwa ni tatizo kila kukicha, sasa wameanza kuvuna mpaka matikitimaji. Katika hali ya kustaajabisha, kuna Kijiji kimoja walivunja nyumba na wakala mpaka hata dawa ya meno. Sasa sijui Wizara itatumia njia gani, maana tembo wa mwaka huu kwa kweli naona imekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, nikianza katika kuchangia, naomba kwanza nianze na suala la diplomasia ya uchumi. Ninavyoona, pamoja na hotuba nzuri sana ambayo Mheshimiwa Waziri aliyoiwasilisha, lakini lazima tukiri kwamba yako maeneo mengi yeye mwenyewe amejipunja sifa. Kuna mambo mengi sana ya msingi ambayo yamefanyika na kwa kweli, kwa bahati mbaya sana hajayataja kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, sikuona hata sababu kwa nini anataja jina la Feitoto kwenye hotuba, labda kwa kutafuta huruma za sisi Wabunge, wakati yako mambo mengi ya msingi ndani ya

Wizara yamefanyika, ndani ya Serikali yamefanyika na ameyaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianzie katika eneo la diplomasia ya uchumi ambapo tumeona Mheshimiwa Rais akisafiri maeneo mbalimbali hapa nchini, katika dunia na Afrika. Katika maeneo yote ambayo Mheshimiwa Rais amesafiri, kila alipofika kuna aidha mikataba tumeingia au kuna makubaliano ya kibiashara tumefanya. Eneo moja ambalo nalikumbuka sana ni pale alipofanya ziara katika Falme za Kiarabu katika eneo la Dubai ambapo kulikuwa na maonesho makubwa ya *Expo Dubai.*

Mheshimiwa Spika, pale ipo mikataba mbalimbali ambayo Taifa letu limeingia, lakini ambao naukumbuka sana ni mkataba wa kampuni kubwa sana ya *Dubai World* ambayo iliingia mkataba na Mamlaka ya Bandari zetu kwa maana ya kufanya biashara, ili mifumo hii ya usafirishaji iweze kusomana. Kwa maana kwamba, Mtanzania anapoagiza mzigo kutoka Dubai uonekane moja kwa moja kwenye mifumo ya Mamlaka ya Bandari ya Tanzania, ili hata suala zima la usafirishaji na utoaji *(clearing and forwarding),* liwe rahisi. Jambo hili Mheshimiwa Waziri halisemi, wala hajalizungumza katika eneo lolote.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo kwenye diplomasia ya kiuchumi Mheshimiwa Rais amelifanya ni mara baada ya kuingia madarakani, alitembelea nchi jirani ya Kenya ambapo kulikuwa na vikwazo 64 vya kibiashara baina yetu na Kenya. Hadi hivi ninavyozungumza, vikwazo vile vimepunguzwa mpaka kufikia 15. Hali hii ni ya kupongeza sana kwa sababu, sasa hivi ukiangalia katika urari wa kibiashara kati ya Tanzania na Kenya, sisi tunauza zaidi Kenya kuliko wao wanavyouza kwetu. Kwa hiyo, hili ni eneo la diplomasia ya uchumi ambalo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri silioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linaungana na hilo kwenye *Dubai Expo* ni kwamba, kulikuwa na kampuni mbalimbali ambazo zingekuja kufungua biashara hapa kwetu. Kupitia eneo letu la Kwara, pale Kibaha, kwenye Kongani la Viwanda; viwanda zaidi ya 200 vinajengwa katika eneo hili la Kibaha Kwara. Wizara ya kisekta ya Viwanda na Biashara wakati wanawasilisha wasilisho lao la hotuba hapa, walitaja kwamba kuna mkakati wa kujenga viwanda 500, na hivi 200 ambavyo tayari vinajengwa sasa na kimoja kitafunguliwa mwaka huu, ni vile viwanda vikubwa ambavyo vina uwezo wa kuajiri watu kuanzia 500 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini tuna viwanda takribani 80,000, lakini viwanda ambavyo vilikuwa vina uwezo huo wa kuajiri watu 500 kwenda 1,000 ni viwanda 41 pekee. Viwanda vingi tulivyokuwanavyo ni vya watu wawili, watatu na kuendelea labda mpaka 100 na kidogo. Kwa hiyo, kujenga viwanda 200 kwa wakati mmoja na ambavyo muda wowote kuanzia sasa vitaanza kufunguliwa ni jambo kubwa ambalo tulitaraji tulione kwenye hotuba hii ambayo Mheshimiwa Waziri kwa bahati mbaya ama kwa kudhamiria hakuweka. Hapa maana yake anajipunguzia sifa, na pia anampunguzia sifa Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania na hili suala kwa kweli siyo zuri.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

## T A A R I F A

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naheshimu sana mchango anaoendelea kuutoa

Mheshimiwa Rashid Shangazi, lakini anavyozungumzia mafanikio ya Mheshimiwa Rais na kile ambacho kimeandikwa kwenye Hotuba ya Wizara ya Fedha, kuna Hotuba za Kisekta zilizopita zimezungumzia mafanikio ya Mheshimiwa Rais na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pili, tukiamua kuandika mafanikio ya Mheshimiwa Rais kwenye hivi vitabu vya bajeti, kwa maana ya bajeti kuu, tutaandika vitabu hata 23 kwa Wizara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe hapa nina barabara ya Makete kuelekea Mbeya, kwenye kitabu haijaorodheshwa, lakini kule tayari mkandarasi anakaribia kwenda. Nina hospitali ya Wilaya haipo kwenye kitabu cha bajeti, lakini fedha zimeshatengwa. Kwa hiyo, tukitaka kuelezea kila kitu kilichofanyika na kuonesha kwamba Waziri ameamua kumnyima sifa Mheshimiwa Rais, ni kwamba hatambui Wizara za kisekta ambazo zimezungumzia mafanikio ya Rais kwa ukubwa. Kwa hiyo, nilikuwa nampa Taarifa Mheshimiwa Shangazi kwa u-*senior* alionao kwenye Bunge hili, sikutegemea haya yatoke kwake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu amesema mimi ni *senior,* naomba nisimjibu. Aah, siipokei. Naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, ninachojaribu kusema hapa, ni vitu vikubwa, sizungumzii habari ya barabara ya Makete, hata Mlalo tuna shida ya barabara. Hapa tunajadili Bajeti ya Serikali. Tunaposhindwa kuhusianisha mambo makubwa kama *Expo Dubai,* makusanyo ya kodi ambayo yanafanyika ndani ya *TRA*

kwa ukubwa, tusipoyazungumza maana yake hata Waziri mwenyewe tunamnyima sifa ambazo alistahili kuzipata. Ndiyo ilikuwa maana yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Katika kipindi cha miezi tisa Mamlaka ya Kodi imekusanya takribani Shilingi trilioni 17.2. Ukipiga hesabu ya kila mwezi ni wastani wa Shilingi trilioni 1.9. Haya ni mafanikio makubwa sana, ambapo kodi hizi zimekusanywa bila kutumia *taskforce* wala mtutu wa bunduki. Ni sifa ambazo zinapaswa ziende kwa Waziri na kwa Mheshimiwa Rais ambaye ndio alitoa mwongozo wa namna bora ya kukusanya hizi kodi. Haya mambo tusipoyaona, na ni wajibu wetu kusema, na siyo kwamba hayapo, yapo, lakini yazungumzwe kwa kiwango ambacho kinastahili. Yazungumzwe kwa sifa ambazo zinastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri. Iko Tume ya Mipango ambayo ndiyo ilikuwa inatoa Dira ya Maendeleo ya Taifa. Hapa mara kadhaa Bungeni Mheshimiwa Josephat Gwajima alikuwa anazungumza habari ya maono ya Taifa, lakini nadhani hoja yake iko kwenye Tume ya Mipango ya Taifa. Tume hii ndiyo iliyomuibua hata Makamu wa Rais, Mheshimiwa Isdori Mpango, ambaye ndiye alikuwa Kamishna wa Tume hii. Sijui nini kimetupata tukafuta tume hii, lakini nadhani sasa ni wakati muafaka kuhakikisha kwamba tunakuwa na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, Dira ya maendeleo ya Taifa ambayo tunaenda kuikamilisha mwaka 2025 ilikuwa ni kazi nzuri iliyofanywa na Tume hii ya Mipango. Maana yake, kama tunaenda kukamilisha Dira ya Maendeleo ya Taifa, tutahitaji tena tume nyingine ambayo watu watajifungua ofisini, *brain* kubwa zianze kutafakari mambo makubwa ya Taifa hili. Ni lazima sasa Wizara ije na mpango mahususi wa kuhakikisha kwamba tunarudisha Tume ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango inaweza ikatupa mpango wa muda mrefu, inaweza ikachakata mpango wa muda wa kati, na baadaye mpango wa muda mfupi wa namna ambavyo tunatekeleza bajeti zetu. Bila kuwa na chombo hiki, maana yake tutakuwa tunabahatisha, nawe umejinasibu ni mwananchi, na unajua kinachotokea hata kwenye mashindano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutokuwa na mipango, wenzenu wa *club* nyingine wanapokwenda kwenye mashindano ya Kimataifa, wanatanguliza wataalamu wa *strategy* na mikakati kwa sababu wana mipango. Ninyi hamkuwa na mipango, mwaka uliopita mlitanguliza mpishi na *CEO,* matokeo yake mmeyaona. Kwa hiyo, hapa ndiyo kuonesha kwamba tunahitaji Tume ya Mipango iweze kutushauri vizuri katika eneo hili la mipango.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni eneo la *Royal Tour.* Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya katika sekta hii ya utalii. Sekta ya Utalii imeendelea kuonesha kwamba, inakua kwa kasi na tutafikia watalii milioni tano itakapofika 2025, dalili zote ziko wazi. Kwa hivi tunavyozungumza sasa, hoteli zote zilizopo katika hifadhi za Taifa zimekuwa *full booked* mpaka mwezi Desemba. Hii ni dalili njema ya kuonesha kwamba kazi njema ya Mheshimiwa Rais imeanza kuzaa matunda.

Mheshimiwa Spika, vile vile uwekezaji na ukuaji wa mitaji katika eneo zima la utalii, pia umeanza kuongezeka. Katika hivi viwanda nilivyovitaja pale Kwara kiko kiwanda ambacho kinakuja kwa ajili ya ku-*assemble* magari ambayo yatahusika katika sekta ya utalii. Kwa sababu tunapoutangaza huu utalii kwa kiasi hiki huko duniani, maana yake sasa wataanza kuja

watu ambao ni wazito zaidi, na inawezekana tukashindwa kuwasafirisha kwa magari haya ambayo tunayatumia sasa. Kwa hiyo, kwa kuona eneo hilo nalo lina umuhimu, kipo kiwanda mahususi kwa ajili ya ku-*assemble* magari yatakayotumika kwa ajili ya utalii. Hili ni jambo kubwa ambalo linaongeza mtaji na thamani katika utalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ziko hoteli kubwa kama Mariot ambao pia wameomba kutengewa maeneo waweze kujenga hoteli kubwa katika baadhi ya hifadhi zetu. Hili nalo ni eneo zuri ambalo tunaona kabisa kwamba, tunaposema watalii wataongezeka, basi ni vyema pia tukaangalia na maeneo ya utoaji wa huduma ili ziendane kabisa na hadhi ya watalii ambao watakuja katika eneo letu.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika katika suala zima la usafiri wa anga, kwa maana ya ndege. Safari zimeanza kuongezeka. Tumeona *Qatar Airways,* kwa mfano sasa hivi wanaruka mara 15 katika nchi yetu ya Tanzania. Tumeona *Kenya Airways* wameongeza miruko kutoka 13 hadi 21. *Turkish Airways* nao wameanza safari, watakuwa wanashuka mara tatu kwa wiki, nadhani wameanza Kilimanjaro na Zanzibar. Hii yote ni dalili kuonesha kwamba kazi njema ya Mheshimiwa Rais aliyoifanya katika *Royal Tour* imeanza kuleta matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nishauri katika eneo la utalii, hasa katika eneo la vitalu vya uwindaji. Eneo hili tumepata pesa nyingi sana kwa sababu tumepiga mnada vitalu kwa bei kubwa kuanzia dola 120,000 mpaka dola 190,000. Isipokuwa iko changamoto. Tunafahamu kama mapori yetu haya yako mbali kutoka kwenye viwanja vikubwa vya ndege, aidha *KIA* ama Dar es Salaam ama Mwanza. Kwa hiyo, watalii watakaposhuka hapo, wanahitaji sasa kwenda kwenye maeneo ambayo yana vitalu vile vya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, sasa changamoto ipo kwenye hizi ndege ndogo ndogo ambazo zinachukua hawa watalii kutoka kwenye viwanja vikubwa kuwapeleka kwenye *airstrip* ambazo ziko katika baadhi ya mapori. Hapa ni lazima sasa Wizara nayo ikae na hawa wadau na Serikali kwa ujumla tuone namna ya kuboresha ndege zetu ndogo ambazo zinaruka kutoka kwenye viwanja vikubwa kwenda kwenye hizi *airstrip*. Pia na gharama za *landing cost* katika viwanja vya ndege na mambo kama hayo ziangaliwe kwa sababu utalii wa uwindaji una gharama kubwa kwa maana kwamba mapori yako maeneo mbali kutoka kwenye viwanja vikubwa vya ndege.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, ni utayari wa kuwapokea wageni. Haitapendeza sana kuona kwamba mtalii anayekuja kutuletea fedha za kigeni katika nchi zetu anakaa foleni na watu wa kawaida. Kwa hiyo, tungependa kuona kwamba kuanzia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana ya Idara ya Uhamiaji ijiandae inavyopaswa, lakini pia Mamlaka za Viwanja vya Ndege ziwe na mifumo ambayo mtalii kuanzia kule anakotoka ajulikane kabisa kwamba *visa* yake ni ya namna gani asiwekwe foleni na wakati mwingine unakuta hata maeneo yetu hayana *air condition* wanapigwa na joto. Kwa hiyo yote hayo ni mazingira ambayo tunaweza tukaanza kuyaandaa kuhakikisha kwamba hii safari ya *Royal Tour* inaleta tija ambayo tumeikusudia.

Mheshimiwa Spika, pia hata madereva wa *taxi* walioko katika viwanja vya ndege vya kimataifa ni lazima Wizara ione umuhimu wa kwenda kuwapa mafunzo namna ambavyo wanaweza kubeba abiria wa kawaida na mtalii lazima iwe tofauti. Hili ni eneo ambalo huko nyuma tulikuwa hatujalipa mkazo wa kutosha, lakini sasa kwa namna ambavyo nchi yetu imeendelea kuwa na ongezeko hili kubwa la watalii ni muhimu maeneo hayo yote tukayazingatia kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo sasa ningependa nichangie ni kwenye sekta ya michezo, kwenye michezo bado kuna shida ya uwezeshaji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi kengele ya pili tayari.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, basi naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu na Mheshimiwa Seif Hamis Said Gulamali ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nitaanza kum-*quote* mchumi mmoja, katika tafsiri ya kawaida anasema; "Malengo halisi ya Serikali iwe kupunguza matumizi na siyo kuongeza kodi kutimiza majukumu."

Mheshimiwa Spika, kwa Kiingereza amesema; *"The real goal should be reducing government spending rather than balancing budget achieved by ever rising tax rate to cover rising spending."*

Mheshimiwa Spika, nadhani moja kati ya mkakati ambao Serikali wamekuja nao ambao ni kupunguza matumizi hasa kwenye magari lakini pia kufanya watumishi hao waweze kununua magari kwa niaba yao badala ya Serikali ambao

wamekuwa wametumia matumizi ambayo siyo sahihi ni suala la kupongeza.

Mheshimiwa Spika, nitaeleza changamoto kubwa ya bajeti. Mwaka hadi mwaka tumekuwa na bajeti ambazo haziwezi kutimilika, bajeti inakuwa na upungufu kila mwaka, ni kwa nini tukiangalia bajeti ya 2021/2022, ilikuwa na upungufu wa asilimia au zaidi ya asilimia 21 ambayo imetimia kwa 78%. Hivyo hivyo kwa miaka iliyopita ina maana tumekuwa tunapanga tukishindwa kukusanya vya kutosha kutimiza malengo. Nini *implication* yake kama bajeti inakuwa haitimii? Kama bajeti inakuwa haitimii kwa 100% au *at least* chini hata tuseme 90 au 95 maana yake malengo tuliyopanga kuyafanya katika mwaka husika hayakuweza kutimia na nitatoa mfano katika bajeti kadhaa, mfano katika mwaka uliopita tunaumaliza mpaka tunafikia Februari, TAMISEMI walikuwa wamepata fedha ya maendeleo asilimia 63; Wizara ya Ardhi, fedha ya maendeleo ilikuwa imepata asilimia 29.2; Wizara ya Kilimo 35%; Madini vivyo hivyo hii ni bajeti ya maendeleo 9.6%; Mifugo na Uvuvi 3.2%, *interpretation* yake ni nini hapa, ina maana malengo makubwa tuliyokuwa nayo hayakuweza kutimia. Hiyo itakuwa ni shida mwaka hadi mwaka, kama hatuwezi kukusanya vya kutosha tutakuwa tunakuja tunachukua muda mrefu hapa kupanga, kujadili, lakini kama hatukuwezi kukusanya fedha za kutosha tutakuwa tunarudi mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kutotimiza malengo hata *motivation* yenyewe inashuka, tunajua tutakuja kila baada ya miezi kadhaa tutakaa Bunge la miezi mitatu, tutaondoka hatutatimiza na tuta-*copy* na ku-*paste* kwenye vitabu vinavyofuatia tutajadili. Hebu tuwe na bajeti ambazo kidogo zinakuwa *a bit realistic,* kwamba tumeshajua *capacity* yetu ya *TRA* kukusanya ni kiwango Fulani, tumeshajua *capacity* yetu ya

kukusanya yale makusanyo yasiyokuwa ya kodi ni kiasi Fulani, halafu tutengeneze bajeti ambayo katika *level* fulani inaweza ikatekelezeka na tukija hapa tunasema tumekamilisha moja, tumekamilisha mbili, tumekamilisha tatu.

Mheshimiwa Spika, Kamati wameshauri hivi basi hata fedha ya matumizi iweze kuwa *covered*. Kwa sasa tunaweza kukusanya na kutumia tukawa na *surplus* ya trilioni tatu, ina maana *surplus* ya trilioni tatu tunaweza kufanya maendeleo yetu wenyewe kwa fedha yetu kwa 8% tu. Kwa hiyo tunaweza ku-*finance* miradi ya Serikali na mambo mengine mbali na fedha za matumizi ya kawaida kwa 8.1% ambayo unaona ni kiwango kidogo sana. Hata hivyo, wameenda mbali zaidi wakasema basi kama tunaweza kupambana tuweze kuji-*finance* kwa asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba unajua kama wewe mwenyewe kwa makusanyo yako huwezi kujitimizia hata asilimia 20 au 30 kama unategemea kukopa na wahisani bado utakuwa na maendeleo ya kusuasua kwa sababu pia inategemea na wao wameamkaje siku inayofuata. Tumeona *trend* mbalimbali zinazoendelea katika uchumi, *automatic* hizo *trend* zinaendelea kutu-*subject* kupata hela ndogo kwa watu tunaokuwa tunategemea watukopeshe au waweze kuleta kama misaada kwenye bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo moja kati ya mchango wangu nitakaojikita ni kuongelea ni namna gani tukiamua kuwa *serious* kuwekeza katika kukusanya kodi tunaweza *at least* kupunguza ile *deficit,* tunaweza kupungua *amount* ambayo tumekuwa tukikusanya. Mfano, wenzangu wameeleza, kwenye suala zima la *property tax* ripoti ya Kamati imeeleza wakati *property tax* zikiwa kwenye halmashauri, walikuwa wanaweza kukusanya kwa mwaka hata bilioni 64, lakini ilivyoenda TRA chini ya miaka

saba au zaidi ya miaka saba wameshindwa kukusanya hata bilioni 44, wakatoa miaka mitatu *consecutive* kwamba wame-*collect less than that*. Hapa unaona kwamba bado hatujawekeza vya kutosha hatukufanya utafiti kwanza kuondoa hicho chanzo kwenye halmashauri yalikuwa ni makosa, lakini hata kama imerudi tumefanya utafiti mkubwa kiasi gani kuona kwamba tutaenda kukusanya vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo wa majengo yaliyoko kwenye Halmashauri hata ya Ilala, hata Kamati ya Bajeti wamesema kwamba tukiwekeza vizuri tunaweza kukusanya hata bilioni 100 kwenye Halmashauri au kwenye Jiji la Ilala niseme. Kwa hiyo tunapaswa kuwekeza na nashauri namna hii, utaratibu waliouweka leo wa kukusanya *property tax* kupitia LUKU unaweza ukawa ni mustakabali kwa sababu hakuna mtu anayeumia, ni kodi inayotoka bila ku-*feel* maumivu ya moja kwa moja. Hata hivyo, sasa ni lazima Serikali waboreshe, kuna wengine ambao wana majengo yana thamani kidogo, hawawezi pia kulipa Sh.1,000. Kwa hiyo nadhani lazima mtengeneze hizo *classes,* watu katika maeneo fulani wachangie kiwango fulani, katika maeneo fulani wachangie kiwango Fulani, hiyo fedha itaweza kukusanywa kwa unafuu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ya Bajeti wakashauri, walichoshauri kinaweza kikarudi tulikotoka mwanzoni, mwanzoni tulikuwa tunashindwa kukusanya *property tax* kwa sababu ya mapendekezo yanayokuwa makubwa, nyumba ya kawaida unaambiwa ulipe elfu 50 au laki moja kila mwaka, *automatic* watu wata-*default,* tutengeneze kiwango ambacho kiko *amicable,* kila mmoja anaweza kulipa kutegemea na thamani ya eneo au jengo lake.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, kodi ya ardhi, tukiwekeza vizuri kwenye eneo la kodi ya ardhi ni eneo ambalo tutapata

hela ambayo hatukuitegemea. Kama tunataka tufanye vizuri, kama tunataka tusiwaumize wanaolipa kodi, *by the way* mfumo tunaoutumia leo wa walipa kodi wanaita *twenty eighty rule,* ina maana asilimia 20 wanalipa kodi ikatumike kwa asilimia 80. Kwa hiyo *automatic* kodi itakuwa ni kubwa, watu wachache watalipa kodi kubwa na wata-*default,* kwa sababu tunalazimika kuwawekea kiwango kikubwa ili waweze ku-*serve the eighty rule* lakini tukiamua ku-*exhaust* vile vitu ambavyo tunavyo, nimeshaeleza *issue* ya kodi ya ardhi, tukiweza ku-*exhaust* tukapima ardhi, kila mmoja akalipa kwa kiwango kidogo kidogo, tena kwa utaratibu kama wa LUKU, tukalipa *property tax*, tukalipa kodi ya ardhi kupitia LUKU, watakusanya *substantial amount of money*.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, upangishaji wa majengo, leo kuna watu wanapangisha majengo, sisi wengi hapa ni wapangaji, lakini *how much do we collect* kutoka kwa wale watu ambao wanakodisha majengo. Ukija kuona kama Dodoma *it a good business,* nyumba zinapangishwa mpaka milioni moja, lakini mtu halipi kodi. Hebu tutengeneze utaratibu mzuri, ambao nimeona maeneo mengine wametengeneza *application* wanasema *air B and B,* majumba yote wameya-*list* mle, wewe ukitaka kupata nyumba unaingia kwenye *application* na unalipa *certain amount* Serikali inapata fedha, yule anayepangisha anapata fedha na sisi tunapata hela ya kuendesha miradi mbalimbali ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, maeneo mengi yana bandari bubu, nitatoa mfano wa eneo ninalotokea Mkoa wa Kagera. Sisi tunazunguka Rwanda, Burundi na Uganda, lakini unakuta kwa kwenda Rwanda kuna mpaka mmoja tu tunaotumia Rusumo lakini watu wametengeneza bandari bubu katika maeneo mengi nitaeleza hususan eneo la Kajunju. Kajunju ni eneo ambalo ukitengeneza ukaweka *TRA* pale na

*Immigration,* tutapiga hela nyingi sana tutaisaidia Serikali kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, nadhani watakuwa waliiongelea Kamati kwamba kuwe na hiyo *tax* ambayo zinaongeza kwenye *goods* ambazo ni *indirect tax,* tunaweza kutengeneza mfumo kwa sababu sisi tunajua ni vitu vingapi vinaingia nchini au watu wanaweza kulipa kodi kwanza na wakauza kama kuna kitu hakitalipiwa kodi au kimeharibika au kimeondolewa sokoni watakuja kufanya tax *emission,* waende ku-*claim that amount* kwa sababu hiyo bidhaa haijauzwa. Hapo tutapata kodi yetu *right away.*

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini nimeongelea haya? Nimeongelea kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi kwa sababu bila kodi kukusanywa, leo nitaendelea kulia na barabara ya kutoka Mrushaka kwenda Nkwenda kwenda Murongo, barabara yetu ni mbovu kwa kiwango kikubwa, lakini kwa ukusanyaji wa kodi hii tuliyonayo tutaendelea kulia. Naomba Serikali pamoja na maoni mengine tuangalie namna ya kuongeza kodi tuweze kuondoa hizi changamoto.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya maji Wilayani Kyerwa, Mkoani Kagera ni changamoto kubwa, lakini kama hatuwezi kukusanya vya kutosha ina maana tutaendelea kulia vile vile. Bajeti ikiweza kupatikana kwa asilimia 70, ina maana hata mwaka ujao nitakuja nalia na mambo yale yale. Sasa nini kimekuwa kinatokea? Katika ukusanyaji wa kodi umeona wafanyabiashara wamekuwa wanaenda kupinga baadhi ya tathmini wanazofanyiwa na Maafisa wa *TRA* ya kulipa kodi, ina maana kumekuwepo na mashauri mengi ya kodi ambayo yapo na kodi hizo hazitalipika mpaka hayo mashauri yawe *solved*.

Mheshimiwa Spika, *CAG* ameeleza zaidi ya trilioni 300 *plus* ambazo zilikuwa zinalalamikiwa, ikiwa trilioni tano ziko kwenye migodi, makampuni mbalimbali ya madini, ina maana kama kuna makadirio yasiyokuwa *fair,* watu watakuwa wanaenda kupinga hayo malipo na kodi inabaki ikiwa haiwezi kulipwa, haiendi kwake haiendi *TRA* ina maana inabaki hapa kati kati na Serikali inakosa mapato. Mwaka hadi mwaka tunasema tunakusanya kodi lakini inakuwa ni kodi ndogo kwa sababu wanaolipa kodi ni wachache na wanaolipa hiyo kodi wanalazimika kutozwa zaidi illi waweze kuwa-*serve* watu wengine.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo Kamati imeshauri, kuwepo na kitu kinaitwa *tax ombudsman. Tax ombudsman* inashindikana kwa nini wakati tuna changamoto tunaziona zimeshakuwepo na kumekuwa na Baraza la Kufanya Mashauriano kama kuna hao watu wamekatalia hiyo kodi wanafanya nini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Hamis Said Gulamali na Mheshimiwa Ally Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Leo nitaongelea zaidi vijana lakini nitakuwa na *concept* moja ambayo katika mambo yote tunayoyafanya na muda wote tuliobaki hapa kujadili bajeti na muda wote tunaoishi duniani, kikubwa sana kinachoangaliwa ni udhihirisho au matendo kwa lugha nyingine unaweza ukasema *manifestation*. Tutapanga mambo yote tunayopanga,

wananchi watanzania wanataka kuona udhihirisho. Nilisoma nikiwa *form four* kitabu kimoja cha mwandishi mmoja anasema *bookworms are not popular,* maana yake ni kwamba maandishi ya kwenye vitabu hayatupi umaarufu wowote, kitakachotupa sisi umaarufu ni matendo *site,* udhihirisho wetu kule *site* tunafanya nini? Hicho ndiyo kitakuwa kitu kikubwa.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa sehemu zile walizoweza kudhihirisha kwa matendo na kule wanatupunguzia maneno mengi. Ukiona mwanasiasa unasimama unajieleza sana mahali unajieleza unaenda unarudi, udhihirisho haujaonekana, lakini udhihirisho ukiwepo utaongea kidogo na watu watakupigia makofi na vigelegele, utaondoka na mambo yatakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa ajili ya mpango mzuri na bajeti nzuri ambayo Waziri wa Fedha ameisoma na nawapongeza sana. Kama alivyosema Mbunge mwingine yote yangeandikwa hapa naamini kwamba tusingekuwa na muda wa kuweza kuyaongelea. Niwashukuru sana nilipokuwa nikichangia bajeti mwaka jana niliongelea suala moja linahusu utelezi, lakini nashukuru sana kwamba ule utelezi ule umetolewa kwa kiasi kikubwa katika Jimbo langu la Manispaa ya Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliongelea barabara ya *Ruaha National Park* nichukua *forum* hii kuwashukuru sana *World Bank* na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa waliyofanya kufanya *mobilization* ya *resource* mpaka tumepata taarifa kwamba barabara ile sasa inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuinua utalii kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika barabara kilometa 216 alizoziandika Waziri humu ambazo zimejengwa kwenye mikoa,

Iringa tumenufaika pia. Ipo mitaa ya Iringa ndani ya Chuo Kikuu Ruaha tumepata, Kata yangu ya Mkimbizi tumepata, Kata ya Mshindo tumepata, Kata ya Gangilonga tumepata, Kata ya Mwangata tumepata kipisi cha lami, tunaendelea kujenga na Isakaliwe. Tunawashukuru sana pia katika elimu madarasa tumepata na mambo yanakwenda vizuri, lakini *Royal Tour* pia sisi Iringa tumeipata utamu wake kwa sababu watalii tunawaona wanakuja.

Mheshimiwa Spika, sasa nakwenda kuongelea vijana udhihirisho *site*. Leo tumesema kwamba Serikali ya Rais Samia inakwenda kuweka mkazo kwenye ajira za vijana. Ajira tunayoitegemea hapa ni kwenye sekta binafsi lakini tunategemea pia na Serikalini. Sasa tunapoongelea vijana ajira ili tuwe na *work force* ambayo inaweza ikazalisha kwanza lazima tuangalie fursa zilizopo kuwapa vijana wetu, lakini pia kuangalia maarifa wanayopata iweze kuwa inaweza kuchangia katika *production* ya uchumi wetu. Vijana wetu wawe na uelewa tumeongea hapa tulikuwa na changamoto Wabunge wengine wameongea ya machinga. Unaponiambia kwamba unakwenda kusisitiza ajira ya vijana halafu unambughudhi mfanyabiashara mdogo kama machinga, maana yake ni kwamba udhihirisho kule *site* haupo, uhalisia haupo.

Mheshimiwa Spika, leo nimepigiwa hapa simu kutoka Iringa, machinga wananiambia watakuja nyumbani kwangu, nikawaambia karibuni sana na sijui nitawaweka wapi, inabidi tulale pale barabarani nje, kwa sababu tayari wanabugudhiwa kuondolewa wakati lile eneo ambalo tumepanga kuwapeleka bado hatujalikamilisha, tunalikamilisha haraka ili waende. Wenzetu walioko huku chini kuelewa yaani kuthibitisha yale maono ya Rais ni nini au maono ya Serikali ni nini katika kutoa ajira kwa vijana hawaelewi. Kwa hiyo tunaomba Serikali

iangalie na iwe na *coordination,* kuanzia ngazi ya Taifa mpaka kwenye Serikali za Mitaa wawe wanajua wanapoongea wa-*dance tune* moja, huku wanasema tunawatetea, tunahakikisha tunajenga ajira kwa vijana, huku wanakwenda kuwabugudhi hatuendi sawa.

Mheshimiwa Spika, kingine ukiniambia Serikali itaangalia itakapopata mapato ndipo itakapowezesha vijana wa elimu ya kati, siyo sawa. Hii ajira unaiwezeshaje, vijana wengi wanawachukua *form four* na wanakuwa wamemaliza vizuri kabisa wamefaulu tena wanachukua *cream,* wengine *division one or two,* wanawapeleka vyuo vya kati masuala ya afya, masuala ya *marine* na vitu vingine vyote. Halafu wazazi wale uwezo hawana wengine wanatoka kwenye shule za kata, vile vyuo vya *marine* ada zake milioni mbili, milioni tatu mpaka inafika mpaka 1,900,000, Watanzania hawawezi halafu waetuchukulia *cream form four,* leo ukiniambia umetoa *form five* na *six* ada bure, halafu huyu mwingine naye amemaliza *form four* anakwenda chuo cha kati cha Serikali, anagharamia gharama kubwa namna, hiyo siyo sawa, kwa hiyo lazima hawa wote wapewe haki sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia unaponiambia unaimarisha ajira kwa vijana, halafu unakwenda kupunguza mikopo ya vijana ya halmashauri, udhihirisho hauko sawa. Uongeze kwa sababu tunahitaji kubwa la ajira, sasa hivi vijana tunavyoongelea ni zaidi ya asilimia 60 ya *population* ya Tanzania, karibu watu milioni 37 ni vijana ukichukulia wenye miaka 18 mpaka 30 au 35, ni *population* kubwa. Kwa hiyo tunapowaongelea hawa watu ni kundi kubwa, sasa unaposema tena unapunguza ile asilimia 10, halafu uwape tano hauko *serious* kwenye udhihirisho wa kutoa hizo ajira kwa vijana. Lazima uongeze kwa sababu pia hili ni kundi kubwa kwenye *society* kuliko kundi lingine lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaposema kwamba utakwenda kuweka kodi ya *VAT* kwenye simu janja, Mheshimiwa Waziri lazima tujue vijana wengi wamejiajiri huko pia, kwenye zile *online* biashara zao za mitandao wanafanya kupitia hizo simu, tunategemea hicho kitengo nacho kitusaidie kuchukua kundi jingine na kiajiri vijana, unapokwenda kuongeza kodi unawatakia nini, kwa sababu suala la kwamba mliweka kodi msamaha halafu kwenye soko haikuonekana siyo suala la wale, suala ni wenyewe tumeshindwa kusimamia ni sawa na unavyosema unakwenda kuwatoza wachimbaji wadogo asilimia mbili eti kwasababu kuna changamoto ya kukusanya kodi kwa wachimbaji wadogo, hivyo, mnawapiga faini kwa kuwaongezea asilimia mbili ya kodi wanahusikaje?

Mheshimiwa Spika, wao siyo wakusanyaji wa kodi maduhuli ya Serikali, unawapaje tozo ya asilimia mbili kwasababu ya changamoto ya wewe kushindwa kukusanya kodi na unataka kutanua wigo wa ajira kwa vijana? Haiwezekani haya lazima tuyafanyie kazi na vijana wetu wasiongezewe kodi. Kwa maana hiyo Mheshimiwa Waziri kwa maana ya ile asilimia 10 hata ile Sheria unayotaka kuibadilisha ya Serikali za Mitaa Namba 290 usiibadilishe, ile asilimia 10 ibaki vilevile *unless* utuambie tena una kitu fulani unataka kuongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi. Tunatanua wigo wa ajira, kodi leo hii tunawawezekaji tumesema sekta binafsi tunataka kuiimarisha na umeongea kwenye hotuba yako kwamba Mheshimiwa Rais ameelekeza zile sheria ambazo hazina ufanisi kwenye sekta binafsi zinaikandamiza sekta binafsi zitolewe. Sasa sisi tunasema hivi sheria hata ile sheria ambayo imeunda kanuni ya ku-*regulate bureau de change* Tanzania ile sheria inatakiwa kufutwa kwa sababu inazuia watu kufungua maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, kwa maana hiyo inakandamiza

juhudi za kukuza utalii, inakandamiza juhudi za kutoa ajira, pia haitambui mchango wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa *Royal Tour* kuhakikisha ina-*promote* utalii katika nchi yetu, hivyo Sheria hiyo nayo inatakiwa ikarekebishwe.

Mheshimiwa Spika, pia tunasema tunataka kwenda kuinua ajira zetu kwa vijana wetu, lazima sasa tuendane sawa na ule mpango wa elimu, tunataka udhihirishe Waziri wa Elimu alituambia hapa kwamba kutakuwa na kozi ambazo vijana wetu watapelekwa kwenye nchi ambazo zina utaalam zaidi kujifunza mambo madogo madogo, sasa haya tunayaomba udhihirisho kwenye *site*. Hapa tumeona tu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ndiyo ameambiwa kwamba yeye atabeba vijana Milioni Tatu, lakini Wizara nyingine katika kutusaidia *share* za ajira kwa vijana zinafanya nini? Wizara ya Utamaduni itafanya nini, kwa sababu bado kuna fursa kubwa sana kwenye *games and sports* lakini kwenye *movie*, sasa hivi Tanzania tutaanza kuwa na *culture* za watu wa nje kwa sababu *movie* zote zinazooneshwa kwenye vituo vya *TV* zinaoneshwa *movie* ambazo siyo za maadili yetu, kwa hiyo sisi je, tunatumiaje *opportunity* hii. Katika kutumia *opportunity* hiyo leo hii tunatumiaje *opportunity* ya vita inayoendelea katika dunia siwezi kuitaja wote tunaijua. Kwamba wale ndiyo walikuwa wakulima wakubwa wa ngano, walikuwa wakulima wakubwa wa alizeti, wale ndiyo walikuwa wanatoa gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna alizeti, Tanzania tuna shayiri, Tanzania tuna mimea mingi sana inayotoa mafuta, hiyo *opportunity* tunaitumiaje halafu tuna vijana Milioni 33 wanaohitaji ajira unasema kwamba ni vijana na wanawake Milioni Tatu tu ndiyo mwaka huu tutakwenda ku-*deal* nao kuhakikisha wanapata ajira. Hebu tuulizane hadi tumalize hawa vijana Milioni 36 tutakuwa tumekwenda miaka mingapi? Je, tume-*stop* kuendelea kuzalisha hao vijana? Kwa hiyo, lazima

kila Wizara tuwe na *preamble,* zile Wizara ambazo zinatoa ajira lazima zituambie zina mpango gani wa kuhakikisha kwamba zinachangia kwenye hiyo *share* ya kutoa ajira kwa vijana. Kwa mfano mimi nimejikadiria…

**SPIKA:** Haya ahsante sana kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja lakini udhihirisho tunauomba *site* ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi siku ya leo kuweza kuwa miongoni mwa wanaochangia kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Binafsi ninapenda kutumia nafasi hii kwanza kumpongeza Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoifanya ndani ya mwaka mmoja hongera sana kwake. Tumeona mabadiliko makubwa kwenye sekta mbalimbali, hususani tumeweza kuona pia kwenye fedha zile za UVIKO shilingi trilioni 1.3 tumejenga madarasa elfu kumi na tano nchi nzima hakuna Kata ambayo hawajajenga.

Mheshimiwa Spika, pia tumepata zile fedha za UVIKO tumepata Milioni Mia Tano kila Jimbo kwa ajili ya miradi ya maji, tunawapongeza sana. Pia tumepata fedha hizo hizo za UVIKO kwenye ununuzi wa mashine za *MRI* kupelekwa kwenye hospitali ya Mikoa, *x-ray*, *CT scan* kwenye hospitali za Wilaya. Ni jambo kubwa ambalo kwakweli litaweka historia kubwa, tumeona katika ubunifu huu wa kwake Mheshimiwa Rais tumepata fedha za tozo za miamala ya simu tumejenga vituo vya afya kwenye

Majimbo yetu kwenye nchi yetu zaidi ya 230 vimejengwa nchi nzima.  Vituo vipya hivi ambavyo vimeingia kwenye hesabu.

Mheshimiwa Spika, pia tumeona kuna vituo karibu 50 vimefanyiwa ukarabati, tumeona mapato ya ndani vituo 110. Kwa hiyo ukivijumlisha vituo vya afya ambavyo vimepata fedha ni 388, kwa hiyo nitumie nafasi hii kupongeza sana hongereni kwa kazi hiyo nzuri, kwakweli sisi ambao tumepata fedha na mimi nimekuwa miongoni Jimbo langu limepata fedha Milioni Mia Tano, kituo cha afya cha Ziba kimejengwa kutokana na fedha hizi za tozo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunakupongeza kutupatia fedha lakini pongezi ziende kwenu nyote kwa maana ya watendaji ambao wapo kwenye Wizara zenu lakini pia na Mawaziri ambao wanaunda hii Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilipenda nilizungumze tumeona pia uendelezaji wa miradi mikubwa kama Bwawa la Mwalimu Nyerere kule Rufiji linaendelea kujengwa, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa hiyo Kamati, Kamati ya Nishati na Madini tunasimamia mradi huu, ujenzi unaendelea na hakuna deni. Kwa hiyo tunaendea kupongeza kazi ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia tunaona ujenzi wa *SGR,* treni ya umeme kazi yenyewe inaendelea tumeanza na *lot* nyingine kama ya Mwanza, Isaka, Tabora, Dodoma lakini pia tumeona *lot* nyingine za kwenda Kigoma zinaendelea mpaka Katavi. Kwa hiyo, hakuna kazi zilizosimama tumeona

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa kama ujenzi wa Daraja la Tanzanite umekamilika, Daraja la Kigongo la kule Busisi linaendelea, tunaamini baada ya muda mfupi daraja lile na lenyewe litakamilika na litaanza kutumika kwa wananchi. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako naomba nishauri baadhi ya vitu ambavyo nimevisikia umevisoma kwenye bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kushauri nimeona umetoa msamaha wa *VAT* kwenye maziwa, Mheshimiwa Waziri nilifikira kwamba ungeweka *zero rate* kwa sababu ukisema msamaha kabisa kwa ujumla kwenye maziwa kuna maziwa ya *powder* lakini pia kuna maziwa ya ng'ombe, ukiweka msamaha Mheshimiwa Waziri utawaumiza wanaozalisha maziwa kutokana na ng'ombe kwa sababu watu watatumia sasa, unawapa nafasi pia wadau wa nje kuleta maziwa yao ya *powder* kutoka nje ya nchi, hii itaumiza sana wazalishaji wa maziwa kupitia ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nimeona umepunguza ushuru kwenye maziwa haya kwa maana ya maziwa *powder* pamoja na maziwa ya ng'ombe. Mheshimiwa Waziri unapopunguza ushuru umetoa kwa kilo moja 2,000 kwenda 1,000, Mheshimiwa Waziri unahamasisha matumizi ya maziwa *powder* badala ya maziwa ya ng'ombe. Hili litaleta athari kubwa sana, hata makampuni sasa unayahamasisha kuagiza maziwa ya *powder* kutumia uzalishaji kwenye viwanda vyao. Niombe maziwa *powder* ikiwezekana muongeze ushuru badala ya kupunguza. Lakini pia maziwa ng'ombe kwa sababu mmepunguza muendelee kuyapunguza msiongezee.

Mheshimiwa Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri hili mlichukue kwa sababu maziwa *powder* sasa yatakuwa ndiyo yanatumika zaidi kuliko maziwa ya ng'ombe, na maziwa ng'ombe ndyio tunayatumia, tuna ng'ombe wengi sana wananchi wetu wanayo na wanazalisha maziwa hii uta*discourage* mauzo ya maziwa ng'ombe kwenye viwanda lakini pia katika mzunguko wa nchi yetu. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri mlichukue hili na kuangalia jinsi gani ya kuwasaidia watu wetu maziwa ng'ombe yaweze kuingizwa kwenye viwanda vyetu lakini pia waweze kupata vipato, msifanye *flat rate* kwamba tunapunguza ushuru kwenye maziwa *powder* pamoja

na ng'ombe hilo hapana. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana uliangalie hili, ili usiweze kuwaingiza kwenye mtihani makampuni yakaanza kutumia maziwa *powder* kwenye uzalishaji wa matumizi ya maziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakuomba sana uliangalie kwenye kodi, lakini lingine nimeliona Mheshimiwa Waziri kwenye kodi kwenye magari yenye *XL* tatu, yapo magari yenye *XL* tatu ya tani tano, tani saba, tani 10, tani 12, na tani 40, Mheshimiwa Waziri usichukue yote kwa upamoja wake maana yake mengine unayaathiri. Nakuomba sana yenye tani ndogo uyaache vile kwasababu ukiweka bei hii kubwa unaenda kuathiri usafiri na usafirishaji wa mazao kutoka shambani utapanda, bei itakuwa kubwa na hatimaye chakula na gharama nyingine zitaongezeka na mzigo huu utakwenda kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri yale yenye tani kama 15, 20, 40 ongeza kodi lakini yale yenye tani tani tano tani kumi usiyaongezee kutoka fedha iliyopo hadi Milioni Tatu na Nusu utawaumiza sana Mheshimiwa Waziri nakuomba sana urudishe ileile gharama iliyokuwepo kwenye haya magari yenye tani ndogo. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana hili litasaidia hata mzunguko wa wananchi wetu katika kusafirisha hata mifugo yetu kupeleka kwenye minada itakuwa imeongezeka zaidi kama utaweka hizi kodi. Lakini lingine nikuombe tumeona kuna misamaha ya viwanda, viwanda vikubwa vinapata misamaha ile ambayo ina mitaji kuanzia milioni sitini inapata misamaha, lakini chini ya milioni sitini hawana misamaha.

Mheshimiwa Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri hivi viwanda vilivyopo chini ya milioni sitini shusha huu msamaha hadi ya milioni ishirini ili hawa pia watu wenye mitaji midogo ya

Milioni Ishirini kwenda juu wapate misamaha na ikiwezekana walelewe na *SIDO* kuhakikisha kwamba unawakuza baada ya muda fulani waingie kwenye kodi ambazo mngependa muwatoze. Kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri hebu fanyeni kwa kuangalia hawa wenye mitaji ambao wapo chini ya kiwango hicho cha Milioni Sitini.

Mheshimiwa Spika, kingine Mheshimiwa Waziri nilipenda niishauri, nimeona pia kuna masuala mazima ya udhamini ya vilabu, udhamini wa vilabu, unadhamini *club* unatozwa 18 *percent* ya *VAT* na tumeona mfano tu wale *Sportspesa* wanadhamini Simba na Yanga wanatozwa *its okey* ni *brand* kubwa ni timu kubwa, lakini timu kama *Mbeya City*, timu kama *Singida United*, timu kama Dodoma Jiji nani atakwenda kuvidhamini kama mdhamini hadi adhamini atoe milioni yake Hamsini kudhamini halafu unamwambia alipe na *VAT* umuongezee ziada, wakati timu yenyewe haina jina kubwa na itatumia muda mrefu kuleta mrejesho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri huu udhamini mturahisishie vilabu vyetu, viondolewe huu udhamini wa asilimia 18 ili udhamini wa timu karibu zote Tanzania ziweze kupata udhamini na Ligi itaongeza ushindani lakini pia vijana watapata ajira naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima lakini nikushukuru na wewe kunipa nafasi hii kuweza kuzungumza katika bajeti hii ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, tunapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha salama kwenye bajeti hii ya pili ya Bunge hili la 12 ambalo pia ni bajeti ya pili ya Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kwanini nikasema hivyo, kuna usemi unasema kwamba Mungu angelifanya siku zote kwamba ndiyo usiku, basi tusingepata mwangaza, lakini angelifanya Mungu kwamba siku zote kuwa nimchana tu hadi ikafika dunia kuisha tusingeweza kuhesabu siku. Lakini tumeweza kuhesabu siku, siku tukafanya wiki, wiki tukafanya mwezi, na mwezi tukafanya mwaka na sasa hivi tuna miaka miwili. Kwa hiyo, tunasema kwa Mheshimiwa Mwigulu kwamba hii ni bajeti yake ya pili, ulipita mwongo wa mwaka jana leo amekuja kutupa utekelezaji, lakini na hii ya mwaka huu tutakuja kuitazama tena hizi ahadi ambazo alizotupa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, waswahili tuna msemo wetu tunasema kwamba *mchamago hanyele* huenda *atawia papo,* yaani utakapoondoka mahali usiseme maneno mabaya huenda ukarudi hapo hapo. Kwa hiyo na Mheshimiwa Mwigulu tunamuomba atekeleze hizi ahadi ambazo alizisema kwenye bajeti hii atakuja *kuwia papo* tutamuona tena pale anasema tena anaweza akataka tusimpe fursa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nizungumze masuala ambayo Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake kwenye ukurasa 102, alizungumzia Serikali inaenda kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya awali ya mapato *(advance income tax)* ya shilingi 20 kwa lita ya wafanyabiashara wa mafuta ya rejareja ya *petrol* nchini, itakayokusanywa na waingizaji wa mafuta kwa jumla ya walipaji hao, lengo alisema kwamba hatua hizi ni kurahisisha ulipaji wakodi katika vituo vya mafuta na kupunguza gharama za ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, sawa tumemsikia Mheshimiwa Waziri amesema hili lengo ni zuri la kutosha shilingi 20 mwanzo kabla mafuta hayajauzwa, lakini tujue kwamba *income tax* ni kodi ya muungano *income tax* ni kodi ya Muungano. Kwa mujibu wa Ibara ya 4(3) ambazo zimetajwa *item* za Muungano, ambayo imeelekeza katika Nyongeza ya Kwanza ukienda katika *item* namba 10 utakuta kwamba *income tax* ni kodi ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kimoja ambacho ni changamoto, Zanzibar katika uingizaji wa mafuta, mafuta yake yanaingia Tanzania Bara kupitia Bandari ya Dar es Salaam, hilo ni kwa mujibu wa *Petroleum Act* kwamba kudhibiti mafuta ya petrol kuingia katika nchi, kwamba ni lazima tupitishe katika bandari ya Dar es Salaam. Hapo hapo Zanzibar mafuta yake yanayopitia hapa yanakuwa kama *transit* yanachukuliwa kutoka Dar es Salaam yanakwenda Zanzibar utakapochaji shilingi 20 *in advance* kwa huyu *wholeseller* wa mafuta kwa maana hiyo mafuta ya yatakayokwenda Zanzibar yameshachajiwa kodi yakienda kule kwamba tayari kodi imekusanywa Tanzania Bara, lakini kwa kuzingatia kuna makubaliano, makubaliano yaliyokuwepo sasa hivi, *income tax* inayokusanywa Zanzibar inabakia Zanzibar na *income tax* inayokusanywa Tanzania Bara inabakia Tanzania Bara, sasa hapa naomba Waziri atupe ufafanuzi juu ya hii *income tax,* itakayokusanywa ya mafuta yanayokwenda Zanzibar ambayo yatakusanywa Tanzania Bara kitafanyika kitu gani hapa atupe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kingine nashauri kwa kuwa mafuta yanayopita Zanzibar yanakuwa *transit* sawa sawa na yanayokwenda Rwanda, basi yaweke katika eneo lake maalum yasichajiwe hiyo *income tax* hapa ili kuepuka hizo gharama za marejesho na muda wa kufanya marejesho ya hiyo *income tax* kwenda Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, wafanye kwamba kama ni *transit* ikachajiwe kule Zanzibar, kwa hiyo hili naiomba Serikali ifanye hilo jambo kwa sababu linaweza likaja likaleta mkanganyiko na baadae tukazalisha kero nyingine ya Muungano kutokana na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo napenda nilizungumze, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza katika ukurasa wa 150 ili kuboresha *blueprint*, kuboresha *blueprint* katika sheria ambayo inahusiana na *TCRA,* ile sheria majukumu ya kuanzisha *standards* yamepelekwa kwa *TBS* na yamepelekwa kwa *TBS* wanasema ili kuweza kufanya mazingira hayo yaweze kuwepo kwa *TBS* kurahisisha katika mazingira ambayo tunaenda kurahisisha ufanyaji wa biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachokiona kitu kimoja ambacho kinaweza kikasababisha uvunjifu wa Katiba ni kitu gani, *TCRA* ni chombo cha Muungano, ambacho kinashughulikia mambo ya mawasiliano, sasa kwa kuwa *TCRA* ni chombo cha Muungano kutoa majukumu ya chombo cha Muungano kuyapeleka majukumu haya kwenye *TBS* ambacho ni chombo kinachotumika kutengeneza *standards* kwa Tanzania Bara, hapo tayari tunakuwa tumeshaharibu na tutakuwa tumekiuka Katiba, kwa sababu kule Zanzibar kuna *ZBS*. Kwa hiyo *ZBS* Kimataifa haiwezi kujulikana Kimataifa, lakini *TBS* anaweza akajulikana Kimataifa, sasa kama tunaweka hizo *standards* na tunavutia biashara na uwekezaji kuweka mazingira vizuri basi Waziri atuambie hapa kitafanyika kitu gani au muujiza gani ili na yule *ZBS* awe na hadhi ile ile Kitaifa na Kimataifa kama na yeye atapewa kutunga hizi *standards* na kufanya hizi *terms* and *conditions* hilo la pili ambalo nimemwambia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu tumesema tumeongeza fedha katika kilimo karibu bilioni mia saba, mimi wasiwasi wangu ni *capacity* ya kwenda kuzitumia fedha hizi, vinginevyo tutazipeleka lakini inawezekana hakuna wafanyakazi wa kutosha. Tulizoea kutumia bilioni mia mbili tisini tunakwenda bilioni mia tisa hamsini hilo la tatu.

Mheshimiwa Spika, jambo la Nne ambalo kwa upande wangu nalisema kama ni *section* ya mwisho, Waziri amependekeza kupunguza gharama kupitia kwa wale Maofisa ambao wamepewa madaraka watakapokuwa yale madaraka yameshuka basi na mshahara wao ushuke, hili naona mimi siyo sawa. Siyo sawa kwa sababu gani, umemuweka mtu Katibu Mkuu amepata muda wa ku-*save* kama Katibu Mkuu amefanya mambo mengi sana katika ukubwa wake ule, na mshahara wake ule mambo yale yamebakia kwenye Taifa hili kama ni faida. Leo hapa kwenye Bunge tunaning'inia kwenye viti tunazunguka humu lakini wale waliofanya kazi hii pengine hawapo siyo waajiriwa wa hapa, pengine hata madaraka yao yameshuka. Sasa tukisema kwamba tunawashusha mshahara tunakwenda kuwaathiri kwenye kiinua mgongo. Tunaenda kuwaathiri katika kiinua mgongo kwa sababu kiinua mgongo kinatazama mshahara wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mshahara wa mwisho wa mtu utakuja kuwa ni mdogo na kiinua mgongo chake kitashuka kumbe, yule mtu alitumia akili zake nyingi sana katika kulitengeneza hili Taifa. Pia kuna athari moja katika hili, watu watakuja kusema kwamba chukua chako mapema, ukishakuwepo kwenye madaraka kwa sababu ukishushwa mshahara unashushwa na kiinua mgongo kinashuka hatima yake itakuja kuwa mbaya, kwa hiyo watu watakuja kusema sasa chukua chako mapema. Hapa tutakuja kukwamisha utendaji na utekelezaji wa majukumu katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ukitunga sheria usimtazame mtu, jaribu kuangalia watu wote, wazungu wanao msemo wanasema hivi *love is to wish your friend good,* mapenzi ni kumtakia rafiki yako jambo zuri, kwa kiarabu anasema *ahibbali-nnasi kama tuhheebu linasi,* wapendelee watu lile ambalo wewe mwenyewe ndani ya nafsi yako unalipenda.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge la Kumi na Moja tulichomoa, tuliambiwa kutakuwa na kodi kwenye kiinua mgongo, sote tulilia hapa tukapoozwa. Kwa hiyo, naomba tuzipende nafasi za wenzetu kama tunavyozipenda nafsi zetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya uchangiaji kwa siku ya leo. Nitataja baadhi ya Wabunge ambao tutaanza nao Mchana. Mheshimiwa Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lililerejea)*

**23 JUNI, 2022**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma M. Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu tunaanza na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali yayote na mimi niungane na wabunge wenzangu kumpongeza sana Rais wa nchi yetu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutuletea maendeleo. Pia nawapongeza wasaidizi wake, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vilevile nimpongeze Waziri wa Fedha kwa andiko zuri lenye mapinduzi makubwa kwa nchi yetu nampongeza Naibu Waziri lakini na watalaam kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani kwa Serikali hii ya Awamu ya Sita. Miradi ya maendeleo katika nchi hii haikuanza awamu hii, imeanza awamu zote zilizopita. Lakini katika Jimbo la Mbinga Vijijini sisi tuna namna ya kipekee katika awamu hii. Hatukuwa na vituo vya afya, sasa hivi ninafuraha

kutamka vituo vya afya vinavyojengwa kwenye Jimbo la Mbinga Vijijini. Tunajenga Kituo cha Afya Muungano, Kindimbachini, tunajenga Kituo cha Afya Mkumbi Kata ya Mkumbi lakini tunajenga Kituo cha Afya Kata ya Matili haikuwahi kutokea, tunaishukuru sana sana Serikali ya Awamu ya Sita. Si hivyo tu, tunajenga Hospitali ya Wilaya, lakini tunajenga pia boma la halmashauri. Ni fedha nyingi zinakuja kwenye halmashauri yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe shukrani kwa mradi wa Barabara ya Kitai – Luanda mpaka Lituhi. Barabara hii kwa muda huu kuna machimbo ya makaa ya mawe, na wananchi wamekuwa wakilalamika muda mrefu kuhusu vumbi. Sasa, Serikali ya Awamu ya Sita imeliona hilo na sasa kilometa 35 mkandarasi yupo *site* ameanza kazi. Mpango barabara hii mpaka Lituhi upo. Barabara hii haiishi pale, inakwenda Ndumbi ambako kuna bandari ya kisasa, bandari kwenye Ziwa Nyasa ambayo Mheshimiwa Manyanya jana aliiongelea. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la magari barabara ya kutoka Makambako kwenda Songea inayopitia Njombe ni finyu sana. Nimeona katika mipango hii, sasa hivi tayari kilometa 120 zinaenda kujengwa, tunaishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizi bado naendelea kushukuru kwa upande wa kilimo; bajeti hii ina mabadiliko makubwa sana. Bajeti hii trilioni moja kasoro bilioni 26 tu; haijawahi kutokea. Nikitumia maneno ya *comrade* Mheshimiwa Mkuchika anasema, haikuwahi kutokea lakini imetokea, safari hii imetokea, bilioni 974. Kwa hiyo tunauhakika sasa mabadiliko makubwa yanaenda kutokea kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ombi langu hapa kwa Wizara ya Kilimo, tunafahamu kutokana na bajeti hii kutakuwa na uzalishaji mkubwa sana kwenye kilimo. Kwa hiyo niombe watu wa masoko, niombe Wizara ijipange vizuri kutafuta masoko ya mazao hayo. Tutakwenda kuhamasisha wananchi walime sana, lakini kama soko halitapatikana wananchi hawa hawatarudia kulima. Maana yake ni kwamba fedha hizi hazitakuwa na msaada tena kwa nchi yetu. Lakini ninauhakika Waziri amejipanga vizuri ametuelezea mikakati mambo haya yanaenda kutokea haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia kwa ile shilingi bilioni 150 ya ruzuku ya mbolea. Sisi wana Mbinga Vijijini bila mbolea hatuvuni. Kwa hiyo tuna matarajio makubwa sana sasa, kwamba tunakwenda kuvuna kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nimesikia minong'ono hapa kwamba utaratibu ule wa kupata hii mbolea unacheleweshwa na watu mmoja, wawili, watatu. Kwa kweli nitoe hapa onyo kubwa sana, watu hawa wasitucheleweshe. Sisi kipindi hiki tunavuna ndicho kipindi hikihiki tunanunua mbolea. Mkulima anatoka shambani anauza mahindi yake gunia mbili, tatu, nne anaenda kuchukua mbolea anahiifadhi. Sasa tukisubiri hawa watu wakituchelewesha itafika mwezi wa kumi na moja hadi wa kumi na mbili mkulima hana fedha ya kununua mbolea. Kwa hiyo niombe sana, Mheshimiwa Waziri mimi nina uhakika yupo vizuri, hawa watu hawataweza kumchelewesha kiasi hicho. Achukue hatua, na mimi nimetoa onyo hapa, wakiendelea tutatafutana huko wanakofanya hizo vurugu zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mpango ule wa wamachinga. Niipongeze sana Serikali kwa kuuona ule

mpango; ni mpango mzuri na muhimu sana. sana lakini shida ni pale tunaposema tunaenda kutoa nini asilimia 10 ile ambayo tumeshawawekea vijana, wanawake na walemavu. Kutokana na umuhimu wake, nafahamu, Mheshimiwa Waziri wewe umeona asilimia 10 namna ilivyofanyakazi tangu tulipoianzisha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mifano michache tu. Mimi katika jimbo langu asilimia 10 tumefanya mambo mazuri mno. Tumefungua kiwanda cha *Innovation Use Group* cha shilingi milioni 42 ambacho kinatengeneza sabuni. Kiwanda hiki kimetoa ajira kwa vijana waliomaliza shule wakakosa ajira wakajiunga wakatengeneza hiki kiwanda kipo Kata ya Mapera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna umoja wa wanawake Mbarawala, wapo Luanda, hawa wametumia milioni 30 kutengeneza kiwanda kidogo cha kuchakata makaa ya mawe. Nimesikia hapa Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anaongelea kwamba wanaleta mitambo ya kuchakata makaa ya mawe ili tuachane sasa na kutumia mkaa huo wa miti. Sisi tumeshaanza kupitia hawa akina mama, wanachakata makaa ya mawe kwa shilingi hizi milioni 30. Si hivyo tu, kuna tumaini Jema kipo Matili; hiki ni kikundi cha walemavu, kimepewa milioni 15. Kuna vikundi vingine zaidi ya hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumehama kuwapa watu milioni sijui laki ngapi hapana tunawaunganisha pamoja tunawapa hela ya kutosha wanafungua viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo sasa hivi Jimbo la Mbinga la Vijijini kila Kata inaviwanda siyo chini ya kimoja, viwili mpaka vitatu. Sasa hofu yangu, tukitoa hii asilimia 10 ikabaki tano mpango huu ambao tuliuimba kwenye Ilani, tuliuimba kwenye kampeni hautatekelezeka, itakuwa athari kubwa na

dosari kwetu sisi, na mimi ndiyo nitapata shida sana kwa sababu niliumba vizuri kweli na wananachi wale wakanielewa vizuri. Kwa hiyo niombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu wa wamachinga ni mzuri, lakini basi tutafute vyanzo vingine ili tuutelekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja nyingine inayohusu watumishi; na ninaomba hapa niongee kwa unyenyekevu na utulivu mkubwa sana. Ninafahamu Serikali yetu ni sikivu sana; na hapa sasa hivi imeshaleta furaha kwa watumishi. Sasa hivi kila mtumishi huko ambaye anaendelea kufanya kazi ana furaha na Serikali hii ya Awamu ya Sita. Shida inakuja wapi, shida inakuja kwenye hii kitu inaitwa kikokotoo. Kikokotoo sasa hivi kinatoa furaha ya watumishi hususani wale wanaotarajia kustaafu au wale wanaostaafu leo na kesho na keshokutwa, furaha imeisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana sana kwa unyenyekevu, Watanzania hawa sasa hivi walishaanza kufurahi, tuwaachie furaha hii iendelee. Suala la kwenda na kikokotoo kipya cha asilimia 33 kimewafanya baadhi ya watumishi sasa hivi wanakimbizana kustaafu kabla ya muda. Shida ikiwa nikutaka wapate ile 50 kwa 50 siyo hii 30 kwa sabini na ngapi hiyo. Niiombe sana Serikali yangu, na ninanafahamu Serikali hii inania njema sana sana kwa watumishi na ndiyo maana imeongeza zile asilimia ishirini na ngapi zile. Ina nia nzuri sana. Nia hiyohiyo naomba iende kwa wafanyakazi hawa wanaostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hata taarifa hii kwenye bajeti tumeongea vizuri sana, wanaolipa kodi nzuri na yenye uhakika ni watumishi. Kwa hiyo watumishi hawa wameihudumia nchi hii kwa muda wote wa ajira. Sasa

wanaenda kustaafu wanatarajia kipato chao cha mwisho kile ndicho kiende kufanya mambo mengine kama alichelewa hapa na pale sasa kwa kumpa hiyo asilimia 33; kwakweli tunatambua nia njema lakini hatuna makubaliano na Mwenyezi Mungu, kwamba huyu mtu baada ya kustaafu ataishi miaka mingapi hakuna.Watu wanaishi leo, na ninaomba hiyo ibaki hivi hivi, kwamba binadamu anaishi leo. Kwa hiyo tukimpa asilimia zake kama mfumo ulivyokuwa unaenda mwache tumuombee Mungu kama ataishi zaidi basi tuombe Mungu aendelee kuishi; lakini mtu anaishi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nitolee mfano mdogo hapa; kwa mtumishi kuna meseji zinazunguka huku nyingi sana. Sina hakika kama kuna Mheshimiwa Mbunge ama hajapigiwa simu ama hajatumiwa meseji na watumishi kuhusiana na hili suala la kikokotoo; kinatoa amani na furaha ya watumishi ambayo ilishaanza kujengeka na walikuwa wanafurahi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwa mtumishi huyu aliyekuwa analipwa mshahara wa milioni moja laki mbili na thelathini tano; kwa *formula* ya sasa hivi atalipwa mafao yake ya milioni arobaini sita; lakini kule nyuma alipaswa alipwe zaidi ya milioni 94, pale panapungufu ya zaidi ya milioni 47 hizi milioni 47 angeweza kufanya kitu fulani cha kumuingizia fedha kuliko hii ambayo tunasema hapa inaenda kuongezeka ya milioni 120. Kwa sababu hapa wanasema kwenye *pension* huyu mtumishi atalipwa 623,733 kutoka 503,000; sasa inaongeza pale 120,000. Huyu mtu akitumia hii hela kwenda kujenga hii nyumba ana uwezo wa kulipwa 200,000 hadi 300,000 kwa mwezi; ameishi, hajaishi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Serikali yangu hii Sikivu, hili eneo la kikokotoo ama tuliache kama lilivyo watumishi walivyolizoea waendelee kuishi lakini kulifanya hivi

tunaenda kuondoa furaha, tunaenda kusababisha *stress* za watumishi baada ya kustaafu nyinyi mnajua watu wanahofuhofu nyingi kwa hiyo tutakuwa na misiba mingi hapa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, ajiandae.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Bajeti Kuu hii ya Serikali ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2022/2023 ambao pia ni mpango wa pili wa Mpango wetu wa Maendeleo wa Tatu wa miaka mitano. Bajeti hii kwa kweli imeonyesha nia thabiti ya kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naanza kuungana na wenzangu wote kwa kumpongeza Mheshimiwa wetu, Mama yetu kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya iliyotukuka kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nampongeza Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri walioifanya. Sitaacha kupongeza kabisa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kati nzuri inayofanya kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imeendelea kuonesha nia njema sana katika kuwajali watumishi wa Tanzania. Unaambiwa usiposhukuru kwa kidogo basi kikubwa hutoweza kushukuru. Tunasema changamoto zipo, ndiyo, lakini Serikali siku zote imeendelea kuonyesha nia thabiti ya kuboresha maslahi ya watumishi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan imeboresha viwango vya posho, tunamshukuru sana mama. Serikali imeboresha na kupandisha madaraja kwa watu wanaostahili na inaendelea kufanya hiyo kazi. Pia Serikali imeridhia kulipa kwa mkupuo mafao ya wastaafu, tunaishikuru sana Serikali. Mambo mengi sana imefanya kwa niaba ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi katika mwavuli wake huo mpana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwakilishi wa wafanyakazi. Wafanyakazi tulikuwa tuna jambo letu, tunaita jambo letu, ambalo lilikuwa ni maombi ya muda mrefu usiopungua miaka mitano; kuhusu suala la kuboresha mishahara ya kiwango cha kima cha chini cha mishahara yetu. Kwa hiyo tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Mei Mosi ya mwaka jana pale Mwanza alisema ataboresha mwaka ujao. Mheshimiwa Rais ni mtu anaye kwenda na kauli zake. Tunamshukuru sana mwaka huu kwa uaminifu mkubwa ameweza kupandisha mshahara wa kima cha chini kwa asilimia 23, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya watumishi wa Tanzania pamoja na Wabunge wenzangu Mama Samia Suluhu Hassan tunasema ahsante tunaendelea kukuombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti yetu hii ya Mheshimiwa Waziri na Serikali, kipengele cha kuboresha tozo

ada na sheria mbalimbali; kuna kipengele cha 108 kwenye sheria inayohusu mfuko wa fidia kwa wafanyakazi. Nia ya hizi sheria hizi sheria na kadhalika inania njema ya kuleta mfumo wa kodi ambayo ni tulivu tunashukuru sana. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri hii sheria ya kuboresha mfuko wa fidia kwa wafanyakazi; naipongeza Serikali imekuwa na nia njema sana ya kushirikiana na sekta binafsi hasa waajiri wa sekta binafsi; kwa sababu mwanzoni kiwango cha mchango huu wa pato ghafi la wafanyakazi kwenye mfuko huu ilikuwa ni asilimia moja kutoka waajiri wa sekta binafsi halafu Serikalini ni 0.5 *percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali kwa kujali ilipunguza kutoka asilimia moja mpaka asilimia 0.6. Hili ni punguzo kubwa sana; na inaonesha ina nia njema na wawekezaji wa binafsi. Lakini sasa kwenye kipengele hiki cha bajeti inayokuja inasema sasa inaenda kuboresha zaidi kupunguza kutoka asilimia 0.6 kwenda asilimia 0.5 kama mwajiri wa Serikali eti vilingane kuwe na usawa. Mimi nasema Hapana, tuangalie vizuri, kwanini, waajiri wa sekta binafsi kuna wakati wanamaliza shughuli zao wanafunga wanaondoka, mashirika binafsi saa nyingine yanakufa Serikali inabeba mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ikumbukwe kwamba madhara yanatokana na kazi *either* migodi ni ya muda mrefu kwa yule muathirika ambaye ni mtumishi. Migodi inafungwa, kama migodi ya *Resolute* wa Nzega ulishafungwa lakini waathirika wanaendelea kutibiwa na huu Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu Serikali inaelemewa, Serikali ni endelevu haiondoki. Kwa hiyo muajiri wa Serikali anaendelea kuchangia lakini yule mgeni ameshaondoka amemuacha Mtanzania ambaye anaugua. Daktari akishagundua kwamba wewe ugonjwa wako umetokana na

tatizo la kikazi anakuandikia moja kwa moja kwenye mfuko wa fidia wa wafanyakazi. Kwa hiyo mfuko utaendelea kukuelemea kwa watu ambao hawaendelei kuchangia kwa sababu muajiri ameshaondoka, na ugonjwa ni wa muda mrefu au wa kudumu. Kwa hiyo mimi nasema sheria hii Mheshimiwa Waziri tuiangalie, haijakaa sawa, vinginevyo tutaipa mzigo Serikali ambayo inachangia kwa uendelevu; lakini yule mwajiri ameshaondoka na mwananchi ameendelea kuugua *either* kwa kudumu au kwa muda mrefu magonjwa haya huwa ni ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala wenzangu wamelichangia sana, lakini nami naomba niseme, kwenye bajeti kipengele cha 34, hili suala la kumpunguzia mteule arudi kwenye ngazi yake ya mwanzo ya mshahara alioteuliwa. Kwanza hakuomba kuteuliwa. Sasa awamu imekuja, hajateuliwa. Kuteuliwa ni bahati, siyo kosa lake. Ila ukumbuke mshahara wa mfanyakazi sio wa mfanyakazi peke yake, una watu wengi nyuma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyakazi akiwa ameteuliwa katika cheo kile, utakuta alikopa; wengine kwenye mabenki, wengine kwenye mashirika kama *National Housing,* wamekopa nyumba, *TBS* wamekopa nyumba. Ameangalia mshahara wake ule akaona atalipaje. Leo unamtoa, unamrudisha kwenye mshahara ule ule. Kwa kweli ni mgororo mkubwa, ni changamoto kubwa, ni kilio kikubwa. Mkumbuke ana jamii kubwa nyuma yake. Kwa hiyo, uchungu hatakuwa nao yeye ambaye hakupata bahati ya kuteuliwa, kutakuwa na uchungu kwa watu waliokuwa nyuma yake, anawaza atalipaje? Hata akienda kufanya kazi kule kwingine, hatafanya kwa ufanisi. Amechanganyikiwa, ana mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naliona katika upande mwingine wa suala zima la kikokotoo. Huu mgogoro unakuja kutukumba kwenye suala la kikokotoo ambalo tunasikia. Mimi kama Mwakilishi wa Wafanyakazi, wananieleza. Linakwenda kuanza Julai mwaka huu. Kikokotoo kitakwenda kuleta changomoto hizo hizo. Labda kwa ajira mpya, mtu anajua kuna kikokotoo sasa nisikope. Ila watumishi wameshakopa wakijua akistaafu atapata fedha kiasi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo umemshushia mafao yake kutoka asilimia 50 mpaka 33, halafu tunasema kundi hili ni asilimia ndogo 19; Asilimia 19 ndio watu gani? Kundi hili linabeba watu ambao wanagusa jamii moja kwa moja. Walimu, watumishi wa afya; hivi Mwalimu anakwenda kufundisha anawaza, Mungu wangu nitalipa nini? Daktari au *Nurse* anatibu mgonjwa anawaza! Kwa kweli hili jambo la kikokotoo tuliangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama amefanya vizuri, Serikali imefanya vizuri, watumishi wamefurahi, lakini sasa wanaanza kupiga kelele za kikokotoo. Ukiangalia ni kweli, mtu alikopa anajua mwisho wa mafao yake atapata kiasi fulani. Leo ukishamshushia, kwa kweli hii tuiangalie vizuri. Pamoja na hili la watu wanaoenda kuchukua ngazi yao walioteuliwa mara ya kwanza kabla hawajateuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye bajeti kipengele cha 31, Mheshimiwa Waziri amesema hivi, Mheshimiwa Rais anakerwa sana na udhaifu uliopo katika suala zima la ufuatiliaji na tathmini ya mambo mengi Serikalini. Mheshimiwa Waziri amesema kwenye kipengele cha 31 mkiangalia kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, niipongeze Serikali imekuja na muundo. Sasa inaandaa sera na baadaye itakuja

na sheria kwa ajili ya hili jambo zima la ufuatiliaji wa tathmini kwenye miradi mbalimbali ya Serikali. Sasa Mheshimiwa Waziri ametenga bajeti, wametoa rasilimali fedha, rasilimali watu na pia wametoa malengo ambayo yatapimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Umeshafungua mradi wako kwa mfano wa Mwalimu Nyerere, umefuatiliwa kama unafanya kazi, unajengwa sawa sawa? Umefanya tathmini, lakini baadaye kuna haja ya kuangalia tija. Mradi umekwisha: Je, jamii inafaidika? Je, tatizo la umeme limekwisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema? Hiki Kitengo cha Tija kiko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Juzi Mama Samia amesema kwenye Mkutano wetu wa Mei Mosi, mnadai mshahara, lakini mbona hamjanipa tija ya Utumishi wa Umma? Kitengo hiki kiwezeshwe, kitengewe sera, kitengewe bajeti, kifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza kwa kuja na sera pamoja na miundo kwa kikundi cha ufuatiliaji na tathmini. Sasa ukishaweka niseme labda huo mradi wa Mwalimu Nyerere; ushafanya tathmini na ufuatiliaji? Tija unapimaje? Kwa hiyo, hiki kitengo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kuleta hiki Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, nakupongeza sana Waziri, ni jambo jema, ofisi hii inafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Aloyce ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye ameniwezesha jioni hii kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kuchangia bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukurani hizo kwa Mwenyezi Mungu, naomba pia nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada anazozifanya za kuhakikisha kwamba nchi yetu inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni Bajeti Kuu ya Serikali, naomba niwashukuru Mawaziri wote, Manaibu Mawaziri na Watendaji wote ambao kwa njia moja au nyingine mmeshiriki kikamilifu katika uandaaji wa bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, sasa naomba nijikite katika mchango wangu. Mchango wangu wa kwanza ni suala zima la kilimo. Nimemsikia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu akielezea vizuri jitihada za Serikali katika kuimarisha kilimo. Naipongeza sana. Nampongeza sana Rais wetu kwa kuamua kuongeza Bajeti ya Kilimo kutoka Shilingi milioni 294 hadi Shilingi milioni 674, ni karibu Shilingi milioni 700. Ongezeko hili ni kubwa sana, na lina stahili sifa. Nina imani ongezeko hili litakwenda kuchochea kilimo chetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya ongezeko hili, Serikali hii ya Awamu ya Sita imefanya makubwa. Mtakumbuka Mama alipoingia madarakani sisi watu wa Mtwara tulibahatika kupata

pembejeo bure, kwa maana ya *Sulphur* na viuatilifu. Jambo hili lilisaidia sana kuinua kilimo na uzalishaji wa korosho, zao ambalo linaiongezea nchi yetu fedha za kigeni. Kwa hiyo, namshukuru sana Mama yetu na wananchi wa Mkoa wa Mtwara wanashukuru sana jitihada za Mama katika kuimarisha zao hili la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, mwaka huu 2021/2022 bado Mama yetu aliendelea kutoa pembejeo bure kwa wazalishaji wa zao la korosho. Hapa namshukuru sana Waziri mwenye dhamana na kilimo, ndugu yangu Bashe. Kwa kweli alifanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba pembejeo hizi zinawafikia walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu katika jambo ambalo limenifurahisha zaidi, Waziri wa Kilimo nataka nikwambie, ule utaratibu ulioweka wa kuwashirikisha viongozi wa vijiji kwa maana ya Wenyeviti na Watendaji, Viongozi wa Vitongoji na ile Kamati ya Ulinzi na Usalama kugawa hizi pembejeo, umefanya jambo la maana sana. Kwa sababu umeshirikisha Serikali yote, tuna uhakika wananchi wanaostahili kupata pembejeo, watapata pembejeo. Hongera sana ndugu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tumemsikia Waziri mwenye dhamana akiwa anawasilisha bajeti yake, ameeleza, kuna mabadiliko ya sheria ya *Export Levy,* kwamba kuanzia mwaka huu, ule mfuko wa *Export Levy* ambao ulifutwa, utarejeshwa. Hili jambo linastahili pongezi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu mfuko huu ulipoanzishwa ulikuwa na malengo ya kuinua uzalishaji wa zao la korosho. Mfuko huu ndiyo ambao ulikuwa unanunua pembejeo, unazalisha miche, unafanya *research and development* kwa watu wetu wa Naliendele, na mfuko huu

ndiyo ambao ulikuwa unawasaidia Maafisa Ugani kule vijijini. Kwa hiyo, kitendo cha kurudisha mfuko huu, imeonesha jinsi gani Serikali inavyothamini zao hili. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu yangu Mheshimiwa Bashe, naomba nimwambie, mfuko huu ulipoanzishwa, fedha hizi zilikuwa zinawekwa kule kule Mtwara. Sasa ndani ya andiko la Mheshimiwa Waziri amesema fedha hizi asilimia 50 zitabaki Wizara ya Kilimo. Yewe unajua maana ya mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu, hii Wizara Mheshimiwa Bashe akiondoka, hizi fedha hazitatumiwa vinginevyo? Kwa sababu ni zao moja tu lenye *Export Levy* hapa Tanzania, zao la korosho. Sasa ndugu yangu Mheshimiwa Bashe nakuomba, lazima ujengewe kanuni na taratibu, vinginevyo mfuko huu upelekwe Mtwara kwenye Bodi ya Korosho. Kwa sababu watakuja watu wengine wasiotutakia mema, wakakuta mamilioni ya fedha pale, wakaanza kuzitumia tofauti. Watalipana posho pale, watafanya safari, kumbe lengo la mfuko huu ni kuliendeleza zao la korosho. Hatutarajii fedha hizi zitaenda kwa matumizi tofauti na zao la korosho. Kwa hiyo, kwa jambo hili naomba utilie maanani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze kwenye suala la maji. Naomba tena nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais, kwani watu wa Mtwara tulikuwa tuna shida kubwa sana ya maji. Ilifikia hatua ndoo ya maji tunanunua kwa shilingi 2,500. Namshukuru sana Rais, alituita pale Ikulu, tulienda kuzindua utiaji wa saini wa miradi mikubwa. Kule wenzetu wa Newala, Tandahimba na Nanyamba, mradi wa Makonde umefunguliwa kwa thamani ya mabilioni *of funds*. *Contractor* wa Kichina amechaguliwa na ataanza kazi hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Nanyumbu, mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kuleta Mji wa Mangaka tumeshatia saini. Ndani ya mwezi Julai mradi huu unaanza kazi. Ndugu zangu, Mama huyu anafanya kazi na kuna kila sababu ya kumwombea uhai na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba ndugu yangu Waziri wa Maji, mradi huu uko kilometa 95 kwenye chanzo hadi kufika Mji wa Mangaka. Kwa bahati mbaya Mji wa Mangaka hauna mamlaka ya maji. Nakuomba anzisha mamlaka ya maji ya Mji wa Mangaka na Kilimanihewa ili waweze kuusimamia mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mradi huu ukasimamiwa kutoka kilometa 150 yalipokuwa Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji ya Masasi. Fedha nyingi zitatumika kulipana posho kwa watendaji kuliko kufungua Mamlaka ya Maji ya Mji wa Masasi. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri, hili jambo alitilie maanani sana. Tunataka mradi wa maji uanze na usimamiwe ndani ya mamlaka ya maji ya Mangaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu linahusu sheria ya asilimia 10. Mheshimiwa Waziri umesikia malalamiko mengi ya Waheshimiwa Wabunge, naomba uwe msikivu kwa hili. Nitakupa mfano mmoja. Ndani ya wilaya yangu bajeti yetu kwa mwaka ni shilingi 1,600,000,000. Asilimia 10 ni shilingi milioni 160. Kwa hiyo, sisi tunatumia shilingi milioni 160 kutoa mikopo kwa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema uchukue asilimia tano kwa ajili ya miundombinu na masoko, maana yake unachukua shilingi milioni 80, unaweka kule, unabaki na shilingi milioni 80. Katika shilingi milioni 80, unasema asilimia mbili ni ya akina mama; asilimia mbili, vijana; asilimia moja, watu wenye

ulemavu. Maana yake unagawanya shilingi milioni 32, milioni 32 na milioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina vijiji 93, vitongoji 560, unagawanya shilingi milioni 16, tunafanya mchezo! Jambo hili tusipokuwa waangalifu litatuletea mgogoro mkubwa sisi Wabunge. Leo hii tukienda vijijini, wananchi wakilalamika tunawaambia msiwe na wasiwasi upo mfuko. Leo shilingi milioni 16! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linanisikitisha sana, mimi ni Mbunge wa Jimbo ingawa ni mlemavu. Ndugu zangu Shilingi milioni 16 nikawagawie walemavu, atapata nani atakosa nani? Mtatupa mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wa Fedha, kwa mapenzi makubwa, uondoe wazo la kubadilisha hii *rate* ya asilimia 10. Kama kuna uwezekano lazimisha hiki kiwango kiongezeke iwe hata asilimia 15 mpaka 20. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni sheria ya manunuzi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umemalizika.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda siyo rafiki, mengine nitayapeleka kwenye maandishi. Nashukuru sana. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Ally Mhata. Nilimtaja Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga ajiandae.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya kwenye Taifa letu hususan kutusaidia kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo katika wilaya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, lakini nampongeza zaidi Waziri wa Fedha. Ndugu yangu Mheshimiwa Dk.t Mwigulu kazi aliyoifanya ya kumshauri Rais kuhusiana na masuala ya fedha inakwenda vizuri. Mimi ni shahidi na Jimbo la Kaliua ni jimbo ambalo linanufaika na miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika ile miradi ya maji ya miji 28, Kaliua tunakwenda kunufaika na maji ya Ziwa Victoria kutoka Tabora kwenda Kaliua. Maji yale yakifika Kaliua, yanapita Kata ya Usimba, yanapita Kata ya Kazaroho, yanapita Igwisi, yanapita Kaliua yenyewe, yanapita Ufukutwa na yanapita Ushokola. Hii kazi ni kubwa, ni lazima tupongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa lingine ambalo nimesimama nianze nalo kupongeza, ni suala zima la kilimo. Mwalimu Nyerere mwanzo wa utawala wake alituambia kabisa kilimo ni uti wa mgongo. Nampongeza sana Mheshimiwa Bashe. Kwa kweli kwa *vision* ya ushauri wake kwenye suala la kilimo, mimi naamini kabisa kwa asilimia 100 nimefurahishwa sana na utendaji wa huyu bwana, ni mwenzetu lakini anavunja rekodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tabora na Kaliua, sasa bei ya tumbaku imekuwa ni bei *almost* mara mbili, kitu ambacho hakijawahi kutokea. Kwenye tumbaku tulikuwa tunapewa *limit* ya kulima. Unaambiwa lina kilo 1,000, usizalishe zaidi ya kilo 1,000. Uwezo wa kuzalisha kilo hata mamilioni tulikuwa nao, lakini sasa wanunuzi wamekuja wa kutosha, wanagombania masoko. Kwa hiyo, tuna uwezo wa kuzalisha na kuuza tumbaku kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wananchi wa Kaliua, kwa awamu hii tumejipanga mapema kulima kilimo cha tumbaku kwa nguvu zetu zote. Ni ombi moja tu ambalo naweza kumwomba Mheshimiwa Waziri. Moja, naomba pembejeo za tumbaku zifike kwa wakati na kwa bei ambayo wananchi wa kawaida wataweza kununua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo naomba pia, Halmashauri zetu baada ya kununua tumbaku, kuna halmashauri bado zinadai *Cess* ya tumbaku ikiwemo Kaliua. Kwa hiyo, naomba zile fedha ambazo tunadai baada ya kuwalipa vyama vya msingi na wakulima wetu, sasa walipe kwenye Halmashauri ili yale mapato ya ndani yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwenye suala la mishahara ya viongozi, wale ambao tunasema utenguzi wa nafasi mbalimbali. Nasema kwamba siishauri Serikali kwamba labda ulikuwa ni Mkurugenzi kwa bahati mbaya, mabadiliko ya utawala yakatokea, pengine hujafanya kosa, ukaondolewa kwenye nafasi yako, halafu tuondoe ile mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza, sasa hivi wanateua mtu ambaye yuko mtaani, anaingia moja kwa moja kwenye *post*. Unapotaka kusema kwamba namtengua nimrudishe kwenye

cheo cha mwanzo, kipi? Kwa sababu vipo vyeo kwa mujibu wa utumishi wa umma. Mimi kwa *qualification* zangu naweza nikaajiriwa kwenye vyeo vitano. Unanirudisha kwenye cheo gani mimi nimetoka *street*? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokishauri, zamani ilikuwa teuzi zinapofanyika, unamkuta ni Mkuu wa Idara. Wakuu wa Idara karibu kila Halmashauri wako karibu 19 pamoja na vitengo vyake. Sasa hivi, unamkuta mtu ni Mkuu wa Idara *competent*. Sasa tofauti ya mshahara mfano wa Mkurugenzi na Mkuu wa Idara ni shilingi 200,000. Kwa hiyo, ukimpandisha Mkuu wa Idara kwenda kwenye nafasi ya Ukurugenzi au nafasi inayofuatia pale ya *LSSE* unakuwa huja-*create gap* kubwa sana la mshahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapomtoa mtu *from nowhere,* sijui naeleweka! Unasababisha *wage bill* inakuwa kubwa. Yaani unanipa mimi Kwezi shilingi milioni tatu labda na nusu, ambayo nilipokuwa Mkuu wa Idara nilikuwa napata shilingi 3,500,000 nilikuwa na nafuu zaidi ya kutoku-*create* ongezeko kubwa la mishahara kwenye Serikali yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri jambo hili tuliangalie vizuri sana. Pia hizi nafasi, kwa sababu ni mabadiliko na lazima, hata kama ningekuwa mimi ili watu wanisikie na kunielewa, lazima niende nikafanye mabadiliko. Ndiyo maana ya *chain of command*. Sasa hicho kitu siyo kibaya lakini wale ambao wanakaa pembeni, tuangalie zile *posts* za kuwaweka. Kinyume cha kusema kwamba tunaenda kumnyang'anya mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea ukitafuta takwimu, siamini kama kuna Mkurugenzi yeyote hajakopa hapa. Hawapo, yaani utakuta ameshakopa labda imebakia ile

*limit* ya *one third* ya kwenye *LAWSON*. Sasa kama mtu alishakopa akafikia huko, unamwambia eti ni hivyo, kwanza tunawa-*demoralize* lakini hatujafanya utafiti wa kutosha wa kuona kazi nzito wanazozifanya hawa watu. Kwa sababu ndugu zangu, kazi wanazozifanya Wakuu wa Idara, Wakurugenzi na watu mbalimbali hawa wenye *post* za uteuzi, ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya kazi hapa za *control* hela, uelewe kabisa ikipotea hapo ni mahakamani, dakika mbili tukisema huko hela imepotea Mkuu wa Idara ame-*misuse* nafasi tunapigia Mkurugenzi. Unapigia Mkurugenzi, hapa tunatoa mfano wa Jiji la Arusha juzi, jamaa yupo ndani tunavyoongea. Sasa ndio nasema kwamba kuna *risk* kubwa sana hebu tuwaachie hii mishahara, tuangalie *source* zingine za kupata fedha. Kwa hiyo naendelea kuwashauri kwamba, tuangalie kwenye teuzi zetu, tuangalie hilo ili *control wage bill* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia kwenye ile asilimia tano ambayo Waziri amesema iende kwa Machinga na tano nyingine ibaki kwa maana ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, jambo hili halijakaa vizuri kwa sababu gani Halmashauri za Wilaya nyingi ukisema unajenga masoko tutajenga mpaka lini, kwa sababu masoko mengi ni magulio. Leo wanazunguka hapa na magari, tarehe fulani watakutana Kongwa, tarehe fulani sehemu fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yanawezekana kwenye Halmashauri za Miji au Manispaa au Majiji, lakini kwenye Halmashauri za Wilaya maana yake tunaenda kuipoteza fursa nzuri kama hii. Kwa hiyo nawashauri, halafu nilikuwa najiuliza sasa tukiweka *five percent* tukajenga masoko mwaka huu, sheria imeshapitishwa kwamba ni *five percent,* tutaendelea

kuwa tunajenga, tunajenga, tunazurura na kuzunguka, nikawa najiuliza kata zangu mimi za Kaliua 13 zote, kila sehemu ni magulio, je tutaendelea katika hali hiyo? Naishauri Serikali yangu iliangalie vizuri jambo hilo na ikiwezekana waongeze kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyoshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine, unahusiana na ile mikopo ambayo wananchi wetu wafanyabiashara wananyanyasika kule. Mtu anakuja kukopa shilingi milioni 30 kwenye benki, anakwenda ana-*trend* vizuri, anapata *emergency* inabakia milioni tano, taasisi zetu za benki zinaenda kuuza nyumba. Watu wanakufa kwa presha, lakini bado hata *interest* jamani tuangalie. Mimi nikijiona niko bora lazima nimpende na jirani yangu, haina sababu ya kuwa na asilimia 17 mpaka 21 ambayo mabenki bado yanatoza, ni kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliangalie ili tuwasaidie wafanyabiashara na wakulima wanapoenda kukopa wawe na angalau mambo ya chini kidogo. Pia watumishi, maana yake na watumishi hivi tunaongea mama aliposema jambo zuri sana, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, la ile asilimia 23, kuna watu wameshajiandaa kupandisha bei, niiombe Serikali wajitahidi kuwa wakali na ku-*control* bei, kwa sababu kuna mwingine anapandisha kiholela, yaani anaamua tu kwamba kesho naamka cement bei Fulani, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikikemea, haya mambo yanakaa vizuri wanasubiri asilimia 23, sasa watumishi watashindwa kuona *impact* ya ongezeko la mshahara. Kwa hiyo nashauri hapo lazima tujiandae ku-*control,* lakini hata taasisi zetu za benki ziangalie hawa watumishi kupunguza zile

asilimia ili na wenyewe wawe na maisha bora na maisha ya nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri vile vile, kuna upungufu wa vifaa vya hospitali, tumejenga hospitali na vituo vya afya vingi sana lakini huduma bado haijaboreshwa. Kwa kuwa zimetangazwa ajira nyingi zinakwenda, naomba tuangalie suala la haraka la ku-*rescue* masuala ya madawa. Upatikanaji wa madawa na vifaa vya tiba sio mzuri. Kwangu kule kuna vituo vya afya vitatu vinajengwa na hospitali moja ya wilaya, kwa hiyo, isibaki kama *white elephant*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi. Tunaendelea na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki wajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza kwa moyo wangu wa dhati Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara nzima, kwa namna ambavyo bajeti kila ukurasa ukijaribu kuangalia unakutana na ajenda ambazo zinahusu masuala kuwasaidia Watanzania na hususani vijana katika namna bora ya kuwawezesha kupata mitaji, lakini kujikwamua kiuchumi na mambo kadha wa kadha. Tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika masuala mawili; kwanza kwenye ardhi, lakini pili upande wa asilimia 10 za vijana akinamama na watu wenye ulemavu. Nikianza na

upande wa ardhi nichukue nafasi hii kwa moyo wa dhati, wa kizalendo na wa kipekee wa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameweza kutenga bilioni 50 kwa ajili ya kuisaidia Wizara ya Ardhi ili kwenda kupima, kupanga na kurasimisha ardhi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yetu ni kubwa kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu fedha hii itatumika kwenda kusaidia wananchi kupanga, lakini pia itasaidia sana kwenda kutatua migogoro ya ardhi, katika nchi yetu ya Tanzania. Niombe sasa Wakurugenzi wote watakaopata fedha hizi kwa awamu ya kwanza waweze kuwa waaminifu, kuwa waadilifu ili waweze kufanya kazi hii kwa uaminifu na kuweza kurejesha fedha hizo na ziweze kusaidia Watanzania wengine kwa maana ya halmashauri zingine na kukidhi kiu ya Mheshimiwa Rais ya kuamini katika kutatua changamoto kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia nafasi hii kuwaomba Wakurugenzi wote wa Halmashauri na hasa zile halmashauri zenye miji midogo kuhakikisha kwamba wanatumia takwa la kisheria Na.8 ya mwaka 2007 inayowataka kutenga fedha ya kuweza kupima, kupanga na kurasimisha ili kuhakikisha wote kwa pamoja tunaweza kuziunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais na kuhakikisha kwamba zile bilioni 50 alizozitoa basi zinaweza kuungwa na halmashauri hizi ili kuweza kufikia lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza pia na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa Shilingi bilioni nne kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Tunaamini kabisa, Mheshimiwa Rais nia na dhamira yake ni njema, hivyo watu wote ambao wamepewa dhamana na jukumu, waweze kuhakikisha kwamba wanaenda kufanyia kazi ipasavyo hizi fedha ili kuweza kutatua changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwa upande wa asilimia 10 za akinamama nne, vijana nne na mbili wenye ulemavu. Naiomba sana Serikali yetu sikivu ya Chama cha Mapinduzi isipunguze fedha hizi bali iongeze ikiwezekana, kwa sababu vijana wetu wengi na hasa ukizingatia kwa sasa hivi, makundi ya vijana wanaomaliza vyuo vikuu na wanakosa ajira na tunawaelekeza kwenye halmashauri waende wakape mikopo, makundi ya vijana wa bodaboda ambao hawajapata fedha tunawaelekeza waende halmashauri wakapate mkopo, makundi mengine yote ya vijana na akinamama tunayaelekeza yaende halmashauri yakapate mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri zamani watumishi wetu, watendaji wetu, walikuwa sio waaminifu na wakawa wanajigawia fedha hizi na kurudi kwenye mfuko wa nyuma na kuzichukua fedha hizi na zikawa hazina manufaa kwa Watanzania, lakini kwa sasa na hasa ukizingatia mwendo wa uhuru wa mwaka huu wa mwaka 2022, kazi kubwa ambayo inaifanya ni pamoja na kufunga miradi yote ya fedha za asilimia nne kwa vijana. Tumeona na tumeshuhudia miradi ya vijana wa bodaboda, miradi mbalimbali ambayo imeweza kunufaika kupitia asilimia hizi za halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia nafasi hii kwa ridhaa yako, naomba niwataje vijana wa kizalendo kabisa vijana wa Kitanzania wanaokimbiza Mwenge wetu wa Uhuru na wanaohakikisha kwamba kila halmashuri yenye dosari ya miradi ya asilimia nne za vijana, wanawachukulia hatua na wanawasema hadharani. Naomba nimtambue Ndugu Sahiri Nyanzabala Geraruma, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022; Ndugu Rodrick Ndyamkama, Ndugu Ally Juma Ally kutoka Unguja, Ndugu Emmanuel Ndege Chacha kutoka Kagera, Ndugu Zadida Abdallah Rashidi kutoka Pemba na Ndugu Glorian kutoka Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kuendelea kutanua goli, goli la asilimia 10 na kuongeza kufika hata asilimia 15 kwa sababu imekuwa ni sehemu ya kusaidia akinamama, vijana na watu wenye ulemavu katika suala zima la ajira. Tumeona manufaa sasa kwa halmashauri na zaidi iwe *alert* kwa Wakurugenzi wote nchini kuhakikisha sasa fedha hizi zinaendelea kusimamia, lakini pia Maafisa Maendeleo ya Jamii kuhakikisha wanawasaidia vijana kuendelea kuzisimamia fedha hizi kwenye biashara zao ili ziweze kuleta tija, lakini pia waweze kuzirudisha kwa wakati pindi wanavyopata faida na uweze kuwa mzunguko wa kuwasadia vijana wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru kwa kunipa nafasi, kubwa zaidi nasisitiza asilimia 10 za vijana ndio kimbilio letu sisi vijana na kilio chetu, tunaomba fedha hizo ziongezwe ili ziweze kuwasadia vijana wanaomaliza *VETA* na maeneo mbalimbali na wanakosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Samia Suluhu kwa kuondoa ada ya kidato cha tano na cha sita, ameweza kuwakomboa wazazi wengi wa Kitanzania kwa sababu hata ni hivi juzi tu karibuni, wazazi ambao wamepangiwa watoto wao shule za mbali walianza kupitisha mabakuli na kuendelea kuombaomba, lakini sasa tunaona suluhisho lao limeweza kutatuliwa kwa nchi nzima na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nipende kusema Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan vijana tuko pamoja na wewe na majibu yetu utakutana nayo 2005 kwenye sanduku la kura. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga. Tuendelee na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga wajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia Bajeti hii ya mwaka 2022/2023. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataallah* kwa kutujalia uzima, salama na kuweza kusimama hapa mbele na kupata sehemu ya kuchangia bajeti hii. Hali kadhalika ningependa pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu na timu yote ya Wizara kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti hii na kuiwasilisha vyema na hadi kufikia wakati huu tunaichangia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru kwanza vilevile na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na zaidi katika *Royal Tour* kwa sababu hii, ametuashiria zawadi nzuri Tanzania na Zanzibar kwa ujumla wake kwa sababu sasa hivi wahifadhi na wenzetu wa utalii tunasimama kifua mbele tukiwa tuna dhana ya kufanyia kazi katika shughuli zetu za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikianza na shughuli za uratibu wa hifadhi hai, ningependa sisi wahifadhi watu wa maliasili na wenzetu wa mazingira tukajiongeza, Mama ameshafanya kazi nzuri na sasa sisi tujiongeze katika hifadhi zetu hizi kwa sababu kwa mfano, Zanzibar kwetu kuna Hifadhi Hai ya Jozani na Ghuba ya Chwaka. Toka mwaka 2016 hifadhi hii ilipopata usajili hadi leo bado haijakamilisha shughuli zake za usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Muungano na Mazingira ambaye ni mratibu wa shughuli za hifadhi hai Tanzania akalichukua hili ili kuweza kuhakikisha kwamba hifadhi hii ambayo tayari imeshapata *recognition* ya *UNESCO* ya kuwa ni hifadhi hai sasa inakwenda kukamilisha utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ambazo zinataka zikamilike kwanza kuwa na Bodi ya Utekelezaji wa Hifadhi Hai, kuwa na taasisi ambayo itakuwa imechaguliwa kuwa kama *care taker* wa hifadhi hai, lakini hali kadhalika kuwa na mpango kazi wa utekelezaji pamoja na kanuni. Sasa Mheshimiwa Waziri anayehusiana na masuala ya Muungano na Mazingira ambaye ndiye Mratibu wa shughuli za hifadhi hai asaidie hili ili ile kazi ya Mama ya kwenye *Royal Tour* basi iweze kupata thamani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwenda moja kwa moja kwenye uratibu wa Mifuko ya Fedha na zaidi kwanza niingie kwenye mikataba. Juzi hapa wakati nachangia hapa Bungeni nilizungumza kwamba kuna Mikataba ya Kikanda na Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Bahati mbaya Baraza la wa Wawakilishi Zanzibar hawakuwa kuridhia, lakini utekelezaji unaendelea sasa wenzetu kule wa Zanzibar wanapata shida katika utekelezaji wa mikataba hii. Nilitoa mfano, kuna mkataba mmoja unaitwa *Basel Convention* mkataba ambao unahusiana na masuala ya biashara ya vyuma chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mzanzibari akitaka kusafirisha vyuma chakavu inabidi atoke Zanzibar aje Dodoma atafute kibali wakati tungeweza kuwa na taasisi mwenza Zanzibar kama vile *ZEMA* wakaweza kufanya kazi hiyo badala ya kwamba *NEMC* wakawa wanafanya kazi hii peke yao. Hali kadhalika kuna mkataba huu wa *CITES* mkataba ambao

unahusiana na masuala ya usafirishaji wa viumbe adimu, viumbe hai. Huu pia Zanzibar kule mchakato ulianza lakini haukukamilika, sasa ningeomba Waziri husika akakaa na wenzetu wa Zanzibar kule ule mchakato ukamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunatakiwa tuchague *scientific authority and management authority* ambazo zitasaidia kuweza kutekeleza ule mkataba kwa upande wa Zanzibar na kuwasaidia Wazanzibari kuweza kupunguza muda wa kufuatilia vibali Dodoma. Kwa sababu kama Mzanzibari anataka kupata kibali cha kuweza kusafirisha mnyama hasa viumbe adimu, inabidi atoke Zanzibar aje Dodoma. Kwa hiyo naomba pia na hili wenzetu waratibu ambao ndio *care taker* wa huu wa mkataba ambao wako *based* Dodoma huku basi watusaidie kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuongelea suala lingine la uratibu wa Mfuko wa Jimbo. Mfuko wa Jimbo unatusaidia sana hasa Zanzibar, kwa sababu Zanzibar mwezangu juzi aligusia hapa Mheshimiwa Haji, kwamba Wabunge kidogo uratibu umekuwa sio mzuri sana kama ulivyokuwa kwa wenzetu Tanzania Bara. Sasa naomba tu kwamba huu Mfuko wa Jimbo tukaufanyie mapatio kwa sababu, utekelezaji wake huko *general* yaani utekelezaji wa Tanzania *Mainland* tunauchukua hivyo hivyo Zanzibar, sasa hizi changamoto tungefanya mapitio tukazibainisha, tukaweza kuboresha hili huu Mfuko wa Jimbo ukawa una tija zaidi kwa sababu kama fedha za mwakilishi hazijaenda halmashauri kwa nini fedha za Mbunge ziende halmashauri. Nafikiri tuna uwezo wa kuweza kufanya vizuri zaidi na hizi fedha, zisiende moja kwa moja halmashauri tukatumia ule utaratibu ambao wenzetu Wawakilishi wanautumia kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala za fedha za mabadiliko ya tabia nchi na mazingira kwa ujumla wake. Nina wasiwasi kuwa tunapoteza pesa nyingi sana katika Mifuko hii ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira, kwa mfano, kuna Mfuko wa *Adaptation Fund, Green Climate Fund, LBCF*. Mifuko yote hii inapata mchango kutoka kwa wenzetu Umoja wa Mataifa, lakini kwa upande wa Zanzibar hakuna ufuatiliaji mzuri na matokeo yake kuna miradi naikumbuka toka mwaka 2016 imeanzishwa, lakini mpaka hii leo miradi ile haikuweza kukamilika, sio kutekelezwa yani kuandikwa na *allocation* ya fedha tayari ilishatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna mradi ulitayarishwa mwaka 2016 kwa kutumia *allocation* ya *fund* ya *GCF*-6, hivi sasa tunaenda kwa *GCF-8*. Sasa *GCF*-6 mpaka hivi leo ule mradi haukukamilika kutayarishwa na fedha zake hazijaanza kutumika. Sasa sijui kama zimeshapotea au vipi, sasa naomba tu tungeunda *task force* ambayo itakuwa inaratibu shughuli za Mifuko hii kwa Zanzibar au Tanzania kwa ujumla wake. Tukachukua wajumbe watano Tanzania *Mainland* tukachukua na wajumbe watano Tanzania *Island*, waka-*implement* kuweza kutekeleza hii Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuzungumzia changamoto za mabadiliko ya tabia nchi. Kila Wizara ambayo imesimama imezungumzia kuhusu suala la mabadiliko ya tabianchi na kwamba ni changamoto inayokwamisha shughuli zake za kibajeti na maendeleo. Sasa naomba kwanza kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Jafo kwa kuja na Mpango Kabambe wa Usimamizi wa Uhifadhi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kama alivyokuwa ameombwa na

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba aweze ku-*allocate* fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Usimamizi wa Maliasili na Hifadhi ya Mazingira tuweze kufanya hivyo. Pia nawapongeza mabalozi ambao Mheshimiwa Jafo amewachagua ambao wanaufanyia kazi huu mpango kazi, mabalozi wamefanya kazi nzuri na vizuri tukawapa motisha ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna vyuo vyetu kama Chuo Cha Mipango. Chuo hiki kina kozi ya masuala ya mabadiliko ya tabianchi yaani *Urban Planning and Environment*. Sasa hao pia nao ni wa kuwapongeza, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Ardhi kuwaona, tukaweza kuwasaidia kwa sababu ni kozi nzuri na ambayo imejiongeza moja kwa moja kuweza kushughulikia mazingira pamoja na kupima ardhi katika maeneo mbalimbali. Sasa naomba tu, kuna mwenzetu mmoja aliwahi kuchangia hapa Bungeni akasema kwamba kuna tatizo vyuo vingine kozi hazieleweki. Sasa napenda nijiongeze kwa sababu Chuo cha Mipango *they are so creative* na wametuwezesha kuweza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hapa, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, tunaendelea na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Serikali kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuja na

bajeti ambayo kiukweli inaonyesha wazi jinsi Serikali hii ilivyojali maslahi ya wananchi wote, haya yamedhihirishwa wazi katika kile kipengele kinachoonyesha ni jinsi gani Serikali inavyoenda kubana matumizi kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaposema inaenda kuandaa utaratibu utakaowawezesha kuwakopesha watumishi wenye hadhi ya kupatiwa magari ya Serikali jambo ambalo litapelekea watumishi hawa kuyamiliki yale magari wao wenyewe na kubeba gharama zote za matengenezo pamoja na vipuli, hili suala siyo geni ni suala nzuri lakini linahitaji maboresho zaidi, tusiishe kubana matumizi katika masuala ya magari tu na kukopesha wale watu ambao wanaonekana wana hadhi ya kupata hii mikopo kwa kutumia vyeo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni lazima iende mbele zaidi kwa kuangalia utaratibu na uwezekano wa kuwakopesha pamoja na kupunguza kodi kwa Watumishi wote wa Umma ambao wanahitaji kuwa na magari na vyombo vingine vya usafiri kama vile magari yenyewe pikipiki pamoja na bajaji. Jambo hili litaenda kuondosha usumbufu kwa watumishi wetu na suala la kukopesha kwa kuzingatia kigezo hicho tunaenda kuwanufanisha wengi zaidi kuliko kukopesha kwa kuzingatia kigezo cha hadhi na nyadhifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke ya kwamba suala la usafiri ni suala la huduma siyo suala la anasa, katika mazingira kama hayo watumishi wengi na wao wanahitaji kupata huduma bora, kwa hiyo tuweke mazingira halisi ya kuweza kuwakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea zaidi na suala hilo pia unaposema unaenda kumkopesha mtu kwa kuzingatia kigezo cha hadhi aliyokuwa nayo katika utumishi wa umma

maana yake nini? Hadhi ni kitu ambacho kina uwezo wa kushuka na kupanda leo hii unamkopesha mtu mwenye hadhi ya Ukurugenzi, utamkopesha *land cruiser* au utamkopesha hizi V8 kwa mujibu wa hadhi yake, lakini wakati anapomaliza utumishi tujiulize lile gari itakuwaje, hivi anapotoka kama muajiriwa yule alikuwa ni Mkurugenzi leo hii anastaafu baadaye gari lake litabakia na hadhi ya Ukurugenzi yeye ataenda kwenye hadhi ya ustaafu, sasa katika mazingira kama hayo huyu mtumishi utaenda kulazimika kuuza hili gari kwa bei isiyo stahiki ili mradi tu atafute gari lenye hadhi inayofanana na yeye kwa rika yake ya kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hili nasisitiza tena, wazo la kukopesha kwa ajili ya kubana matumizi ni wazo nzuri, lakini utekelezaji wake ni lazima uangaliwe kwa umakini zaidi, hasa katika kuangalia kigezo cha kipato cha mtumishi kuliko kuangalia hadhi waliyonayo. Kwa sababu kuna wakati mwingine watumishi wa kawaida wanakuwa na kipato kikubwa kulinganisha na hadhi zao na katika mazingira kama hayo, wanao uwezo wa kurejesha fedha ndani ya muda unaotakiwa. Sasa tuangalie jinsi gani tunao uwezo wa kuwasaidia watumishi wa namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba Serikali kwa namna yoyote ile haiwezi ikakwepa gharama katika utekelezaji wake hususani katika masuala ya magari, Serikali inamiliki vitu vingi vya thamani, Serikali inamiliki magari, Serikali inamiliki majumba, Serikali inamiliki hospitali, tuchukulie mfano katika hili suala la hospitali hivi kwanini kama kweli tunayo nia halisi ya kubana matumizi, kwanini tunazingatia hadhi za mtumishi halafu tunatoa kigezo cha kukopesha, leo hii tumchukue Daktari Bingwa kutokana na hadhi yake halafu tumwambie kwamba hii *X-Trail* hii ni yako tunakukopesha, kafanyie kazi sisi tutachangia umeme au chukua gari la wagonjwa halafu

mwambie kwamba dereva wewe kutokana hadhi yako tunakuachia hili gari tunakukopesha wewe fanyia kazi, tutachangia masuala ya mafuta, masuala ya vipuri na mambo mengine utakuwa unahudumia wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kama huu Serikali ni wazi haiwezi kukwepa kila haina ya majukumu, kitu kikubwa hapa kinachotakiwa, kitu kikubwa ambacho kinahitajika juu ya suala hili ni kuwa na matumizi bora na kuweka mazingira mazuri kwa watumishi wetu. Kwa hiyo, mkakati wa uhakikika wa kubana matumizi kwa magari na rasilimali nyingine za Serikali ni usimamizi bora na kuwa na uongozi mzuri kwa kusimamia mali za umma pamoja na uwadilifu wa watumishi wetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea zaidi siyo vizuri kuzungumzia kubana matumizi tu kwa masuala ya magari wakati kuna sehemu nyingine nahisi tukiweza kuzi- *control* hizo tunaweza kubana matumizi zaidi na athari zake na zikaonea za mara moja. Natoa mfano wa Ligi Kuu inayoendelea sasa hivi, ligi ipo katika kingo za mwisho kumaliza, kuna vilabu ambavyo havitegemei nafasi ya aina yoyote wala hakuna mabadiliko yoyote ya kutegemea, hivi hatuoni haja ya hizi *game* nyingine kwa wale wasiokuwa na matarajio yoyote, kupangwa Mchana au Saa Nne Asubuhi kuepusha hili suala la kuharibu umeme wa bure, hii ni njia sahihi ya kuweza kubana matumizi ni lazima tuende na mipango, hili naomba Serikali ilizingatia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nielezee kidogo suala zima sekta ya utalii, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sintoweza kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi kwa kujitokeza wao wenyewe katika kutangaza vivutio vyetu vinavyopatikana ndani ya nchi vya utalii. Kweli kazi yaliyoifanya ni kubwa na Watanzania tunaheshimu, matunda

ya *Royal Tour* imeanza kuonekana. Kutokana na hilo lazima tuangalie kitu kimoja, dunia imebadilika watu wamejifungia ndani kwa muda mrefu, wamekaa *lockdown* watu wamejifungia ndani kwa muda mrefu, sasa hivi watu wamehamasika wanataka kutembea sehemu tofauti tofauti, kwa maana hiyo lazima Serikali iweke mipango mikakati ya namna bora ya kuwapokea wale watalii wanaoweza kuja hapa na kutaka kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizingumza hili kwa sababu utalii siku zote ni sekta ambayo haiwezi ikajitegemea yenyewe, kuna kilio kikubwa sana kwa yale maeneo ambayo yamepitiwa na sekta nzima ya utalii. Tunapozungumza sekta ya utalii, maana yake *Royal Tour* itakupa mfano halisi wa hiki ninachokizungumza kuimarika kwa utalii wa Tanzania bara ni kuimarika kwa utalii wa Tanzania visiwani. Vile ile *opposite* ya hilo kuimarika kwa utalii wa Tanzania Visiwani ndiyo kuimarika wa Tanzania Bara.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa kengele ilishagonga nilikuwa nangoja umalizie suala lako la utalii.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki nilimtaja Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga na Mheshimiwa Agnesta Lambert, ajiandae.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia bajeti hii ya Serikali lakini pia kuwawakilisha wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kushukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kutekeleza vizuri Ilani yake kupitia Mwenyekiti mahiri na hodari Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Pia napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Makamu wake, Watendaji wote wa Wizara kwa bajeti hii nzuri ya kimkakati ambayo imebeba maoni mengi ya Waheshimiwa Wabunge lakini pia inayokwenda kumgusa mwananchi wa Tanzania moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mapendekezo ya mapato na makadirio ya bajeti hii ya matumizi ya Serikali ya bajeti kama ilivyoainishwa. Kwanza kabisa Serikali na jamii ielewe kuwa kuwajenga wajasiriamali ndiyo tunajenga uchumi wa nchi, tunatengeneza ajira kwenye nchi yetu na kutambua sekta isiyo rasmi lakini kubwa zaidi kuwajenga wafanyabiashara na kuandaa wawekezaji ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwajengea uwezo wajasiriamali wetu nchini hususani wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam, hii asilimia 10 iliyokuwa inatolewa bado haitoshi na haikidhi matakwa ya wajasiriamali wa Taifa hili. Ukizingatia riba kubwa na masharti magumu ya kwenye mabenki, wajasiriamali wengi hasa wanawake walikuwa ni wanufaika wakubwa na walikuwa wanategemea sana mikopo hii pamoja na uchache wake. Hivyo basi pendekezo la kuigawa asilimia tano kupeleka kwenye miundombinu ya wamachinga binafsi siliungi mkono badala yake niiombe Serikali ije na mkakati maalum kama ilivyoongeza kwenye pato la bajeti ya kilimo basi iangalie na kwa upande wa wamachinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaiomba Serikali ije na tamko gani kuhusu mifuko 52 na zaidi ya kuwainua wajasiriamali kiuchumi na makundi maalum ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliiomba iundwe hapa baada ya kuhutubia Bunge hili. Je, mifuko hii inawasaidiaje wajasiriamali hawa kwani asilimia 10 haitoshi, mifuko mnajua ipo mingi lakini ni kweli inawasaidia wajasiriamali hawa na vijana na watu wenye makundi maalum? Tatizo kubwa la mifuko hii ni uwazi na upatikanaji wake wa taarifa katika makundi haya. Kundi kubwa la wanawake vijana na wahitaji wa makundi maalum hawana uelewa wa mifuko hii hakuna taarifa rasmi zinazoweza kuonyesha mifuko hii inapatikana vipi, utaratibu upoje, haina *website* hakuna *social media* dunia sasa hivi imebadilika taarifa ni kiganjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, basi tuiombe Serikali mifuko hii iwe wazi taarifa zitolewe, elimu itolewe tunayo *television* ya Taifa, tunazo redio, tuna mitandao ya kijamii taarifa ziwekwe ili wahusika waweze kupata taarifa na kutumia mifuko hii, kwa sababu uendeshaji wa mifuko hii gharama zake ni kubwa kuliko wanufaika wanaotakiwa kunufaika na mifuko hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niiombe Serikali iseme imefikia wapi kurudisha na kuboresha mfuko wa kuendeleza wajasiriamali wa nchi hii kupitia Benki Kuu *(SME Credit Guarantee Scheme)* ambao ulikuwa umesimamishwa tangu mwaka 2004. Hizi ni fursa zingine za kuwainua wajasiriamali hawa kuweza kujikita kwenye ajira, shughuli za uchumi kama ambavyo tunaona. Mfano, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alipoapishwa aliongea na wanawake wa Taifa hili kupitia hapa Mkoa wa Dodoma katika ajenda sita za Mheshimwa Rais ajenda mojawapo ilikuwa ni kuwahamisha akinamama kujikwamua kiuchumi kupitia vikundi na alisema natamani kuona wakina mama wanapata mikopo mikubwa

siyo hii midogo, anatamani kuona viwanda vya wanawake, miradi mikubwa itakayotengeneza ajira baina yao, sasa leo hiki kidogo kinachopatikana kikienda kupunguzwa kitaleta taharuki kubwa sana kwa akina mama. Tuiombe Serikali iangalie namna ya kuboresha zaidi hii asilimia 10 lakini mifuko hii inayoweza kusaidia wakina mama, vijana na watu wenye makundi maalum iwe wazi na isaidie kweli makundi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niiombe Serikali isamehe kodi na tozo ambazo ni lukuki kwa wajasiriamali wadogo. Kwa mfano, sasa hivi Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam kuna tamko limetoka kwamba vikundi vya wajasiriamali ambavyo vilishafanya *process* zote za kupata mikopo wapo kwenye foleni wameambiwa waanze upya kuomba kupitia mtandao, hivi kweli hawa wajasiriamali wadogo wangapi wanatumia simu janja? Kuandaa tu katiba hizi za kawaida kwenda *stationary* na kujaza hizi fomu ulikuwa ni mtihani mkubwa, watu wanahangaika imetuka sehemu kubwa sana kuweza kuwapa hii elimu mpaka hapa walipofika, sasa leo hii gafla zoezi linasitishwa watu wanaambiwa waende kwenye mtandao huku siyo kuwatendea haki wajasiriamali hawa. Niiombe Serikali wale wote waliokwishafanya taratibu zote utaratibu uendelee kama hili tamko linataka lianze, lianze baada ya hawa kuwa wamepata mikopo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwanini Serikali isianze na elimu kwanza tumepoteza fedha nyingi sana za mikopo ya akina mama ulipoanza huu utaratibu wa mikopo hii ya asilimia 10 watu walikuwa hawana elimu, wanapewa mikopo wanagawana wanatumia fedha hairudi na wengi walikuwa wanajua hii fedha ni bure, hawakupewa elimu ya kurudisha fedha hizi kwamba zinatakiwa zirudi zizunguke ili na wengine wapate. Sasa leo hii tunapokuja na matamko kama haya ghafla tu utaratibu unafungwa watu waende kwenye mtandao

ni wazi kwamba watakaoenda kunufaika ni wajanja wachache ambao wanajua mambo ya mtandao siyo wale ambao ni walengwa wa chini. Kwa hiyo niiombe Serikali tusirudie makosa yale ya mwanzo tutoe elimu kwanza, watu wapate elimu, waelewe jinsi ya kuomba mikopo hii kupitia hiyo mitandao ikishaeleweka basi ndiyo tufuate huo utaratibu, lakini isisitishwe ghafla wakati watu walishafanya taratibu zote, wapo kwenye foleni wanasubiri mikopo hii. Hii ni taharuki kubwa simu zimekuwa nyingi, wakina mama hawana amani wameshaanza kuona hii mikopo kama haiwahusu wao ni ya watu fulani fulani. Niiombe Serikali iliangalie hili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napendekeza utaratibu mzuri wa kuhusu hii mikopo uweze kuangaliwa, sawa mikopo hii ilikuwa inaanzia kwa Mtendaji wa Mtaa na Kata lakini pia ninaomba washirikishe Madiwani na Ofisi za Wabunge. Hiii itasaidia kupunguza wimbi kubwa la vikundi hewa lakini ufuatiliaji wa fedha hizi zisipotee. Mikopo hii inatoka kuna watu ambao wananufaika na mikopo hii siyo wahitaji. Tumeona mikopo inatoka kwa mtu mmoja unatoka mkopo mkubwa sana kiasi kwamba mkopo ule ungegawanywa ungeweza kusaidia hata vikundi 10 au zaidi ya 10 kwa kina mama. Kwa hiyo niombe utaratibu uangaliwe upya washirikishwe Madiwani zishirikishwe Ofisi za Wabunge ili tuweze kushirikiana kung'amua vikundi vipi ni halali vipi ni wahitaji husika lakini hasa ufuatiliaji wa hii fedha ili isiweze kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe pia Serikali yetu kupitia Benki Kuu iendelee kuweka mikakati madhubuti ya kushirikiana na mabenki ili kupunguza riba na masharti magumu kwa wajasiriamali. Tunatumia hiyo nguvu kubwa kuwaangalia wajasiriamali wadogo lakini kuna wale wa kati na wakubwa ambao bado wanahitaji msaada kupitia mabenki. Siyo wahitaji wote wanahitaji kukuza biashara zao au kufungua viwanda

kupitia mikopo hii midogo lakini wapo wanaotumia mabenki lakini tuangalie hizi riba za kuweza kuwasaidia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge kabla sijampa ruhusa mchangiaji niliyemtaja naomba niwatangaze wageni ambao wapo Bungeni jioni hii.

Kuna wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika ambao ni wageni wa Bunge ambao ni Uongozi wa *Dodoma Polytechnic Institute (DPI)* ambao ni Ndugu Joshua Daniel ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma na Fedha, karibu sana, tunae Ndugu Prince Matowo - Makamu Mkuu wa Chuo, Utawala na Miradi; Ndugu Saida Nassoro - Mkuu wa Idara ya TEHAMA, karibu; Ndugu Cuthbert Nziku - Mkufunzi Umeme, karibu; Ndugu Neema Mazuguni, Mkufunzi TEHAMA, karibu sana wageni hawa kutoka *Dodoma Polytechnic Institute*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao Viongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma na Mchungaji Christian Ndosa, Msaidizi wa Askofu, karibu sana Msaidizi wa Askofu; Ndugu Rodrick Lyimo, Katibu Mkuu wa Dayosisi; Ndugu Erick Makigi, Mtunza Hazina; Ndugu Batholomew Miyanga, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Rogathe Uronu, Mratibu wa Jinsi, karibuni sana uongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT). *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia hapa tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge kama alivyoelekeza Mheshimiwa Spika asubuhi, tunao wageni timu ya mchezo wa *draft,* mabingwa wa mchezo wa *draft* ambao ni wageni wa Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo pamoja na wageni wa Mheshimiwa Antony Mavunde hawa wote ni mabingwa wa mchezo wa *draft* ambao wamefanya mashindano na timu ya Mheshimiwa Antony Mavunde wamefunga magoli 19 kwa manne, kwa

hivyo wote ni mabingwa pia wageni wengine kama wapo wa Waheshimiwa Wabunge mnaweza kuleta ili tuwataje.

Pia kuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni viongozi pamoja na wanachama 140 wa Taasisi ya *Mzalendo Global Fund* ya Jijini Dodoma, wako hapo. Karibuni sana viongozi pamoja na wanachama wa Taasisi ya *Mzalendo Global Fund*, nawakaribisha nyote katika Bunge letu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Agnesta Lambert, nilimtaja, na baadaye Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tunajadili bajeti hii hatuna budi kufahamu kwamba bajeti hii haina tofauti na zile bajeti ambazo huwa tunazifanya katika *family level*. Nasema hivyo kwa sababu katika familia huwa tunakaa na kupanga bajeti kulingana na kile tunachokwenda kukipata, tulichonacho lakini na kile tunachodaiwa. Katika *family level* hiyohiyo ambayo naongelea haiwezekani ukapanga bajeti mwanzo mwisho ukasahau wanaokudai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mchango wangu wa leo utajielekeza katika maeneo makuu mawili kama si matatu. La kwanza nitakwenda kuchangia kuhusiana na mfuko wa bima wa afya. Ripoti ya *CAG* ya sasa imeeleza waziwazi namna ambavyo Mmfuko huu uko hoi taabani. Mfuko huu ndiyo mfuko ambao unagharamia huduma zote za afya kwa wanachama wake na kwa Watanzania kiujumla. Pale unapoonekana mfuko huu unayumba moja kwa moja afya za wanachama wa mfuko huu zinakuwa zimeyumba pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya CAG ya sasa inasema zipo sababu kuu tatu zinazopelekea mfuko huu kuyumba. Sababu ya kwanza ni malimbikizo ya michango ya wafanyakazi wa Serikali kutokupelekwa katika mfuko huu. Sababu ya pili ni Serikali kukopa katika mfuko huu pasipo kurejesha; na sababu ya tatu CAG anasema ni Serikali kukopa fedha kwenye mfuko huu bila utaratibu unaotambulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kuna changamoto ya Serikali kutokupeleka michango ya wafanyakazi wake kwenye mfuko huu. CAG anasema Serikali inadaiwa shilingi bilioni 8.76 ambayo ni malimbikizo ya wanachama hawa kwa maana ya wafanyakazi wa Serikali kwenda kwenye mfuko huu wa bima. CAG anaendelea kusema kuwa mfuko huu uko hoi taabani kwa sababu taasisi tatu za Serikali zimekopa fedha kiasi cha shilingi bilioni 98.47. Wakati CAG anafanya ukaguzi, mnamo Juni 30, 2021 fedha hizi zilikuwa hazijalipwa hata shilingi moja. Ikumbukwe nimesema kuwa mfuko huu ni mfuko unaoangalia afya za wanachama hao. *Which means* mfuko unapoyumba afya zinayumba, maendeleo yanayumba na hata utekelezaji wa bajeti unakuwa ni mgumu kwani afya zinakuwa haziko salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo CAG anaendelea kusema katika ripoti yake ya sasa, kwamba Serikali ilikopa shilingi bilioni 129.4 tangu mwaka wa fedha wa 2010/2011. Fedha hizi mpaka hivi tunapoongea katika Bunge lako hili Tukufu hazijalipwa hata shilingi moja. Kama haitoshi fedha hizi zilichukuliwa au zilikopeshwa kiholela; hakuna mkataba, hakuna kusainiana kwamba tumekopesha shilingi ngapi, kwa masharti yapi na ni lini kulipa. Sasa ninavyoongea fedha hizi ni miaka 10 Serikali haijalipa katika Mfuko huu. Nimeshangazwa sana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wakati anaelezea yote aliyoyaelezea hakuna sehemu yoyote

alipoelezea ni kwa namna gani mmejipanga kwenye eneo la matumizi kulipa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja katika hoja yangu ya pili. Hoja yangu ya pili inahusiana na utendaji wa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)*. Mambo haya ni mapacha; na katika hili naomba nitambue jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Mama Samia Suluhu Hassan kwa upande wa kuhakikisha yanakuwepo majengo ya hospitali, majengo ya zahanati na miundombinu yake kama jinsi ambavyo tumekuwa tukiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini majengo haya hayawezi kuwa na tija ikiwa katika hospitali na vituo vya afya hakuna dawa na vifaa tiba. Na vifaa hivi na dawa hizi haziwezi kupatikana kama hakuna fedha katika Bohari Kuu ya Dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati nachangia katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa 2022/2023 Novemba, 2021 nilionesha masikitiko yangu makubwa juu ya Serikali kutokulipa madeni ndani ya *MSD*. Nikasema, hii ni changamoto kubwa inayopelekea madawa na vifaa tiba kutokupatikana katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninavyoongea na wewe mpaka sasa hivi Serikali inadaiwa na *MSD* shilingi bilioni 303.861 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 73.861, kwa maana ya lile deni la awali. Hatuwezi kutegemea miujiza katika hili, kwamba tunajadili hapa mapato na matumizi, hatujadili namna ya kulipa madeni haya ili kuhakikisha *MSD* inajiendesha kama jinsi ipasavyo. Na maneno haya siyo ya kwangu, maneno haya ni ya *CAG* amesema *MSD* inashindwa kujiendesha kutokana na ukosefu wa fedha na akasema fedha hizi Serikali ikilipa *MSD* ina uwezo wa kusimama angalau ikaanza kutembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati Mheshimiwa Mwigulu anakuja ku-*wind up* kwanza atuambie, kwenye mapato na matumizi, kwa maana ya matumizi haya, ni namna gani Serikali imejipanga kwenda kuhakikisha inalipa deni hili la *MSD* lakini pia inakwenda kunusuru Mfuko wa Bima ya Afya ili wanachama na Watanzania waweze kupata matibabu wanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye suala la zima la Tume ya Haki za Binaadam. Nimemsikiliza Mheshimiwa Mwigulu, lakini pia nimepitia hotuba yake kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho sijaona sehemu yoyote ambapo Serikali inaongelea suala zima la haki za binaadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kabisa kwamba mwaka wa fedha unaoishia sasa Tume hii ya Haki za Binaadamu ilitengewa fedha kidogo sana mpaka tukapiga kelele sana. Tulitegemea kwenye bajeti hii angalau Serikali itafanya *budget reallocation* angalau katika bajeti ya maendeleo tuone kitu fulani ambacho kinaonekana pale cha kwenda kuwezesha Tume hii iweze kufanya kazi. Kwa masikitiko makubwa katika Tume ya Haki za Binaadamu fedha za maendeleo ambazo zimetengwa ni sifuri. Sasa Mheshimiwa Mwigulu wakati utakapokuwa unakuja hapa ku-*wind up* utuambie; inawezekana hapa kwenye eneo la maendeleo kwa upande wa Tume ya Hazi za Binaadamu huenda Serikali imekamilika vizuri sana, kwamba hatuhitaji magari, hatuhitaji Ofisi katika Mikoa, katika Wilaya, tumekamilika vizuri sana kila kitu kinachohitajika tunacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndiyo hivyo Mheshimiwa Mwigulu basi tutakupigia *big up* kabisa, lakini kama mahitaji yapo Mheshimiwa Mwigulu, leo hii unatuletea kwamba bajeti

ya maendeleo kwa upande wa Tume ya Haki za Binaadamu ni zero hii ni aibu kubwa sana. Na ni aibu siyo nchini lakini ni aibu hata kwa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kumalizia nimuombe Mheshimiwa Mwigulu atakapokuja hapa atuambie hivi ni kweli tume hii ipo au ni kama geresha fulani tumeiweka ili Umoja wa Mataifa waone kwamba Tanzania nao wapo wana chombo ambacho kinalinda na kinasimamia haki za binaadamu. Kwa sababu kama kweli tume hii ipo na inafanya kazi *there is no way out* ambapo mnatuambia mmetenga sifuri, sifuri, sifuri kwa upande wa bajeti ya maendeleo. Sasa Mheshimiwa Mwigulu *may be* inawezekana kwa sasa siyo kipaumbele kabisa, haki za Watanzania siyo kipaumbele kwa sasa, nalo utuambie. Lakini kama ni kipaumbele na unajua ni kipaumbele kwa upande wa Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa sababu amekuwa akipiga kelele usiku na mchana kutokana na uvunjifu wa haki za binaadamu. Lakini mnapokuja kwenye bajeti hamuonyi namna gani sasa tunakwenda kuisaidia na kuisaidia hii Tume iende kufanya kazi yake kwa ukamilifu vijijini ambako ndiko matukio mabaya kabisa ya uvunjifu wa haki za binaadamu unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeona nichangie kwa harahara ili niweze ku-*meet* hizi hoja zangu tatu. Lakini mambo yangu matatu nimesema madeni kutoka *MSD* mlipe na mtuambie kwenye matumizi hapa mmejipangaje. Lakini na lingine kule kwenye mfuko wa Bima ya Afya, wanachama wanashindwa kutibiwa, wanakwenda wanapewa *Panadol*, wanakwenda wanaambiwa hiki kipimo huwezi kupima; ni kwa sababu mmeshikilia fedha zao. Lakini Mheshimiwa Mwigulu zile fedha mlizozikopa bilioni 129 kwenda kujenga Hospitali ya Benjamin Mkapa, mlichukua bila Mktabata, mkachukua bila

utaratibu wowote, utueleze, utuambie ni lini mnazilipa na kama…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** …basi Hospitali hii ikabidhiwe kwenye Mfuko wa Bima ya Afya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Agnesta.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti na Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, ajiandae.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuruku kwa nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo anaendelea kufanya kazi kubwa ya kujenga Taifa letu. Kule kwetu Misungwi Rais amefanya mambo makubwa sana. Upande wa elimu, afya, maji, nishati na miundombinu ya barabara. Kusema kweli tunamshukuru sana kwa niaba ya wana-Misungwi wamenituma nifikishe salamu zetu za shukrani, tunashukuru sana kwa kazi aliyotufanyia wanamisungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie mambo matatu. Jambo la kwanza ni kuhusu barabara ya kutoka Mwanangwa, Bisasi mpaka Kahama. Barabara hii imesemwa tangu Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005, 2010, 2015 na 2020. Mheshimiwa Waziri sitaki kugombana na wewe mwaka huu, na

mwaka huu mimi nimesamehe. Barabara hii naomba uitengee fedha mwaka wa fedha ujao. Ninaweka oda mapeama kabisa ili tusigombane Mheshimiwa Waziri. Ninamuomba sana aandike kwenye *notebook* yake barabara hii iwe ni kipaumbele. Mwaka huu tumesamehe, tunaomba mwakani barabara hii iingie kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niizungumzie halali ya uzalishaji mali. Tumekuwa tukisema sana habari hizi, kwamba ili tuepukane na masuala ya kuagiza kila bidhaa kutoka nje ya nchi ni vizuri tuwekeze kwenye maeneo ya kimkakati, hasa ya kwenye uzalishaji mali. Tumekuwa tukisema sana; yako mashamba makubwa yaliyotelekezwa, yako mashamba unakuta shamba lina ekari 40,000 amepewa Mwekezaji ameshindwa kuliendeleza na badala yake analima ekari 200 kwenye elfu 40. Yako mashamba ya ngano kule Basutu Wilayani Hanang yameachwa, yako matrekta makubwa kama nyumba yametelekezwa, halafu bado ngano tunaagiza nje ya nchi, haya ni mambo ya kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali; hivi tunashindwa nini kuyafufua haya mashamba ambayo yameachwa kwa muda mrefu. Bado tunaagiza ngano, bado tunaagiza mafuta ya kula. Tunasema kuna vita; hivi tungekuwa tumezalisha mafuta ya kula ya kutosha ndani ya nchi hapakuwa na sababu ya kuagiza mafuta nje ya nchi. Sasa niombe Serikali kama kweli tuko *serious* na mambo haya hebu tufike mwisho maana yake tulimeshashauri sana habari hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaagiza nyama, yako mashamba ya ufugaji kule Simanjiro yametelekezwa, ukienda kule Misungwi kuna shamba zaidi ya ekari 40,000 linaitwa *Mwabuki Farm*, shamba la ekari za 40,000 lakini lina ng'ombe 100. Kama tumeshindwa, kama hatuwezi basi tuwekeze, na

mwekezaji akishindwa basi anyang'anywe yarudishwe kwa wananchi. Wananchi wanaozunguka maeneo haya wamekuwa wakitamani sana kuwekeza kwenye maeneo hayo lakini Serikali imesema inataka kuwekeza lakini hatuoni mwendelezo wa uwekezaji kwenye mashamba hayo. Sasa tunawezaje kuzalisha kama hatuwezi kuwekeza kwenye maeneo hayo ambayo ni ya kimkakati na yameachwa kwa muda mrefu? Kwamba Serikali imeyaacha, Wawekezaji wameyaacha, wananchi wameyaacha, kila mtu ameyaacha na kila mtu anamshangaa mwenzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunajua uwezo wake, uwezo wake ni mkubwa. Nina hakika mipango hii mnayoipanga ni mipango mizuri. Lakini shida moja tuliyonayo sisi Watanzania maneno ni mengi sana kuliko utekelezaji. Mheshimiwa Waziri akishapanga mipango hii mizuri wale wanaotakiwa kwenda kutekeleza mipango hii hawaonekani wanaishia kupiga maneno *story* zinaingilia huku zinatokea kule; hii kwa kweli haifai kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taifa lolote bila utafiti ni taifa lililokufa. Zipo Taasisi zetu ambazo tuliziweka kwa ajili ya utafiti. Kwa mfano Taasisi moja ya Ukiligulu; pale Ukiligulu wako watafiti ma-*Ph.D holders* wanafanya utafiti. Lakini hii miradi inapokuwa inadhaminiwa na wenzetu wa mataifa ya mbele wanapositisha huu ufadhili sisi Watanzania na Serikali yetu tumeshindwa kupeleka fedha kwenye maeneo hayo. Kinachotokea maeneo hay ana taasisi hizi za utafiti zinakufa. Leo ukienda Ukiligulu, Mtumishi mwenye *Ph.D holder*, mwenye *masters* anayetakiwa achakate aumize akili yake kwa ajili ya taifa lake anaishi kwenye nyumba ndogo kama jiko. Unaweza ukafika kwenye nyumba ya mtumishi huyo ukadhani ni chooni. Nyumba haijawahi kukarabatiwa miaka nenda miaka rudi, miaka zaidi

ya 30 haijawahi hata kupakwa rangi, mabati yanavuja, sakafu imeisha; lakini ndio wataalam ambao tunategemea waumize bongo zao kwa ajili ya Taifa letu, hiyo siyo sawa. Tutengeni fedha wapelekewe watu twende tukafanye ukarabati wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunatumia gharama kubwa sana, na kwa bahati nzuri nimemuona Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi yuko hapa; kama Taifa tunatumia gharama kubwa sana kuandaa askari wetu kwa ajili ya kulinda nchi yetu. Iwe JWTZ, iwe Polisi na Majeshi mengine. Na tunafurahi sana Wanajeshi wetu wanafanyakazi nzuri sana hasa ya kulinda mipaka yetu. Ziko Kamisheni nyingi ambazo tumekuwa tukituma askari wetu kwenda kusaidia mataifa ya jirani. Hatukatai, jirani akiwa na matatizo tumsaidie, haina mbaya; lakini jirani tunayemsaidia awe ni jirani anayejitambua; wako majirani hawajitambui.

*Inauma sana tunapopeleka askari wetu, vijana wetu wanakwenda kupigana vita zao wanarudi wamekufa; halafu wale wa nchi husika tunaowasaidia wao wala hawajali nchi yao wanaruhusu madini yao yanaondoka wao wako Tanzania wanatetema kifua, wanatetema mikono eti wamefunga magoli. Hizo nguvu wanazotumia kutetemeka kifua na mikono kwa nini wasibebe mtutu wa bunduki wasaidie mataifa yao ili dhahabu yao ibaki kwenye nchi yao? Hili siyo sawa. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi lazima mlione hili haya mambo ya mtu kuja kutetemeka Tanzania halafu ameiacha nchi yake inaibiwa dhahabu huko hiyo haikubaliki.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine…

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alexander, taarifa pokea. Mheshimiwa Kilumbe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alexander, pokea taarifa. Mheshimiwa Kilumbe.

**T A A R I F A**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelazimika kumpa taarifa mzungumzaji kwa sababu naona amekwenda nje ya mstari, kwa sababu mambo haya yanayohusu masuala ya uhusiano wa Kimataifa na masuala binafsi yanayohusu mtu kuchukuliwa kufanyakazi mahali pengine popote duniani, havihusiani. Naomba ajielekeze katika mchango wake juu ya bajeti yetu na aachane na mambo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, taarifa muhimu hiyo unaipokea?

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo sina shida nayo, wala siipokei. Naomba muda wangu ulindwe, na awe na nidhamu wenzake wanapochangia kama ambavyo wengine wamekuwa na nidhamu kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kusema hivi, Waheshimiwa Mawaziri nawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. Nawaomba sana, fanyeni kazi kwa mujibu wa Katiba, kwa mujibu wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, na kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi inasema nini. Yako maneno mengi sana yanasemwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pastory naomba usubiri. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa. Mheshimiwa anayechangia amepewa taarifa lakini naomba nitumie kanuni ya utaratibu. Maneno ambayo yamesemwa na Mheshimiwa Mbunge ni maneno ambayo ni hatarishi. Naomba kama itakupendeza, yaondolewe katika *Hansard*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alexander Pastory, naomba ufute hayo maneno ambayo umezungumza ambayo Mheshimiwa Waziri amethibitisha kwamba ni hatari, ingawa taarifa ya Mheshimiwa Kilumbe uliikataa.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yale ya kutetema, siyo! Basi nimeyafuta.

**MWENYEKITI:** Maneno yote ambayo yanalenga kuondoa uhusiano mzuri baina ya Tanzania na nchi nyingine.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni suala la kimtazamo. Kwa mtazamo wangu, naona kama maneno haya yalikuwa sawa, kwa sababu sijataja Taifa la mtu, sijamtaja mtu…

**MWENYEKITI:** Hapana, mimi naomba uyafute tu ili tuweke sawa *Hansard*.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba maneno hayo yafutwe ili *Hansard* ikae sawa sawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante nashukuru.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kupongeza sana Serikali yangu ya CCM na Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naiomba Serikali yangu, na kwenye hili naomba mnisikilize vizuri. Taarifa hizi hazina maana sana wakati mwingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, taarifa ni kwa mujibu wa kanuni zetu. Kwa hiyo, unahitaji uzipokee ama ukatae, lakini kwa ustaarabu.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mnisikilize vizuri. Nimesema natumia nafasi hii kuipongeza Serikali yangu ya CCM. Waheshimiwa Mawaziri mnafanya kazi nzuri. Naomba sana msiondolewe kwenye reli ya uchapakazi wenu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** …kwa sababu yako maneno mengine yanaweza kuwa ya kukatisha tamaa, na wako wengine inaweza kuwa ni *stress.* Sasa *stress* za mtu zisiwasababishe kushindwa kufanya kazi mkaondoka kwenye utaratibu. Naomba sana kwenye hili, mtu anapoongea pumba zake zisihusishwe na kabila analotoka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pastory Alexander.

Waheshimiwa, nilimtaja Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, na Mheshimiwa Maimuna Pathan, ajiandae.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii muhimu sana katika nchi yetu. Awali ya yote naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu, babu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba; nampongeza sana Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoendelea nayo katika kumsaidia Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea nayo katika nchi yetu. Mama huyu amefanya kazi kubwa, na kipekee kabisa amewaaminisha umma ya Watanzania na nje ya Watanzania kwamba mwanamke anaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Katika bajeti hii tuliyosomewa, Mama ameondoa ada katika kidato cha tano na cha sita. Hii inaonesha ni jinsi gani Serikali ya Awamu ya Sita ipo kazini kuhakikisha mtoto wa Kitanzania anapata elimu. Pia kuwaondolea wazazi na walezi mzigo mkubwa waliokuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, mama huyu amefanya kazi kubwa sana katika Mkoa anaotokea. Katika sekta ya afya amejenga vituo vya afya, amejenga zahanati, hospitali za wilaya na pia ameiendeleza Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere maarufu kwa jina la Kwangwa, sasa inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, hakuishia kwenye sekta ya afya; katika sekta ya maji Mama huyu ametuletea miradi mingi katika Mkoa wetu. Sasa tuna mradi wa Mugango, Kiabakari, ametuletea zaidi ya shilingi bilioni 70. Kuna mradi wa chujio la maji pale Bunda, ametuletea zaidi ya shilingi bilioni 10. Pale Musoma Mjini kuna miradi inaendelea, ametujengea tenki kubwa la maji, sasa liko katika hatua za mwisho, ametuletea zaidi ya shilingi bilioni nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama huyu hakuishia hapo, katika miradi hiyo sisi katika Mkoa wetu kuna wilaya zimeingia katika miradi ya vijiji 28; wilaya ya Serengeti, Wilaya ya Tarime na Rorya. Hii ni dhahiri kwamba mama amejipanga kumtua ndoo mwanamke wa Mkoa wa Mara. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mara, nasema ahsante sana mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nitagusia kidogo sekta ya maliasili na utalii. Tumemwona Mama akiitangaza nchi yetu kupitia filamu ya *Royal Tour* na amefanya vizuri sana na watalii sasa wako nchini. Mheshimiwa Waziri alisimama akatuambia, kuanzia sasa mpaka Desemba wageni wamekuja, hoteli zimejaa kule hifadhini. Nataka kushauri nini hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Watanzania wengi ambao wanatamani na wanapenda sana kutembelea hifadhi zetu. Kwa hiyo, naiomba hii Wizara iweze kuwa na mpango wa kujenga hoteli zenye bei ambazo Watanzania wataweza kwenda kulipa ili kuongeza kipato katika nchi yetu, na pia katika kumuunga mkono Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan katika kuitangaza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wenzangu, wanaume kwa wanawake waliosimama kuitetea hii asilimia 10 ya Halmashauri zetu. Tumemsikia Mheshimiwa

Mwigulu katika hotuba yake amesema wanawake wamekuwa ni walipaji wazuri sana katika mikopo hii. Nakubaliana naye, lakini sijui ni wapi aliona kwamba angeweza kuipunguza hii asilimia 10 kurudi katika asilimia tano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu zinapishana. Huwezi kuilinganisha Manispaa ya Ilala na Halmashauri ya Rorya, ni vitu viwili tofauti. Kwa sababu Manispaa ya Ilala mapato yake ni makubwa sana, lakini Halmashauri ya Rorya mapato yake ni madogo. Katika mapato ya mwaka mzima ambayo yanatengwa kwenye ile fedha ya Halmashauri, yaani ya makundi madogo ya vijana, wanawake na walemavu, asilimia inayotengwa kwa mwaka ni kama Shilingi milioni 100. Ile fedha, anayoihitaji Mheshimiwa Mwigulu ni asilimia tano, ambayo ni kama Shilingi milioni 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Shilingi milioni 50 anataka aichukue akajenge miundombinu ya barabara na masoko. Shilingi milioni 50 kwanza kwake yeye mwenyewe kwa mwaka mzima itajenga barabara ipi? Itajenga soko lipi? Ile Shilingi milioni 50 pia inayobaki kwa yule mama, kijana au mlemavu, haiwezi kuwa na tija. Kwa hiyo, naomba aliangalie hili ili waweze kuendelea kupewa ile asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwenye Halmashauri yake wanakubaliana na hilo jambo pale Iramba. Nina imani wanawake wote kwenye Halmashauri hizi hawawezi kukubaliana na hicho kitu. Pia, wanawake wa Mkoa wa Mara kwa unyenyekevu mkubwa sana tunaomba tuongezewe hiyo asilimia 10, yaani ibaki pale pale; au ikiwezekana iongezwe kutoka asilimia 10 kupanda juu. Hilo ndilo ombi letu sisi wana-Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusisitiza, miradi yote iliyopangwa fedha zake zitolewe kwa wakati. Naendelea kusisitiza tena, miradi yote itakayopelekewa fedha isimamiwe ili kuleta tija kwa Mheshimiwa Rais wetu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusisitiza kuwaambia Watanzania na kuwaomba tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, yuko kazini kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, tunaendelea na Mheshimiwa Maimuna Pathan na Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo ajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kupata nafasi ya kuongea siku ya leo. Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 kwa Mpango huu wa Tatu wa Miaka Mitano kwa kweli inatutia moyo sisi Watanzania. Nimeisoma vizuri, kwa kweli Waziri wa Fedha na Serikali kwa ujumla mmejitahidi sana. Mama yetu mama Samia Suluhu Hassan ameupiga mwingi kwenye bajeti hii. Amefanya mambo mengi sana mazuri. Ameongeza bajeti kwa asilimia kubwa sana, tunamshukuru sana mama yetu amefanya mambo mengi sana mazuri ambayo nikianza kuyaongelea sasa hivi, yatamaliza muda wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya CCM ya mwaka 2020 - 2025 kwenye Ibara ya 43 imeongelea kuhusu kuwaboreshea wavuvi maisha ili waweze kuvua vizuri, wafanye

kazi zao vizuri, wasipate matatizo yoyote. Pia nikinukuu kwenye bajeti yetu, *page* ya tatu, wamesema: "Mheshimiwa Spika natambua kuna maeneo yatakayogusa sheria na kanuni mbalimbali, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametuelekeza isiwepo sheria yoyote inayotumika kama kikwazo cha kuwaletea Watanzania ufanisi". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kanuni mbalimbali ambazo zinatumika kwenye uvuvi, zinawarudisha nyuma sana wananchi wetu ambao ni wavuvi. Ninavyofahamu, kama mnachukua maoni, yalitakiwa yachukuliwe kwenye vyama vingi vya uvuvi, lakini cha kushangaza, yamechukuliwa kwenye chama kimoja tu kinaitwa *UWAWANDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi, maoni haya yaliyotolewa na wale wavuvi yamelenga moja kwa moja kwenye uvuvi wa *ring net;* wao wametoa *suggestions* zao na pia wakatoa adhabu. Sidhani kama wao ni wanasheria. Wamesema kabisa kwamba hiki kifanyiwe hivi, kifanyiwe hivi na adhabu yake ni hii. Kinachoshangaza Serikali ikachukua kama ilivyo ikaweka vile vifungu; kifungu namba 66D(d) kwenye kanuni hiyo, na kanuni Na. 66F(f). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi hawa wanafanya kazi, wanajitahidi ili nao wapate kipato pamoja na familia zao. Wana maisha duni sana. Boti moja inachukua wavuvi kama 80 na wavuvi hao wanalipa tozo za Serikali; kila mmoja analipa leseni yake na chombo pia kinakuwa na leseni. Jambo la kwanza wanatuletea mapato kwenye Serikali yetu; jambo la pili, wavuvi hawa wanatunza familia zao. Wanaume wana wake zao, wana watoto wanawasomesha na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii inapowekwa kanuni ambayo inawabana watu upande mmoja, kwa kweli inasikitisha sana. Kuna kanuni inasema kwamba kuna katazo la kutumia *ring net* baharini wakati wa mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kanuni nyingine inasema ni katazo kutumia *ring net* baharini kwenye maji ya kina pungufu ya mita 50. Wakati huo huo, wale wa Ziwa Tanganyika wameambiwa wao wanatakiwa wavue zaidi ya mita 1,000. Huku ni kuwaonea watu kwa kweli. Unapowaambia watu wavue zaidi ya mita 1,000, sidhani kama inawezekana. Hawa wa baharini unapowaambia wavue zaidi ya mita 50, na wasivue mchana, sababu za msingi hazieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wanapata mapato yao kupitia uvuvi huo. *TAFIRI* ilitumwa ifanye tafiti baada ya kuonekana kuna sababu ambazo zimetolewa hapa za uvuvi huo. *TAFIRI* wameshafanya utafiti, lakini sielewi kwa nini majibu hayatolewi mpaka leo, wanazungushwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wanapata shida. Kuna sehemu, kazi ya uvuvi ndiyo kubwa kuliko kazi nyingine. Sehemu inayozunguka bahari, mito, maziwa, tunaomba kanuni hizi zirekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tarehe 17/6/2022 kuna Mbunge wa Kilwa, Mheshimiwa Ali Kassinge aliuliza swali kuhusu kanuni hizi. Naishukuru Serikali yangu Tukufu na Serikali yangu Sikivu, walisema wanazifanyia kazi kanuni hizi na watazibadilisha. Naomba nisisitize tena, naomba sana, kanuni hizi zitiliwe mkazo, kwa sababu wavuvi hawa, wanatuletea kipato kwenye nchi yetu, nao pia wanajiletea maendeleo kwa ajili ya familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hii kwenye miaka ya nyuma pia ilishawahi kuleta matatizo, lakini Mheshimiwa Rais, Marehemu Dkt. Joseph Pombe Magufuli alikuja baadaye, na baada ya kuliangalia sana akaruhusu waendelee na uvuvi *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kuu nililonalo kwa Serikali yangu Tukufu, sheria hizi wazibadilishe, kwa sababu zinabana baadhi ya watu. Naomba wafuatilie tafiti ambazo zimefanywa na *TAFIRI* na majibu hayo wayachukue, kanuni hizi zibadilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali yetu Tukufu kwa kuondoa ada kwa Kidato cha Tano na Kidato cha Sita, lakini tuna ushauri pia ambao tunaomba wauzingatie. Serikali ifanye tathmini kwenye vyuo vya kati kwa sababu kuna watoto wengi wanasoma pale wazazi wao hawana uwezo. Sisemei kwamba waingize kwa mwaka huu wa fedha, itakuwa ni ngumu, lakini ifanye tathmini hata kama ni mwakani na miaka mingine, nao wapate msamaha au punguzo ya zile ada ambazo zinatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukiangalia Chuo cha Mipango, mtu wa Diploma analipa Shilingi 800,000/=, lakini kuna Chuo cha *CBE* kozi kama hiyo hiyo mtu analipa Shilingi 1,300,000/=. Kuwepo pia na ulinganifu wa ada kwenye vyuo vya Serikali. Kwa sababu, wote wanachukua Diploma zinazofanana, lakini ada zinakuwa tofauti, na vyuo vyote ni vya Serikali. Basi kuwe na ulinganifu angalau, wafanye tathmini waone tukiweka Shilingi kadhaa itakuwa sawa kwa wote. Itasaidia sana wananchi wetu. Wananchi wengi ndio wanaosoma kwenye hivyo vyuo vya kati, lakini wazazi wao uwezo ni mdogo sana. Naiomba Serikali yetu sikivu itusaidie kwa hilo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunashukuru Serikali yetu kwa kuongeza bajeti kubwa sana kwenye kilimo. Bajeti ya kilimo ilikuwa Shilingi bilioni 294, imeongezwa mpaka kufikia Shilingi bilioni 954. Kuna tofauti ya Shilingi bilioni 700. Tunaishukuru sana na kuipongeza Serikali yetu. Tunachoomba sasa, kilimo cha umwagiliaji kitiliwe mkazo sana. Kuna mabadiliko sana kwenye tabianchi. Wananchi wanaweza wakajitahidi kulima lakini mvua zisiwe za kutosheleza. Tunaomba sana watilie mkazo kwenye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi ya kuongea, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Pathan. Tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, atafuatiwa na Mheshimiwa George Nathany Malima na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi wajiandae.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie katika bajeti hii. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na pia kutupa amani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa miradi na maendeleo makubwa anayoendelea kuyafanya katika nchi yetu. Pia, naendelea kumpa pongezi Mheshimiwa Rais, hasa kwenye hii *Royal Tour* kwa kweli, *Royal Tour* inaenda kutuletea manufaa makubwa na faida kubwa sana kwa Taifa letu na katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwa sasa tu hoteli zote mbugani zimejaa. Ukiachana na mbugani hata huku Dar-es-Salaam pia hali ya hoteli sasa inaanza kurudi katika hali nzuri.

Kwa kweli, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi hizo anazoendelea nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuchangia katika hili punguzo la *10%* kwa walemavu, akinamama na hata kwa vijana. Kwa kweli Mheshimiwa Mwigulu, kaka yangu, naomba nimwambie kwamba, hiyo sikubaliani nayo naungana na akinamama wengine na Wabunge wengine kwamba, hiyo haitakuwa na manufaa kwa akinamama wa Tanzania, kwa walemavu na kwa vijana. Kwa hiyo, hiyo naomba azingatie aweze kuiacha kama ilivyo ibaki *10%. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia kwenye Sekta ya Viwanda. Napenda kuiomba Serikali kutokana na mfumuko wa bei, tumeona mafuta yamepanda na bidhaa zote nchini zilipanda kwa ghafla ambapo ilileta taharuki kubwa. Kwa hiyo, sasa ushauri wangu napenda kuiomba Serikali na Wizara husika ya Viwanda na Biashara kwenda kubadilisha mfumo, hasa kwa wafanyabiashara binafsi. Kuna masoko kama Kariakoo, kuna wafanyabiashara ambao wana uwezo wa kuanzisha viwanda vidogovidogo na vya kati, wanao uwezo kabisa labda wa kununua kiwanda cha milioni 100, cha milioni 20 au cha milioni 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukienda kuwaelimisha vizuri wafanyabiashara hawa na kuwapa *confidence* na kuwajengea uwezo, wana uwezo kabisa wa kununua viwanda na kuanzisha viwanda. Shida iliyopo hawana *confidence* kwa sababu, Watanzania wengi hatujatoka kwenye sekta ya viwanda, hatujatoka kwenye familia zenye viwanda, kwa hiyo, hili jambo kwetu ni geni. Hata kama nina pesa najiuliza mara mbilimbili, pesa hii nimeipata labda kwenye mkopo nimefanya biashara leo nina kafaida kamilioni 50, leo nikatoe milioni 50 kununua kiwanda ambacho tangu nizaliwe sijawahi kumwona

mjomba wangu au kaka yangu au mama yangu akifanya biashara hii. Leo naenda kutupa pale milioni 50 au milioni 100, je, isiporudi nitakuwa mgeni wa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hapo Serikali iingilie kati kuona itawaelimisha vipi na itawajengea vipi uwezo wa kuamini na kujiamini kwamba, sawa, sasa kale kamilioni 100 kangu au milioni 10 yangu na mimi sasa nakwenda kifua mbele naagiza kiwanda changu kama ni China, India au popote pale. Kwa hiyo, viwanda hivi vikija kuanzishwa hapa tutapunguza sana suala la mfumuko wa bei, lakini vilevile tutapunguza *importation* na vilevile tutaongeza mapato kwa Serikali, lakini vilevile tutapunguza tatizo la ajira nchini kwetu. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mwigulu na Serikali kwa ujumla wazingatie mchango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda nichangie kwenye vitenge. Kwa kweli, suala la vitenge, kodi iliyopo kwa sasa hainiridhishi kabisa kwa sababu, nina mfano mmoja wa rafiki yangu au wafanyabiashara ambao wapo pale Kariakoo. Mwezi uliopita alikuwa ameagiza *container* lake akaleta, likafika bandarini kama mwezi mmoja na nusu umepita. *Container* la *20 feet,* amelipa *container* lile milioni 242 kama ushuru na pia akalipa *charges* ndogondogo za bandarini milioni 17, jumla ya malipo hayo ni milioni 259.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama huyo, mfanyabiashara huyo ni mwanamke, amepata hasara ya 98,672,000/=. Sasa kweli Serikali yetu inasema inaenda kuwa-*support* wanawake au wafanyabiashara, sasa hapa kweli kuna *support* au ni kumrudisha nyuma? Kama ana mkopo mama huyu si atapata *pressure* na kufa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, niiombe Serikali na kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu hili suala la vitenge kwanza ukweli kabisa wanapoteza mapato makubwa sana, kwa sababu wafanyabiashara ukimzibia njia hii anatafuta njia mbadala. Sasa tumefungulia njia za panya, lakini tungeangalia kodi gani ambayo inaweza ikawa *reasonable,* tungerudi hata pale kwenye *0.4%* angalau pale Waziri angekusanya mapato mengi sana ambayo sasa yanapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, tunaweza tukadhani tunasaidia labda viwanda vya ndani, lakini je, viwanda hivyo vya vitenge viko vingapi? Pia, hata hivi vitenge vilipokuwa vinakuja vile viwanda viliathirika na mauzo? Hapana, kwa sababu bado *demand* ni kubwa. Pamoja na kuongeza huu ushuru wafanyabiashara wanapata hasara wanatafuta njia mbadala kwa hiyo, Serikali inapoteza mapato makubwa sana. Niiombe Serikali ilifikirie hili jambo, pesa nyingi sana zinapotea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela. Nilimtaja Mheshimiwa George Natany Malima, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad wajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza napenda nimpongeze sana Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu. Sisi kule Mpwapwa kwa mara ya kwanza tumeshuhudia miradi mingi sana kila sekta. Upande wa maji kuna miradi ya kutosha, uko mradi mkubwa

wa milioni 500 ambao unatekelezwa pale Didilo, Kisokwe; lakini kuna mradi mkubwa wa maji wa bilioni 1.2 ambao unatekelezwa pia katika Kata ya Lupeta; na tunategemea kuchimba visima zaidi ya 10 katika vijiji mbalimbali katika Jimbo la mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa afya, pia tumejenga vitu viwili, vinaendelea kujengwa na ujenzi wake uko karibu asilimia 80 katika kata za kimkakati. Upande wa elimu pia tumejenga madarasa ya UVIKO-19, jumla yake madarasa 103, lakini pia tumejenga shule mbili za sekondari katika kata za kimkakati. Kwa upande wa mifugo tumepata majosho matano na yote yamekamilika. Kwa hiyo, napenda sana nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa ajili ya miradi hii ambayo inaendelea katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuweka nukta hapo kwamba, kipaumbele cha watu wa Mpwapwa ni barabara. Barabara kutoka Njiapanda ya Kongwa kwenda Mpwapwa Mjini kwenda Kibakwe na kutokezea Chipogolo. Barabara hii ni muhimu, nimeisemea mara nyingi, lakini naamini Serikali yangu sikivu itaendelea kulichukulia uzito wa kutosha jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba sasa nichangie bajeti hii nikianza na kuwapongeza sana *TRA*. *TRA* wamekusanya vizuri sana mapato ya ndani na hasa mapato yanayotokana na kodi, mapato yanayotokana na Serikali za Mitaa, lakini mapato ambayo hayatokani na kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka Aprili, *TRA* wamekusanya trilioni 19.99 ambayo ni sawa na asilimia 93 nawapongeza sana. Hata hivyo, napenda kutoa ushauri, bado kuna maeneo ambayo hatujafanya vizuri. Wako wafanyabiashara wachache

ambao sio waaminifu wanakuwa na bei mbili, wateja wakienda kwenye maduka yao wanawashawishi kwamba, ukitaka kununua bidhaa hii ukidai risiti bei yake ni hii, usipodai risiti bei yake ni hii. Kwa hiyo, wananchi wetu wana-*compromise* na wafanyabiashara wanaamua ku-*opt* kununua bidhaa bila kudai risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtindo huu tunapoteza fedha nyingi sana. Naomba sana *TRA,* Wizara na Serikali kwa ujumla tutoe elimu, kwanza kwa wafanyabiashara waelewe umuhimu wa kuchangia, kukusanya kodi ya Serikali, ili wawe na moyo wawe na nia hasa ya kutoa risiti kwa wanunuzi wetu. Pia wananchi wetu wafundishwe umuhimu wa kulipa kodi na hii itawasaidia kutoku-*compromise* na wafanyabiashara. Jambo hili ningeomba sana Serikali kupitia vyombo vya habari iendelee kutoa elimu ili hata hayo mapato machache yanayovuja kwa stahili hii yaweze kuwa *recovered.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni mafao ya wastaafu. Katika kipengele hiki naomba kuzungumzia habari ya kikokotoo. Katika hotuba ya Waziri amezungumza kwamba, kikokotoo wamependekeza asilimia 33.3 mstaafu atalipwa kwa mkupuo, lakini asilimia 66.7 itabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *amount* hii au asilimia hii ni ndogo sana. Sisi wote tunajua mstaafu anapostaafu anakutana na changamoto nyingi sana. Kuna mwingine wakati wa utumishi wake hakupata bahati ya kujenga kibanda, anapostaafu anataka atengeneze kibanda chake, lakini mwingine bado anasomesha, mwingine kwa umri ule wa kustaafu huwa kunakuwa na changamoto nyingi za maradhi, unaweza kukuta anaugua. Sasa fedha hii ya asilimia 33 inaweza kwisha hajakamilisha changamoto hizi, matokeo yake

tunawasababishia *stress,* tunawasababishia magonjwa ya moyo na hawadumu, hawaishi katika maisha marefu ya ustaafu, kwa hiyo, anaacha fedha zake zote kule zimebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri jambo hili liangaliwe kwa ukaribu sana. Kikokotoo kingerudi katika ile asilimia 50 au kama sio asilimia 50 basi angalau ifike 45 ili mtu huyu anapopata fedha hizi aweze kutatua matatizo yale, zile changamoto za kustaafu za mwanzo halafu abakize hata hela kidogo ya kufungua banda la kuuza hata nyanya au vitunguu kuliko amalize fedha yote halafu anabaki na msongo wa mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna shida katika eneo hili la wastaafu. Kuna shida ya usumbufu, wastaafu wetu wanasumbuliwa sana wanapoanza kufuatilia mafao yao, kuna ile nenda, rudi, nenda, rudi. Kule Mpwapwa nimekutana na *incidents* kama hizi nyingi sana, unakuta mzee amechoka, anaambiwa aende Dodoma arudi, nauli hana, fedha yenyewe kapata kidogo. Akikupa *documents* zake unakuta ama hazijakamilika au hazipo, hana *documents.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu huyu ambaye amestaafu hana *access* ya ofisi, hana *access* ya kujua michango yake imekwendaje. Unakuta mwingine hata michango haikwenda, imekwenda kidogo, lakini sehemu kubwa ya michango yake haikupelekwa na huyu unategemea aanze kufuatilia yeye michango ilipoenda. Kwa kweli, tunaleta usumbufu mkubwa sana kwa wastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kufuatilia, nimekutana na mambo haya; wastaafu wetu wengi habari zao au taarifa zao hazikukamilika na nimeenda kushangaa sana, Taifa kama

hili ambalo sasahivi tunatumia TEHAMA karibu kila taasisi, inakuwaje taarifa za mstaafu zisipatikane? Inakuwaje taarifa za mstaafu zisikamilike? Inakuwaje taarifa, michango ya mstaafu isipelekwe kule inakotakiwa kwenda wakati viongozi na wale wanaowasimamia wako pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jambo linaipata Serikali matope. Watu hawa wanazunguka, wamefanya kazi kwa muda mrefu katika Serikali yetu, lakini leo wamekuwa *marginalized,* wanaishi maisha ya kimaskini mno kwa sababu tu mambo yao hayakuwa yamewekwa vizuri na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kuzungumzia wafanyabiashara ndogondogo au wamachinga. Tumezungumza sana na tumeona miji mingi inachukua hatua mbalimbali, lakini bado eneo kubwa tunakosea kwa sababu, tunaenda kujenga miundombinu ya kufanyia biashara watu hawa mbali na mji, maeneo ambayo hakuna watu. Naomba nichukue fursa hii nimpongeze Mkuu wa Mkoa wangu wa Dodoma, Mheshimiwa Anthony Mtaka, amekuja na ubunifu wa hali ya juu sana, eneo ambalo ametenga na kujenga miundombinu kwa ajili ya machinga ni eneo ambalo lina watu, lina mlundikano wa watu na naamini bila wasiwasi wowote kwamba, baada ya kukamilika eneo lile wafanyabiashara hawa ndogondogo watafanya biashara yao pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba, hawa watu wana mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi hii, kama tutaweza kuwatengenezea mazingira ya kufanya biashara, lakini pia faida nyingine ni kwamba, miji yetu itabaki safi. Badala ya wafanyabiashara hawa kutapakaa kila mahali, lakini watakuwa na mahali pamoja, lakini ambapo pana watu wa kutosha kwa ajili ya kuuza bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lile la Dodoma liwe mfano, watu wengine tujifunze pale, liko katikati karibu na sokoni. Kwa hiyo, mtu akitoka soko kuu la Dodoma ni rahisi kufika kwenye *Machinga Complex* ile pale kwa hiyo, nampongeza sana Mkuu wa Mkoa na ningeomba watu wengine wote waige huu mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuchangia ni upande wa sekta ya kilimo. Nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ndugu yangu Mheshimiwa Bashe na Naibu wake Mheshimiwa Anthony Mavunde. Bajeti hii ambayo imeongezwa maradufu, labda mara tatu, naomba sana ikatumike katika umakini wake wote, ilete tija tuliyokusudia. Tija kubwa ya kwenye kilimo ni ajira, ni pamoja na ajira na usalama wa chakula katika nchi yetu. Kama bajeti hii sehemu kubwa itatumika katika kilimo cha umwagiliaji, kilimo ambacho kinavutia vijana wengi kuliko kilimo cha msimu itakuwa mkombozi kwa ajili ya shida kubwa ambayo ipo ya ajira, lakini pia uhakika wa kuwa na chakula katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Kilimo itumie vizuri fedha hizi ambazo Mheshimiwa Rais amezitoa kwa ajili ya kutaka kuongeza ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa George Nathany Malima. Tunaendelea na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti kuu ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Pamoja nayo nampongeza sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa bajeti hii inayogusa matarajio makubwa ya Watanzania, matumaini makubwa ya kuboresha maisha yao ya kijamii kwa sababu, bajeti imetaja maeneo mengi ya kuleta unafuu kwa maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza moja kwa moja kwa mifano hii kwamba, sasa Watanzania wategemee kwenye sekta ya elimu kwanza kuna kuboresha miundombinu ya elimu, lakini hili la wanafunzi kusoma bure kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita. Matumaini ni mengi kwamba, hata kwenye afya tunaendelea kujenga vituo vya afya kwa hela za tozo, lakini tumeona pia mpango wa miundombinu, tunaenda kujenga barabara nyingi pamoja na kuongeza mtandao wa barabara za lami. Pia hata kwa nishati, Watanzania wameweka matumaini makubwa kwamba, sasa vijiji vyote vitapata umeme, lakini sasa tunasogea kwenye vitongoji vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekeleza matumaini haya makubwa kwa Watanzania, lazima tuone namna gani tunapata makusanyo ya kutosha ya kwenda kutekeleza miradi hii ya maendeleo. Ni lazima tukusanye hii trilioni 41 tunayokusudia kuikusanya ndipo ambapo tutaenda kwenye kutekeleza miradi na kufikia matumaini makubwa ya Watanzania. Vinginevyo tutarudi hapa ndani tutacheza na sarakasi kama miradi mingine haitatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikubaliane na mpango huu na mkakati wa Serikali wa kwenda kubana matumizi ya Serikali. Nimshukuru sana Waziri kutuonesha. *Spirit*

hii, moyo huu wa kubana matumizi ya Serikali tulianza toka Serikali ya Awamu ya Tano ilipowafungua macho Watanzania kuhusu watumishi hewa ambapo walikuwa wanalipwa kwa kodi za Serikali, watumishi zaidi ya elfu 19 kuja kutolewa kwenye *Payroll* ya Serikali hiyo ilikuwa ni mifano mizuri tu na tuka-*save* mabilioni ya pesa za kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo. Tukaja kwenye wanafunzi hewa, lakini tuliweka vipaumbele pia katika kuadhimisha sikukuu za kitaifa tu kwamba, tulifanya kumbukizi hizo, lakini kwa kubana matumizi na hela nyingine zilienda kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru tu kabisa kwamba, Waziri amemulika sasa kwenye eneo hili la usafiri na usafirishaji, ameona kwamba, tunaweza tukabana matumizi kutoka bilioni 558 mpaka bilioni 50. Nampongeza sana, ni kitu kinawezekana, angetupa hata muundo wa mpango kazi tu kwamba, itakapofika Disemba pengine hata magari ya Serikali sasa yaanze kutumia gesi, ili tuone kwamba, tume-*save*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna pikipiki pia tumewapa watumishi wetu, hizi zitaenda kuwa mzigo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri. Naomba bado zikiwa mpya pia, hawa wakamilikishwe ili kuweza kuendelea kubana matumizi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tochi iliyotumika kama ni tochi kama ni Mwenge bado kuna mianya mingi ya kupoteza mapato ya Serikali, niombe tu Waziri aendelee kumulika. Kwa mfano, kwenye taasisi moja kununua tu *stationery* kwa vitengo tofauti kama ni *stationery* kama ni wino wa aina hiyo hiyo lakini utakuja kwa gharama tofauti. Vilevile tukiangalia miradi inayotekelezwa pengine na Wakandarasi mradi huo huo kama ukijengwa kwa *force account* utajengwa pengine kwa

gharama nusu ya hiyo. Hebu niombe tu Serikali waendelee kuangalia hiyo mianya ili tu-*serve* gharama ipelekwe kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu makusanyo yetu ya ndani bajeti kubwa inaenda kwenye matumizi ya kawaida kabisa, sehemu kidogo sana kama asilimia 33 ndiyo inaenda kwenye miradi ya wananchi. Sasa natamani kabisa siku moja tufikie nusu ya makusanyo yetu ambayo ni kodi za wananchi ikiwezekana ndiyo iende kwenye miradi ya maendeleo, lakini nusu ndiyo ingeenda kwenye matumizi mengineyo ya Serikali. Kwa hiyo niombe tu kabisa kwamba makusanyo yaongezwe, sasa pengine maeneo tunayopaswa kuyachagua kuwekeza ili tuweze kupata mapato ni sekta hizi za kiuchumi ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta zote hizi zinazo fursa kubwa tu kabisa ya kuweza kuleta mapato na kuleta mapinduzi makubwa kabisa. Kwa mfano nikienda kwenye kilimo, fursa kwenye kilimo ni kubwa sana, kwanza kama ni ardhi inayofaa kwa kilimo ni kubwa, tuna hekta zaidi ya milioni 44 ambapo tunatumia pengine asilimia 40, kuna asilimia kama 60 ya eneo linalofaa kwa kilimo bado hatujalitumia. Lakini tuna eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji zaidi ya hekta milioni 29 na yenyewe hata nusu yake hatujaweza kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fursa kubwa sana kwenye kilimo na ndiyo maana na fursa nyingine ni hii kwamba na Mheshimiwa Rais ameiona ametupa bajeti. Bajeti hii imeongezwa mara tatu ya bajeti tuliyoitumia mwaka jana, sasa tutegemee tu kwamba tupate mapato kutoka kwenye kilimo zaidi ya mara tatu ya bajeti iliyowekezwa na kwa ajili ya kuweza kupata mapato makubwa kutoka kwenye kilimo, lazima

tuchague maeneo gani sasa tunaenda kuwekeza tukitegemea kabisa kwamba kilimo cha Tanzania kinaendeshwa kwa namna mbili kuna wakulima wadogo, wanaotekeleza kilimo kwa asilimia 90 wakulima wadogo sifa zao tunajua wanafanya kilimo cha kujikimu ambayo ni *subsistence* kilimo na ambayo wanatumia zana duni kama jembe la mkono bado asilimia 64 wanatumia jembe la mkono, asilimia 24 ndiyo wanatumia wanyama kazi, na asilimia 12 ndiyo wanatumia trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wadogo ndiyo wanaoilisha Tanzania kwa usalama wa chakula kwa asilimia 100 na zaidi, sasa niombe tu Wizara kwa ajili ya wakulima wadogo changamoto zao ni pembejeo za kilimo, ikiwepo mbegu na mbolea, ambapo mbegu na mbolea gharama zake ziko juu na pengine hazipatikani kwa wakati wa msimu. Sasa niombe tu Wizara kuwasaidia wakulima hawa wadogo kwa habari tu za pembejeo za kilimo, mbegu zipatikane wakati wa msimu tena kwa bei ambayo wanaweza wakaimudu. Kwa habari ya mbolea kuna habari njema ni kwamba Serikali imeenda kutoa ruzuku kwenye mbolea Milioni 150. Kwa hiyo nawapongeza na ninaomba kwamba waipate kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kilimo cha wakulima wadogo kinaendelea tukitaka kuleta mapinduzi makubwa kwenye kilimo lazima tuende kwenye mashamba makubwa. Mashamba makubwa tuliyoyaacha tuliyoyatelekeza naomba tu Serikali sasa iyarejeshe lakini waendelee kutafuta mashamba makubwa mengine. Tulikuwa na mashamba makubwa kama 110 lakini lengo ni kufikisha mashamba 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba makubwa ni kilimo ambacho hakitegemei jembe la mkono na mashamba tunaenda ku-*mechanize,* ni mashamba ambayo yatatuletea pesa za kigeni, kwa sababu tutaelekeza kwa mfano tuna

mkataba wa kuuza labda mazao kama soya China, lakini tukiwa na mashamba makubwa tunajua tunaweza tuka-*control quality* na *control* ya mazao yanayotakiwa nje. Tunahitaji kupeleka mazao mengi ya kilimo nje ili kuweza kupata fedha za kigeni, tuongeze Dola za Kimarekani kutoka Bilioni 1.2 mpaka Bilioni Tano kwa sababu mashamba makubwa yanayo uwezo mkubwa na tuna uhakika yanazalisha na kwamba yana uwezo wa kuajiri watu wengi wakiwepo wataalam lakini pamoja na wasio wataalam. Kwa hiyo, kilimo cha mashamba makubwa ni kipaumbele tuwekeze hilo ili tuone manufaa ya bajeti iliyoongezwa kwenye kilimo tuone kwamba tunapata mavuno ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika ufanisi sasa wa sekta hizi za kiuchumi mimi nichangie tu kwamba, sekta za kiuchumi tumeongezea fedha kwa mfano kilimo na mifugo watekelezaji wa miradi ya kilimo na mifugo wako Halmashauri wako TAMISEMI, lakini utaratibu mwingi na miradi mingi inasimamiwa na Wizara. Mara ya mwisho Mheshimiwa Bashe wakati anatoa hotuba ya bajeti yake alieleza vitu kwa mfano, Wizara ina nia njema imejenga labda *Ward resources center* ziko Halmashauri, ikifika kule inaenda kubadilishwa pengine matumizi hii ni kwa sababu Wizara inayobuni miradi na Wizara inayoenda kutekeleza miradi iko tofauti na utekelezaji wake wapo Wizara tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kama tunataka ufanisi mzuri, ufuatiliaji wa miradi hii ya kilimo mifugo na zingine *either* hao Maafisa Kilimo au Watendaji wa miradi hiyo warudi kwa Katibu Mkuu wa Wizara husika au kule TAMISEMI tuweke sasa kiungo kama ni Katibu Mkuu au Naibu Waziri kama ilivyo kwenye Wizara za Elimu na kama ilivyo kwenye Wizara ya Afya ili ufuatiliaji huu uwe mzuri na kwamba tuweze kupata kipato kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuchangia ni habari ya *restructuring* ambayo iko Halmashauri ya kuunganisha Wizara za Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mwongozo wa Spika.

**MENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe subiri nitakupa baadae, tunaendelea na nilimtaja Mheshimiwa Juma Usonge Hamad.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa ya kuweza kusimama na kuchangia kwenye hotuba hii ya Serikali Kuu. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, kazi ya kuimarisha Muungano, pili kuinua uchumi wa nchi yetu kupitia nchi lakini kupitia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuimarisha uchumi wa Zanzibar lakini pia nimtie moyo Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya aendelee kufanyakazi vizuri zaidi na kutuletea maendeleo Wazanzibar. Baada ya kusema hayo machache sasa nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na bajeti hii ambayo imejikita zaidi kwenye makadirio pamoja na matumizi, yapo mambo makubwa ambayo yamefanyika, yapo yanaendelea kufanyika, kwa hiyo tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Kwenye bajeti hii kuna tozo

mbalimbali ambazo tayari zimependekezwa, tozo hizi zinaenda kufutwa moja kwa moja lakini ziko tozo nyingine zinaenda kupunguzwa zaidi, kwa hiyo niipongeze sana. Tozo zikipunguzwa maana yake tunatengenezewa mazingira mazuri sisi kama Watanzania namna ya kulipa kodi pia kupunguziwa unafuu wa kulipa kodi kwenye bidhaa zetu ambazo zinapatikana kwenye viwanda lakini na zile ambazo tayari tunazizalisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kuna gharama za mifugo pamoja na nafaka ambazo zinatoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar, nilitegemea sana kwenye bajeti hii tutaangalia namna gani kwenda kuzipunguza tozo hasa zinazoumiza wananchi wa Zanzibar ambao wananunua bidhaa kutoka huku bara. Kwa mfano, tunazo bidhaa za nafaka kama mchele, maharage na bidhaa nyingine, lakini pia tunazo bidhaa za mifugo. Sasa hivi ukinunua mifugo ukiitoa Tanzania Bara kuileta Zanzibar ni ghali sana na ndiyo maana ukichukulia kwa mfano kama kilo moja ya nyama kwa upande wa Zanzibar sasa hivi ina-*range* kuanzia shilingi 7,800 na kuendelea, lakini kwa Bara ni pesa ndogo, naiomba sana Wizara tuangalie namna gani Mtanzania wa Zanzibar tukampunguzia gharama ya tozo ili aipate bidhaa hii kwa bei nafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mfano mzuri ukienda Zanzibar nyama inaliwa kipindi cha Sikukuu, inaliwa kipindi ambacho kuna harusi na jambo jengine lolote lile, lakini siku za kawaida huwezi kumkuta Mtanzania wa Zanzibar anakula nyama hii yote inasababishwa na gharama kubwa. Gharama hizo kuanzia kwenda kununua kuna tozo, kuna tozo za vibali za usafirishaji, kuna tozo za vibali kupitia Wizara ya Mifugo, kuna tozo za *customer duties* kupitia bandarini, zote hizo anazilipa mfanyabiashara wa Zanzibar ambae anachukua bidhaa

kutoka Bara kuzipeleka Zanzibar. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara tuangalie kumpunguzia Mtanzania ambaye yupo Zanzibar lazima tuziondoe hizi gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi moja, leo hii ndiyo maana utakuta wafanyabiashara wengi wananunua bidhaa kutoka nchi ya jirani kuzileta Zanzibar lakini Bara huku hawawezi kununua sababu ya tozo hizi ni kubwa ndefu na nyingi kabisa, tunaiomba sana Wizara tuangalie namna ya kuzifuta hizi tozo zote ili mradi zikifika Zanzibar basi hizi bidhaa za nafaka, nyama pamoja na vitu vingine hivi mtu anazipata kwa bei nafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye upande wa pili nitazungumzia suala la mwani. Tukifungua Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi 2020/2025 kwenye Ibara ya 45(m) ambacho kinazungumzia naomba uniruhusu ninukuu kifungu hiki kidogo cha (m) ambacho kinazungumzia kwamba "kuwawezesha wakulima wa mwani hususani vikundi vya akinamama, vijana ambao wanakaa mwambaoni mwa bahari kuwaongezea uzalishaji wa tani 1,400 hadi 1,500 za zao la mwani" lakini Ilani hii imeendelea pia zaidi kuzungumzia kwenye Ibara ya 162 Kifungu cha (c) kuwa, Tanzania inataka kuweka kituo cha uvuvi pamoja na mazao ya bahari ikiwemo zao hili la mwani, lakini Kifungu (d) pia kutumia mazao ya baharini ikiwemo samaki, mwani na chumvi kama chachu ya maendeleo ya viwanda. Kwa hiyo tunayo fursa kubwa sana Watanzania kwenye zao la mwani tukilipa kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la mwani kama zao jingine la korosho pamoja na karafuu bado hatujaangalia fursa, miongoni mwa majukumu ya Wizara hii moja *to collect revenue,* pili; *how to make the expenditure*, tatu; *how to make the policy to the Government,* yote ni majukumu yetu hayo. Wizara hii

imepewa mamlaka na jukumu la kukusanya mapato lakini pia kuvumbua vyanzo vingine vya mapato. Kwa hiyo kwenye suala la mwani una *value* kubwa sana, zipo nchi ambazo zimeendelea na zimepiga hatua kwenye suala hili la mwani ikiwemo Indonesia pamoja na Ufilipino, nchi hizi zimepiga hatua kubwa sana na zinachangia pato kubwa sana la Taifa kupitia mwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwani una faida kubwa sana mbali ya kupeleka viwandani lakini unatumika kwa matumizi mbalimbali likiwemo kwenye suala la vyakula, mle kuna *ice cream,* kuna *chocolate,* kuna siagi, pia kwenye suala la vipodozi kuna vipodozi mbalimbali *cosmetic products,* kuna mafuta ya kujipaka mbalimbali. Mwani pia unatumika kwa madawa ambayo yanatumika kwa binadamu na kutibiwa Wanyama, zote ni faida za mwani. Naiomba sana Wizara hii tuliangalie zao la mwani tulizidishie thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mwani thamani yake ni ndogo sana ndugu zangu, sasa hivi mwani unanunuliwa na makampuni zaidi ya 18 Zanzibar pamoja na Bara, sitaki nilizungumze hili kama kuonekana zao hili la Zanzibar Hapana! Tuna Mikoa zaidi ya mitatu Tanzania Bara, Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Tanga pia, Mikoa yote hii inavuna mwani na kuna zaidi ya asilimia 99 ya akinamama ambao wako kando kando ya bahari wote wanajishughulisha na kuuza huu mwani. Mwani unauzwa nchi za nje sisi kama Taifa inabakia asilimia moja tu ndiyo tunauchakata kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara ya Biashara lakini pia nawapongeza sana vijana wetu wa *TIRDO* wamefanyakazi kubwa mno, lakini tunao vijana wetu wa *TANTRADE* na wao pia wamejitahidi kufanyakazi mno ingawa

bajeti zao tunazijua ni ndogo, bajeti zao ni ndogo lakini wanajitahidi kufanyakazi kubwa za kuwasaidia wananchi kule kando kando ya bahari. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara tuliangalie hili zao la mwani. Zao la mwani lina faida kubwa sana, kama nchi tunaweza tukapata kipato lakini pia tunatengeneza ajira kubwa sana ya akinamama ambao wanakuwepo kando kando ya bahari kule Zanzibar pamoja na huku Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na changamoto mbalimbali ambazo wanapitia wakulima wetu wa mwani, mojawapo mitaji yao ni midogo gharama kubwa sana wanazozitumia kwa ajili ya kuzikuzisha hili zao la mwani, pia kuna *connection* ndogo sana ambazo wanazozipata hawa kwa ajili ya kuunganishwa na matamasha mbalimbali ya biashara kwa ajili ya kuziuza bidhaa zao hizi ambazo tayari wanazizalisha. Pia bidhaa ambazo wanazizalisha hizi ndogo kwa asilimia moja, zinaharibika kwa muda mfupi kwa sababu hakuna teknolojia ya kutosha. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara tuliangalie hili zao la mwani kwa litaingiza faida kubwa sana na linaweza likaingiza fedha za kigeni, mbali na fedha za kigeni pia itaongezea bajeti yetu japo asilimia 18 na kuendelea kwenye hili zao la mwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba sana Wizara kama suala la kuanzisha viwanda litachukuka muda mrefu, basi huu ununuzi wa mwani tuwaachie wenzetu wa stakadhi ghalani kupitia Wizara ya Biashara wanunue mwani huu *then* watafute masoko ya nje, hii itapunguza sana huu ukiritimba ambao unafanywa na wanunuzi wa mwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo makampuni zaidi ya 18 *still* bei ya mwani ni ndogo, mwani sasa hivi unanunuliwa kwa kilo shilingi 800, shilingi 600 lakini nje huko mpaka dola tatu sasa

hivi unanunuliwa huko maeneo ya Indonesia pamoja na Ufilipino lakini kwa Zanzibar pamoja na Tanzania bado hatujaona. Pia, naomba sana huu mfumo wa stakabadhi ghalani utasaidia sana kuliongezea thamani hili zao letu la mwani na tutakuwa tumewasadia sana wakulima wetu wa mwani, sasa hivi wameshakata tamaa kwa sababu hakuna *connection* nzuri kati ya Serikali na wakulima wenyewe, wanaachiwa tu sasa hivi wafanye wanavyotaka wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze sana wenzetu hawa wa Wizara ya Uvuvi akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri Abdallah Ulega, nitakuwa nimefanya makosa makubwa sana nisipomtaja, anajitahidi sana kufanya *connection* na kuwasaidia sana wakulima wa mwani, kuwasaidia taitai pamoja na kamba, lakini bado inaonekana mwani *value* yake ni ndogo katika soko. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali bajeti ijayo lazima tuhakikishe kwamba mwani huu tunauongezea thamani lakini tunatafuta viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza zao la mwana lina faida nyingi kama chakula, madawa na kutuumika kama vipodozi na mambo mengine utatuingizia faida lakini utatengeneza ajira nyingi kwa Watanzania pamoja na Wazanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba sana Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania washirikiane na wenzao wa Zanzibar wahakikishe kwamba tunatafuta wawekezaji ambao watakuja kujenga viwanda hapa nchini Tanzania, mwani ukinunuliwa Bara ukinunuliwa Zanzibar yote ni nchi moja na bei itakuwa ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 76 kuomba mwongozo wako juu ya tukio au majadiliano yaliyopita muda mfupi, wakati Mheshimiwa ndugu yangu na Mbunge mwenzangu Alexander Mnyeti alipokuwa akichangia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama kutoa taarifa kumpa Mheshimiwa Mbunge mwenzangu na nia yangu kubwa katika taarifa ile ilikuwa ni kutaka kumwonesha kwamba atenganishe kazi ya Jeshi letu ya kwenda kulinda amani katika nchi jirani na kazi za michezo au mikataba ya wanamichezo wanaoingia na vilabu mbalimbali hapa nchini kwetu, ndiyo ilikuwa lengo langu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yapo duniani kote hata tulipokuwa vitani mwaka 1979 tulipovamiwa na Nduli Iddi Amin siyo Watanzania wote walikwenda *front line,* wapo wengine waliendelea na shughuli zao mbalimbali na wengine walikuwa katika mataifa mengine ya nje wakifundisha kama Walimu, wakifanya shughuli za michezo na nyingine. Hata sasa hivi vita inapoendelea ya Ukraine na Urusi wapo Warusi wako nje ya nchi wanafanya kazi zao nyingine za kitaaluma na wapo Ukrainians wapo nje ya nchi yao wakifanya kazi zao nyingine za kitaaluma. Maana yangu ni nini kwamba, kazi ya Jeshi ni kazi ya taaluma na wanaifanya wale ambao wanautaalam nayo na wananchi wengine wanaendelea na kazi zao za kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotoa mwongozo huo ulielekeza Ndugu yangu aukubali au kuukataa, alipoukataa aliongeza maneno haya ambayo kwangu mimi nimeona siyo maneno ya Kibunge na kwa kweli yalikuwa hayanipi hadhi na heshima kama Mbunge mwenziwe. Alisema hivi ''…..awe na nidhamu wenzake wanapochangia kama wenzake wanavyokuwa na nidhamu yeye anapochangia''. Kitendo cha kumuongoza mwenzangu na mwongozo uliowekwa kwa mujibu wa Kanuni zetu haumvunjii yeye heshima, bali ulikuwa na nia ya kumwongoza ili Bunge kumbukumbu zetu zikae sahihi hasa katika jambo hili kubwa ambalo linahusu diplomasia ya nchi yetu na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niliona maneno yale aliyoyamalizia yalikuwa ni maneno ambayo siyo ya Kibunge na yananivunjia heshima, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda amesimama kwa Kanuni ya 76, ambae ameomba mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea muda siyo mrefu ambalo sina haja ya kulirudia amelieleza kwa uzuri kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 77 itabidi niisome leo kwa sababu hili jambo limekuwa likijirudia Kuhusu Taarifa. Kanuni ya 77(1) inasema Mbunge yeyote ninanukuu ''Mbunge yeyote anaweza kusimama mahala pake na kusema Taarifa na kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa au ufafanuzi kwa muda wa dakika zisizozidi mbili kwa Mbunge anayesema, ambapo Spika atamtaka Mbunge anayesema aketi kusikiliza Taarifa hiyo. Kanuni ndogo ya (2) inasema; ''Mtoa taarifa atakapomaliza kutoa taarifa na kuketi, Spika atamuuliza Mbunge aliyekuwa akisema mwanzo kama

anaikubali au haikubali taarifa hiyo kabla ya kumruhusu kuendelea kuchangia hoja'' mwisho wa kanuni kuhusu Taarifa.

Kwa hiyo, ni kupokea, kuikubali ama kuikataa bila kutoa maelezo ya ziada ambayo yanaweza kuharibu hiyo taarifa ambayo imetolewa. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda anacholalamikia ni kwamba Mbunge ambaye alikuwa akichangia Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti amekiuka Kanuni ya 71 ambayo naomba pia niirudie kwa faida ya wote na hili jambo lisiweze kujirejea tena.

Kanuni ya 71(1) inasema; bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge naomba niziache zote niende 71(1), (j), Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine, lakini na (k) chini yake inasema hatafanya vitendo vya ujeuri au uchokozi.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili limekuwa likirejea na Mheshimiwa ambaye amekataa leo taarifa kwa namna alivyokataa amevunja Kanuni pia. Kwa hiyo, sijui kama yupo hapa?

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Ilitakiwa aombe radhi kwa sababu amevunja Kanuni na ameleta maudhi kwa Mbunge mwenzake. Kwa vile hayupo na nilishasema pale kwamba iondolewe kwenye *Hansard,* kwa hiyo na taarifa ambayo ameikataa, maneno yote aliyosema yaondolewe kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tumeelewana kwa mwongozo huo naamini kabisa wengine watajifunza na wataendelea kuheshimu Kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu kamili Asubuhi.

*(Saa 1.43 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 24 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*